Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Nne – Tarehe 16 Juni, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawajibika kusema kwamba ukumbi huu ni salama kabisa kwa hali zote, leo hii ni siku ya kwanza tumekutana kama Bunge tangu uvumi kuhusu yanayodaiwa matukio humu ndani ya Bunge ambayo mimi kama Spika niliarifiwa siku ya Alhamisi tarehe 12 mwezi huu, yaani wiki iliyopita siku ya Bajeti. Sasa naomba nitoe taarifa rasmi ili tusiendeleze uvumi na kuleta hali ambayo inaweza kuwatia mashaka, siyo ninyi tu Waheshimiwa Wabunge, lakini wananchi wote hapa nchini.

Taarifa niliipokea toka kwa Katibu wa Bunge siku ya Alhamisi mchana kabla tu ya kuingia kusikiliza Hotuba ya Bajeti na taarifa inasema kwamba, siku ya Jumanne usiku maana yake hata tarehe na muda umekuwa ukisemwa kwa namna tofauti. Siku ya Jumanne, usiku wakati Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wakiwa kwenye *caucus,* katika mkutano wao wa chama.

Waheshimiwa wabunge, moja ya kamera za usalama zilionyesha kwamba kuna watu wawili mmoja akidhaniwa ni Mbunge na mwingine akidhaniwa kuwa ni Afisa ambaye ni mtumishi wa Bunge, waliingia humu majira ya saa mbili na dakika kumi usiku wa siku ya Jumanne na inasemekana kwa kuangalia hiyo kamera yenyewe kwa sababu kamera inaendelea kurekodi, wakaona kwamba watu hao walitanga tanga ndani ya ukumbi huu na mmojawao alionekana kama mkono wake una dalili ya kutupa vitu fulani humu ndani.

Waheshimiwa Wabunge, nalisema hili sasa, mimi binafsi wala ofisi yangu hatuna kabisa imani ya kishirikina. Niliunganishe na hili, baadaye Mheshimiwa Victor Mwambalaswa Mbunge wa Lupa akaniandika barua hapa mezani sasa wakati bajeti inasomwa kwamba Mheshimiwa Mwakyembe amechukuliwa na yeye amemsaidia kuondoka ndani ya ukumbi na kumpeleka kwenye kliniki.

Waheshimiwa Wabunge, jioni hiyo sasa kwa kuyaunganisha haya mawili nikaona nina wajibu wa kushirikisha vyombo vya usalama kwa sababu kwanza kama kweli kimetupwa kitu acha hayo ya ushirikina, hicho kitu kinaweza kuwa ni sumu za kisasa, sasa na hapa ndio Serikali ipo na sisi Wabunge. Kwa hiyo, ikawa siyo kitu cha kuupuza na nisingeweza kuongea nanyi kwa sababu nilikuwa nasubiri jioni hiyo niweze kupata maelezo zaidi.

Siku ya pili kama mnavyofahamu Ijumaa haikuwa siku ya Bunge ilikuwa ni siku ya kupumzika, leo ndio tunakutana. Katikakati ya hapo vyombo vya habari kwa kutimiza wajibu wao kwa wananchi wakaendelea kuniuliza maswali, ni bahati mbaya katika baadhi ya majibu ofisi ilijibu kidogo tofauti lakini ni hali halisi tu ya jambo lenyewe.

Kwa hiyo, Ijumaa hiyo hiyo idara za usalama na polisi na usalama wa Taifa walifanya ukaguzi wa makini sana kuhakikisha kwamba ukumbi uko salama, hilo lilifanyika na kufikia Jumamosi timu nzima ya hao walioifanya kazi hiyo walikuja kunieleza nyumbani kwamba ukumbi uko salama kwa matumizi.

Kwa hiyo nilikuwa nataka nitoe taarifa hiyo kwamba sasa tusubiri tu. Kwa nini linachukua muda kidogo? Linachukua muda kidogo kwa sababu inabidi katika mashine zinazorekodi (kamera zinazorekodi), warejee kule kwenye chombo kinachohifadhi kumbukumbu iangaliwe vizuri siyo tu kuanzia Jumatatu, waangalie kiasi cha saa 72 za mtiririko wa mambo na kuziweka katika *CD*. Ni sehemu tu ya uchunguzi ili kuweza kujihakikishia.

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge tuko salama lililopo tu ni kwamba tuuchukulie huu kwamba ni uvumi tu hadi hapo taarifa nyingine itakayotolewa baadaye. Ninawashukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, iko taarifa ya ziada. Katika Mkutano wetu wa kumi na moja Bunge pamoja na shughuli nyingine ilipitisha Miswada ya Sheria ya Serikali saba ambayo ni *the Petroleum Bill*, 2008 namba nne wa 2008, *the Financial Leasing Bill*, 2008 namba tano wa 2008, *the Ant Trafficking in Persons Bill*, 2008 namba sita wa 2008, the *UNESCO National Commission Bill*, 2008 namba saba wa 2008, *the Social Security Regulatory Authority Bill*, 2008 namba nane wa 2008, *the Financial Laws Miscellaneous Amendment Bill,* 2008 namba tisa wa 2008 na the *Electricity Bill*, 2008 ambayo ni namba kumi wa 2008.

Miswada hiyo niliifikisha kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ili ipate kibali chake baada ya kupitia katika hatua zake zote za uchapishwaji, ninafurahi kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba Mheshimiwa Rais ametoa kibali chake na sasa Miswada hiyo niliyoisoma ni sheria kamili za nchi yetu. (*Makofi*)

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mezani Taarifa ya Utendandaji na Hesabu za Bodi ya Pamba zilizokaguliwa kwa mwaka 2006/2007 (*the Annual Report and Audited Accounts for the year ended 30th June, 2007).*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 na mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI – MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni na Msemaji Mkuu wa Upinzani Bungeni wa Wizara ya Fedha na Uchumi Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, napenda kuwasilisha mezani Taaarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Fedha na Uchumi juu ya Hali ya Uchumi wa Taifa na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo na Mfumo wa Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2008/2009, pamoja na Makadirio na Matumizi ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 30

**Kupuuza Maamuzi ya Bunge**

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO** aliuliza:-

Kwa kuwa, wakati Serikali inapojibu maswali ya Wabunge Bungeni, hufanya hivyo kwa mjibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za Nchi; na kwa kuwa majibu yao ndio mwongozo wa Serikali lakini wakati mwingine majibu hayo huwa yanapuuzwa na

mamlaka nyingine za nchi kwa kisingizio kuwa mamlaka hizo zina kanuni zake na haziwezi kufuata kauli za Bunge:-

Je, mamlaka inayokataa kutekeleza au kupuuza maamuzi ya Bunge wachukuliwe hatua gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama alivyoninukuu Mheshimiwa Mbunge katika swali lake la msingi kwamba Serikali huwasilisha Bungeni majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge kwa kuzingatia Katiba, Sheria na Kanuni za Nchi. Aidha, ni kweli pia kwamba majibu hayo ya Serikali huzingatia hoja na mantiki ya swali linaloulizwa na Mbunge yeyote katika kutaka kupata ufafanuzi toka Serikalini kuhusu jambo lolote kama sehemu ya Utekelezaji wa Majukumu ya Bunge kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 63 (3), vipengele (a) – (e).

Mheshimiwa Spika, majibu ya Serikali kuhusu utekelezaji au ufafanuzi wa jambo lolote linalohusu maslahi ya umma, huwa ni mwongozo kwa wananchi katika kufuatilia uwajibikaji wa Serikali waliyoiweka madarakani kwa ridhaa yao wenyewe. Aidha, ni wajibu wa Bunge na Waheshimiwa Wabunge kuhakikisha kwamba majibu yanayotolewa na Serikali ni sahihi na yanayokidhi haja.

Pamoja na kuhakikishia Mheshimiwa Philemon Ndesamburo na Bunge hili Tukufu kuwa Serikali iko makini sana katika utekelezaji wa ahadi na maamuzi mbalimbali yanayotolewa kupitia Bunge; na pale inapoonekana maamuzi au ahadi hizo zinapuuzwa tunaomba Wabunge na wananchi wawasilishe matukio hayo Serikalini haraka iwezekanavyo.

Na. 31

**Fedha Zinazopelekwa Wilayani**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi sasa fedha nyingi toka Serikalini na kwa wafadhili zinapelekwa moja kwa moja Wilayani ambako kunatakiwa kuwe na usimamizi mzuri:-

(a) Je, Serikali ina uhakika kwamba watendaji (Wakuu wa Idara) wote wana fedha za kusimamia fedha hizo?

(b) Je, Serikali imefikia wapi katika zoezi la watumishi wake na imechukua hatua gani?

(c) Je, Serikali inasemaje juu ya watumishi wa Halmashauri za Wilaya ambao wamekaa muda mrefu kwenye kituo kimoja na wengine kutawaliwa na mazingira na kusahau kazi zao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu a, b na c kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Serikali imekuwa ikitoa fedha nyingi kwenda katika Halmashauri ikiwa ni pamoja na fidia ya vyanzo vya mapato, ruzuku kutoka Serikali Kuu, fedha za wafadhili kwa ajili ya matumizi ya kawaida na fedha za maendeleo katika miradi mbalimbali ya maendeleo. Kimsingi jukumu la usimamizi wa fedha zinazopelekwa katika Halmashauri, pamoja na kutenga fedha kwa ajili ya tathmini na ufuatiliaji wa kazi kwa ajili ya madiwani na maafisa wa Halmashauri ni la Halmashauri zenyewe. Hata hivyo, katika kuhakikisha kuwa fedha zinazopelekwa Halmashauri zinasimamiwa vizuri Serikali, imetoa mwongozo kwa kila Halmashauri kutenga asilimia 15% ya fedha za ruzuku ya maendeleo kwa ajili ya tathmini na ufuatiliaji. Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa maelekezo yaliyotolewa yanazingatiwa ili fedha zinazotolewa zitumike kwa malengo yanayokusudiwa. Vile vile katika mwaka wa fedha 2008/2009 Idara zote katika Halmashauri zimetengewa fedha za matumizi ya kawaida ikiwa ni pamoja na zile za Idara ambazo siku za nyuma zilikuwa hazipati ruzuku ya Serikali. Idara hizo ni pamoja na Mipango, Maendeleo ya Jamii, Biashara, Maliasili na Ushirika.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu zoezi la kujaza nafasi wazi ili kuhakikisha kuwa Halmashari zinajiendesha kwa ufanisi, Serikali imeendelea kujaza nafasi wazi. Kwa mfano nafasi za Wakuu wa Idara katika Halmashauri karibu zote zimejazwa na watumishi wenye sifa. Katika mwaka wa fedha 2007/2008 Serikali imeajiri na kuwapangia vituo vya kazi Maafisa Mifugo 46, Maafisa Mifugo Wasaidizi 119, Maafisa Kilimo 218, Maafisa Kilimo Wasaidizi 101, Wahasibu 322 na Wakaguzi wa Ndani 256. Aidha, kwa watumishi ambao wamebainika kukiuka taratibu za matumizi ya fedha, wamechukuliwa hatua za kinidhamu na kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa katika vyombo vya kisheria.

(c) Mheshimiwa Spika, kuhusu watumishi waliokaa muda mrefu katika kituo kimoja cha kazi Serikali imefanya zoezi la tathmini ili kubaini watumishi wa aina hiyo katika Halmashauri mbalimbali na kuwahamisha. Zoezi hili litaendelea kutelekezwa kwa awamu kutokana na ukweli kuwa ni la gharama kubwa na Halmashauri zetu hazina uwezo mkubwa kifedha kumudu uhamisho wa watumishi wengi kwa wakati mmoja. Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali kwa nia ya kuboresha utendaji na ufanisi wa watumishi na hatimaye kuleta maendeleo.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niulize mswali mawili madogo ya nyongeza.

(a)Kwa kuwa Serikali iliwaonea huruma wananchi wake ikawafutia kodi ya maendeleo na ikaanza kutoa fedha kutoka Serikalini ziende moja kwa moja kama asilimia 20 kwenye kila kijiji, kila Wilaya kwa ajili ya kujianzishia miradi ya maendeleo yao wenyewe. Kwa kuwa fedha hizi sasa hivi hazifiki kwa idadi na wakati unaotakiwa kwa sababu zinakatwa Hazina kulipia madeni ya Halmashauri ambazo ziliingia kwa matumizi mabaya kutokupeleka hela kwenye vyombo ambavyo watumishi wanaatakiwa wachangiwe. Je, Serikali inasemaje juu ya hilo?

(b)Kwa kuwa hiyo asilimia 20 inatakiwa iende kwenye Serikali ya Kijiji lakini zikifika Halmashauri wanazipangia miradi yao wakisingizia kwamba ni miradi ya kijiji, utaratibu huo utakoma mara moja? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mgana Msindai, kama ifuatavyo.

Ni kweli kabisa kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge Serikali baada ya kuondoa zile kodi ambazo zinaonekana kama ni kero kwa wananchi, iliamua kwamba iwe inazifidia Halmashauri na Halmashauri hatimaye ziweze kupeleka kiasi hicho katika *level* ya kijiji. Kwa hiyo, pesa zile ambazo zinakuja kama fidia, utaratibu wa Serikali ni kwamba zikifika pale kwenye Halmashauri zinatoka zinaenda kwenye Kata na zinaenda moja kwa moja mpaka katika *level* ya kijiji kwa ajili ya shughuli za maendeleo zinazofanyika pale. Sasa amezungumzia kwamba kuna vyombo mbalimbali kama *LPF* na vyombo vingine ambavyo zinakatwa hizi kutoka Hazina na kwamba kwa hiyo hela hizi hazifiki kule, majibu yake ni haya yafuatayo, asilimia 20 kwamba inatakiwa kwenda kijijini ni maelekezo ya Serikali, ndivyo ilivyowekwa, iko kabisa na asilimia nyingine tano kwa ajili ya kina mama na asilimia nyingine kumi, asilimilia nyingine tano kwa ajili ya vijana, hili ni tamko la Serikali. Kwa hiyo nakubaliana kabisa na Mheshimiwa kwamba utaratibu huo ndio utaratibu tunaoufahamu. Kwa hiyo, tunatakiwa tupeleke hizi hela pale kwa sababu kile chanzo kilichokuwa kinatumika sasa hakitumiki.

Kuhusu asilimia 20 anazozizungumza ni *almost* jambo lile lile kwamba nazo zinakuja zinachukuliwa kutoka kule tarehe fulani zinachukuliwa pale Halmashauri, jibu lake ni hilo hilo zile zinazokuja kwa ajili ya *development* kwa maana ya *capital development* ni asilimia 50 na zile nyingine anazozizungumza zile ambazo zimechukuliwa sasa kwa ajili ya kufidia ni asilimia 20.

Mheshimiwa Spika, ningeomba nichukue nafasi hii kuzitaka Halmashauri kwa niaba ya Waziri Mkuu zitekeleze maelekezo hayo. (*Makofi*)

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, ninaomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa kumekuwa na matatizo ya wataalam katika

Halmashauri zetu na wanapogundulika wamefanya vibaya Wizara huhamisha kutoka Halmashauri moja na kupeleka katika Halmashauri nyingine.

Je, Waziri haoni wanahamisha tatizo Halmashauri moja na kupeleka tatizo hilo hilo Halmashauri nyingine? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Kilimanjaro kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ukimhamisha mtumishi mbovu kutoka Halmashauri moja ukampeleka kwenye Halmashauri nyingine maana yake pale unachofanya ni kwamba unahamisha tatizo lingine.

Lakini kumbukumbu zetu hazionyeshi kwamba tumekuwa tunafanya hivyo, Halmashauri ambazo zimekuwa na watendaji ambao wamekuwa na matatizo, hatua za kinidhamu zimekuwa zinachukuliwa dhidi yao, wamekuwa wanapelekwa mahakamani na mimi ninazo takwimu hapa tumewahi kupata matatizo katika Wilaya ya Dodoma, Kondoa na pia tumewahi kupata matatizo katika Wilaya ya Korogwe, tumekuwa na matatizo katika Wilaya ya Chamwino na hawa watu wamepelekwa mahakamani na juzi juzi tu hapa, matokeo ya Mahakama kwa upande wa Korogwe yalionyesha kwamba yule ambaye alikuwa ni Mkurugenzi Mahakama ilimwona kwamba hana tatizo lolote lile katika maana hiyo iliyozungumzwa hapo. Kwa hiyo nataka kusema hapa kwamba hatumchukui mtumishi tukamhamishia Wilaya nyingine, bali tunamchukulia hatua za kinidhamu. (*Makofi*)

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwa kuwa kuweko kwa Wakuu wa Idara katika Halmashauri za Wilaya ni jambo mojawapo ambalo linafanya Serikali iamue kuipa Halmashauri hiyo ruzuku au isiipe kama Wakuu wa Idara hawapo wote. Sasa Wilaya cha Chamwino sasa hivi Wakuu wa Idara karibu robo tatu wote wanakaimu.

Je, Waziri haoni umuhimu wa kuipa Wilaya ya Chamwino Wakuu wa Idara wa kudumu ili baadaye tusipate hasara ya kunyimwa ruzuku kwa kutokuwa na Wakuu wa Idara?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa John Malecela, Mbunge wa Mtera, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge mzee John Malecela kwamba moja ya kigezo ambacho unakitumia ili uweze kupeleka hela kwa ajili ya maendeleo katika Halmashauri ni pamoja na kuwa na Wakuu wa Idara ambao wako pale wamewekwa wa kudumu siyo huyu anayekaimu na ninakubaliana naye kwamba kama huna utaratibu wa namna hiyo ni chanzo cha kuweza kupoteza hela za Serikali kwa maana ya kuweza kuleta maendeleo katika eneo lile.

Amezungumzia Wilaya ya Chamwino na ninatambua kwamba Wilaya ya Chamwino ni Wilaya mpya inawezakana kabisa Mheshimiwa John Samwel Malecela kwamba pale pana Wakuu wa Idara ambao wanakaimu.

Lakini nataka nilithibitishie Bunge hili kwamba sasa hivi utaratibu tuliouweka ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na Wakuu wa Idara wa kudumu na siyo hao tunaozungumzia wa muda wanaozungumzwa hapa.

Kwa hiyo ninataka niseme tu kwamba hili la Wilaya ya Chamwino ninalichukua hapa na nina hakika kwamba ninatoa kauli hii kwa niaba ya Serikali kwamba tutalifuatilia na kuhakikisha kwamba Wakuu wa Idara walioko katika Wilaya ya Chamwino watakuwa ni wale wa kudumu. (*Makofi*)

Na. 32

**Tatizo la Rushwa Nchini**

**MHE. OMAR ALI MZEE** aliuliza:-

Kwa kuwa rushwa na ufisadi ni tatizo linalovunja adhima ya Serikali ya kuimarisha utawala bora kwa kuhakikisha nchi inaendeshwa kwa misingi ya sheria, kanuni na taratibu za kidemokrasia:-

Je, Serikali ina mpango gani mahususi wa kukabiliana na wala rushwa na mafisadi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mbunge wa Kiwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua tatizo la rushwa na madhara yake katika Taifa na ndio maana ikachukua hatua ya kuandaa mkakati wa Kitaifa dhidi ya rushwa na

mpango wa utekelezaji wake kwa Tanzania (*NACSAP*) ambao kwa sasa upo katika awamu ya pili ya utekelezaji.

Katika awamu ya kwanza ya utekelezaji (1999 – 2005), mkakati huu uliweka msisitizo kama maeneo yafuatayo:-

- Mabadiliko katika Ofisi ya Serikali na nidhamu katika matumizi ya fedha na kuongeza ufanisi katika kutoa huduma.

- Kuongea uelewa wa umma katika mapambano dhidi ya rushwa.

- Kuongeza uwazi, uwajibikaji katika shughuli za Serikali.

- Kushirikisha taasisi za kisheria na sekta binafsi katika kupambana na rushwa.

- Kusisitiza na kudumisha utawala wa sheria.

Awamu ya pili ya mkakati huu (2006 – 2010) imelenga katika:-

- Kuongeza wigo wa kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa. Sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa Na. 11/2007, kwa mfano, ni matokeo ya utekelezaji wa kipengele hiki.

- Kuboresha utoaji wa huduma zitolewazo na Ofisi ya Umma.

- Kuziongezea nguvu za kisheria taasisi zinazosimamia masuala ya rushwa na utawala bora *(watchdog institutions)* kama vile TAKUKURU na Tume ya haki za Binadamu na Utawala Bora (*CHRGG*) na vyombo vingine vinavyosimamia sheria kama vile mahakama.

- Kushirikisha sekta binafsi, taasisi za kiraia na vyombo vya habari katika mapambano dhidi ya rushwa.

- Kuongeza uelewa wa umma kuhusiana na rushwa.

- Kuhimiza na kusimamia uwazi, uadilifu na uwajibikaji kama nguvu muhimu katika kuzuia na kupambana na rushwa pamoja na kukuza utawala bora nchini. Hili limetekelezwa, kwa namna moja kwa kuanzisha Kamati za maadili katika Wizara, Idara na wakala za Serikali.

- Serikali pia imeboresha ushirikiano wake na mataifa mengine kupitia kusaini mikataba ya Kimataifa ya kuzuia na kupambana na rushwa jambo linaloziwezesha taasisi zenye dhamana hiyo nchini, kama vile TAKUKURU, kushirikiana na taasisi za nje katika chunguzi za vitendo vya rushwa vilivyofanyika nje ya Tanzania.

**MHE. OMAR ALI MZEE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. mimi nataka kuuliza kwamba je Serikali imechukua hatua gani kwa wale wote waliobainika na rushwa na ufisadi?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS(UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Omar Ali Mzee, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa Serikali inaendelea na uchunguzi wa kina ili tuweze kupata ushahidi wa tuhuma hizo za rushwa na mara uchunguzi utakapotimia basi watapelekwa Mahakani na Mahakama ndiyo itakayotoa adhabu yoyote dhidi ya watuhumiwa wala rushwa.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ninashukuru kwa kunipa hii nafasi.

Mheshimiwa Spika, kila siku tunapouliza swali hili tunaambiwa kwamba kuna uchunguzi wa kina je uchunguzi huo wa kina utamalizika lini?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu swali lake Mheshimiwa Shoka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uchunguzi wa kina unaendelea na mara utakapomalizika ningependa nieleze kwamba masuala ya rushwa ni masuala ya Kisheria yametoka kwenye siasa yamefika kwenye Sheria na katika Sheria ni lazima tupate ushahidi ambao unaweza ukakubalika Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, tukienda kichwakichwa tu nao pia wana haki. Watuhumiwa wa rushwa wote wana haki ya kujitetea, kwa hiyo mpaka sasa tuna watuhumiwa ambao na wao wana ushahidi wao *unless* tunapata ushahidi wa kutosheleza ambao bado tunaendelea kukusanya hizo shahidi na ndipo tutakwenda Mahakamani. Hatuwezi kwenda halafu tukienda na tukishindwa hizi kesi nadhani Bunge litasema tumewaachia huru.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko swali linaulizwa na Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza.

Na. 33

**Sheria Ya Uandikishaji wa Biashara Kutumika**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa, sasa ni zaidi ya mwaka mmoja tangu Sheria ya Uandikishwaji wa Biashara kupitishwa na Bunge na hatimaye kukubaliwa na Mheshimiwa Rais.

Je, kuna tatizo gani linalofanyika Serikali ichelewe kuandaa Kanuni na taratibu muhimu ili Sheria hiyo ianze kutumika?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara (*Business Activities Registration Act* – BARA), Na. 14 ya mwaka 2007, ilipitishwa na Bunge hili katika kikao chake cha mwezi Februari, 2007. Sheria hii itachukua nafasi ya Sheria ya Leseni za Biashara Na. 25 ya Mwaka 1972, ambayo inatumika kusimamia jukumu la utoaji wa Leseni za biashara.

Mheshimiwa Spika, katika mchakato wa kutayarisha Kanuni za kutekeleza Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara, baada ya majadiliano ya kina na Wadau, Mshauri Mwelekezi ameishauri Serikali kufanya marekebisho madogo (*miscellaneous amendments*) katika Sheria hii ili kuondoa kasoro ambazo zimebainishwa.

Serikali ilichambua ushauri huo wa kina na ilikubaliana kimsingi na mapendekezo ya Mshauri Mwelekezi, pamoja na Wadau wa Sekta ya biashara ya kufanya marekebisho madogo ili kuhakikisha kuwa utekelezaji wa Sheria hii unaleta matokeo yanayotarajiwa. Hii ndiyo sababu iliyochelewesha Serikali kukamilisha mapema Kanuni na Taratibu za kutumia Sheria husika.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu hivi sasa inakamilisha rasimu ya marekebisho yaliyobainishwa ili yawasilishwe katika Bunge lako Tukufu kwa uamuzi. Mara baada ya marekebisho ya Sheria,Kanuni na Taratibu nazo zitakamilishwa ili Sheria ianze kutumika.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, madhumuni makubwa ya kuanzisha Sheria ya Uandikishaji wa Biashara ilikuwa ni pamoja na kuzitambua Biashara na kuwajengea mahusiano mazuri na uwezo mkubwa wafanyabiashara wadogo wadogo ili hatimaye waweze kuwa wafanyabiashara wazuri na walipaji wazuri wa kodi.

Mheshimiwa Spika, je ucheleweshaji huu Mheshimiwa Waziri haoni kwamba unawacheleweshа, vilevile kujenga wafanyabiashara hawa wadogo uwezo wao?

Pili, ni kwamba Sheria hii wakati inajadiliwa ilikuwa inahusiana vilevile na uwezekano wa kutoa unafuu mkubwa katika ada za leseni za biashara. Sasa bado wananchi wanasumbuliwa katika ulipaji wa ada za Leseni za Biashara. Ucheleweshaji huu unaleta migongano, Mheshimiwa Waziri anaweza kutuambia ni lini hasa Sheria hii katika mabadiliko aliyoyasema itafanyiwa kazi ili matatizo haya yapungue?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Herbert Mntangi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuzitambua biashara ndogo na kujenga uwezo wa biashara wa wafanyabiashara wadogo ni kweli ndiyo madhumuni ya sheria yenyewe na ninakubaliana na Mbunge kwamba ucheleweshaji huo vilevile unachelewesha kujenga uwezo wa wajasiria mali.

Kwa hiyo, nitakaloweza kulisema tu hapa ni kuahidi kwamba Wizara itajitahidi sana ili mapema itakavyowezekana na ikiwezekana mwezi wa kumi wa kadri nafasi itakavyojitokeza ya kutunga Sheria basi tutaleta marekebisho hayo na ili baadaye tukamilishe Kanuni na taratibu za kutekeleza Sheria hiyo.

Swali la pili, kwamba Sheria yenyewe ilikuwa inataka kupunguza ada na kwa hivyo ucheleweshaji kwa vyovyote vile unaleta adha kwa wajasiriamali. Napenda kusema kwamba nasikitika kwa athari hizo walizopata wajasiriamali lakini napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu itabidi kukamilisha marekebisho haya ili baadaye tutunge Kanuni na Sheria ianze kutumika mara moja.

Na. 34

**Viwanda Vya Saruji Na Mabati Kujengwa Mwanza**

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU** aliuliza:-

Kwa kuwa, imewezekana kuanzishwa viwanda vya bia Jijini Mwanza na hivyo kuwapunguzia adha na gharama watumiaji wa kinywaji hicho katika kanda ya Ziwa.

Je, kuna ugumu kwa Serikali kusimamia kidete na kuhakikisha viwanda vya Saruji na mabati vinajengwa Mwanza haraka iwezekanavyo ili kuwanusuru wananchi wa ukanad huo na gharama kubwa za ujenzi zinazowakumba hivi sasa?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mbunge wa Magu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna ugumu wa kujenga kiwanda cha Saruji katika moja ya mikoa ya kanda ya ziwa kwani Serikali imekuwa na lengo la kujenga kiwanda cha Saruji eneo hilo tangu miaka ya sabini (70) bila mafanikio. Hii ni kutokana na malighafi zilizoko katika mikoa hiyo kuwa hafifu.

Mheshimiwa Spika, katika utengenezaji wa saruji malighafi kuu ni madini aina ya chokaa (*limestone*), udongo mwekundu na jasi (*gypsum*). Kwa kila tani moja ya malighafi ya kutengenezea saruji, asilimia 75 – 80 ni madini aina ya chokaa. Utafiti uliofanywa kwa kuchukua sampuli kutoka katika mashimo zaidi ya 300 ambayo yalichimbwa katika maeneo ya Bushora, Mwamala, Nyabeho, Mirinuma na Nyamisengeza umedhihirisha kuwa chokaa iliyopatikana haina ubora unaofaa kwa ajili ya uzalishaji wa saruji. *(Makofi)*

Chokaa ahiyo naonyesha kuwa na kiwango kikubwa cha madini aina ya silica (karibu asilimia 16) ikilinganishwa na kiwango kinachohitahika ambacho ni chini ya asilimia 8).

Mheshimiwa Spika, ili kuitumia chokaa hiyo, ni lazima kuisaga na kuichekecha (*beneficiation*) na baadaye ichanganywe na chokaa yenye ubora zaidi (*high grade limestone*) ndipo itumike katika kutengeneza saruji. Pamoja na kuwa saruji inaweza kutengenezwa kwa mchakato kama huu bei yake itakuwa kubwa kiasi kwamba itakuwa haiuziki.

Hata hivyo kwa vile umuhimu wa kujenga kiwanda cha saruji katika kanda ya Ziwa bado upo, Serikal itaendelea na utafiti ili kubaini maeneo yenye chokaa bora, hali itakayopelekea wawekezaji kuvutiwa na kuwekeza katika kanda hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kiwanda cha bati naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa ili kutengeneza bati moja mkoani Mwanza, malighafi aina ya *hot rolled coils* inabidi iagizwe kutoka nje ya nchi hadi Dar es Salaam kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza. Hivyo, gharama za kuifikisha malighafi hiyo Mwanza ni kubwa sana ikilinganishwa na malighafi hiyo inapoishia Dar es Salaam. Pamoja na kwamba kuna soko kubwa la bati, wawekezaji hawajahamasika kujenga viwanda vya kutengeneza bati Mwanza kwa sababu ya gharama kubwa za kuzalisha bidhaa hiyo ambayo watatakiwa kuuza kwa bei kubwa na hivyo kutoweza kushindana na bei ya bati zinazozalishwa Dar es Salaam na kuzwa Mwanza. Hata hivyo, Serikali taendelea kuimarisha njia za usafirishaji, hususani usafiri wa reli na barabara ili kupunguza gharama za usafirishaji na kuvutia wawekezaji kujenga viwanda vya kuzalisha bidhaa hiyo katika kanda ya Ziwa.

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kanda ya Ziwa na hususani wananchi wa Jimbo la Magu wamekuwa wakijenga nyumba kwa gharama kubwa sana za *cement* pamoja na mabati. Kwa kuwa wananchi wa Magu nao ni kama Watanzania wa Maneromango ambao wako karibu na viwanda vya saruji na mabati na kwa kuwa Serikali inaandaaa utafiti bado toka miaka ya 70 na hakuna mwelekeo kulingana na jibu la Waziri kwamba huo utafiti utaleta manufaa hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali haiwezi kuangalia utaratibu kama unaofanyika kwenye Kilimo ambapo mbolea ya ruzuku inapelekwa kwenye Mikoa minne yaani *The Big Four* yenye ruzuku kwa nini Serikali pia isipeleke *Cement* kwenye Mikoa ya Kanda ya Ziwa yenye ruzuku?

Mheshimiwa Spika, pili, kwa sababu viwango vinavyotolewa kwenye ujenzi wa miradi kama madarasa ni sawasawa kwa Mikoa ya Mashariki na Mikoa ya Kanda ya Ziwa. Kwa nini Serikali isifikirie kuongeza viwango sasa kwa ujenzi wa miradi kama Madarasa, Zahanati na Kadhalika ili viwe vikubwa zaidi kwa sababu mabati na *cement* ni kubwa zaidi katika Kanda ya Ziwa?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, na mimi nawaonea huruma wananchi wa Kanda ya Ziwa kwa sababu kutokana na gharama ya usafirishaji kwa vyovyote vile bei ya *cement* na bei ya bati itakuwa juu Mwanza kutokana na gharama inayotokana na usafiri na gharama nyingine.

Mheshimiwa Spika, ni bahati mbaya utafiti haujatusaidia kwa sababu kama hakuna malighafi inayotakiwa si rahisi kufanya jambo lolote lile ile malighafi hiyo ipatikane. Lakini Wizara vilevile imeliona tatizo hilo na kujaribu kuzungumza na viwanda vya *cement* ili kufungua maeneo ya wao kuweza kutawanya cement huko badala ya *agency* au mawakala kwenda Dar es Salaam kuchukua *cement* na hivyohivyo kwa bati.

Naomba nimwombe Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Kanda ya Ziwa waelewe kwamba Serikali inatambua tatizo ili uwezo wa kuondoa tatizo hilo kwa upande wa Serikali si rahisi na ni kweli kwamba tumekuwa na mkutano na wanaozalisha *cement* Tanga, Mbeya na Dar es Salaam kwamba waweze kufungua vituo vya kuwawezesha wale wanaotoka Mwanza badala ya wao kugharamia gharama ya usafiri basi waweze ku-*share* zile gharama.

Sasa kutokana na kwamba viwango vinavyogiwa vya Bajeti ni sawa nchi nzima mimi nina hakika kuna mambo ambayo yatakuwa na bei nafuu kwa Mwanza na pengine yakawa na bei ya juu Mbeya au sehemu nyingine. Kwa hiyo, katika ujumla wake nina hakika kila mmoja atakuwa anapata adha katika sehemu moja na unafuu kwa sehemu

nyingine. Lakini hilo ni jambo ambalo Serikali iliangalie na panapo uwezo basi niwaachie wale wanaohusika kuliangalia hilo.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa uhitaji wa viwanda vya aina mbalimbali ni kwa maeneo mengi hapa nchini ukiwemo Mkoa wa Singida.

Kwa kuwa Mkoa wa Singida kuna viwanda vidogovidogo tu kwa ajili ya kukamua mafuta ya alizeti na mkoa huo unalima alizeti nyingi sana. Je, Serikali itatuonea huruma kutujengea kiwanda kikubwa cha kukamua mafuta ya alizeti ili wananchi wetu kupunguziwa adha ya kukesha usiku kucha na kukaa wiki nzima kwa ajili ya kusimamia ukamuaji wa mafuta ya alizeti?

**SPIKA:** Aah! naona hili ni swali jipya kwa sababu tumetoka kwenye Saruji lakini kwa kuwa ni kiwanda sijui Waziri kama ungependa kujibu.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum Singida na ninampongeza kwa kupigania mkoa wake.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna viwanda vidogovidogo vingi vya kukamua mafuta Mkoani Singida kwa sababu Singida wanalima alizeti nyingi na vilevile sisi wa Manyara na wa Mikoa mingine inayozunguka Singida wanalima alizeti nyingi.

Napenda kumueleza Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa hivi Serikali haiwekezi tena kwenye viwanda au kwenye biashara, wanaofanya hivyo ni sekta binafsi. Mimi kama Waziri wa Viwanda na Biashara na yeye tusaidiane kuhamasisha sekta binafsi iweze kuona umuhimu huo ili wananchi wa Singida waweze kufaidi malighafi ambayo wanailima wakulima wa huko.

**SPIKA:** Swali la mwisho la nyongeza kutoka kwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa njia moja ya kuweza kupunguza bei ya bidhaa yoyote ni kuwa na bidhaa hiyo kwa wingi katika nchi, na kwa kuwa wapo wawekezaji wengi wamekuja kutaka kuwekeza katika viwanda vya saruji lakini bado Serikali haijakuwa na Sera maalum ya kujua ni viwanda gani na sehemu gani wanavihitaji wawekezaji hao wamerudi hivyo kusababisha saruji katika nchi kuwa na upungufu mkubwa.

Je, Serikali ni lini itatoa sera kamili ya kusema viwanda vingapi vya saruji vinatakiwa na mahali gani ?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kuona kwamba Wabunge wengi wanahamasika na suala la viwanda hapa nchini.

Ni kweli kuna wawekezaji wengi ambao wameonyesha nia ya kuwekeza Tanzania kuzalisha saruji nyingi na mimi nataka kumweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali haina pingamizi na ninataka nimwambie kwamba mwekezaji mkubwa duniani wa kuzalisha saruji hivi karibuni ameonyesha nia ya kuwekeza Mtwara na wapo wengine ambao wameonyesha nia ya kuwekeza kwingine. Serikali itawawezesha kufanya hivyo ili sisi tuweze kunufaika na ajira tutakazopata na bidhaa ya *cement* tutakayopata na manufaa mengine yote yanayotokana na kuwekeza katika viwanda.

Na. 35

**Kiswahili Kutumika Kutunga Sheria**

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA** aliuliza:-

Kwa kuwa wote tunajua kwamba miswada yote ya sheria inayoletwa Bungeni na Serikali inaandikwa kwa lugha ya Kiingereza licha ya kwamba huwasilishwa kwa Kiswahili:-

(a) Je, Serikali inaweza kueleza kwa nini baada ya miaka 47 tangu uhuru bado inatumia kiingereza na siyo Kiswahili?

(b) Je, Serikali ina mipango gani kuondoa kasoro hii?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Stephen Jonas Galinoma, Mbunge wa Kalenga, naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Nilipokuwa najibu swali Na. 72 la Mheshimiwa Col. Saleh Ali Farrah, Mbunge wa Rahaleo, katika kikao cha sita tarehe 6 Februari 2007 nililieleza Bunge lako Tukufu kwamba:-

Miswada yote inayoletwa mbele ya Bunge hili kwa madhumuni ya kujadiliwa na kupitishwa huandikwa kwa lugha ya kiingereza kwa sababu ya mfumo wa Sheria ambao nchi yetu imeurithi kutoka mfumo wa Waingereza. Mfumo huo wa Sheria na utaratibu wa kurithi sheria kama ilivyofanya Tanzania pia unafuatwa na nchi nyingi ambazo zamani zilikuwa chini ya utawala wa kikoloni wa kiingereza. Baada ya maelezo hayo mafupi naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba kabla ya Bunge letu Tukufu kuanza kutunga sheria zetu wenyewe, tulikuwa tukitumia sheria zilizotungwa na Bunge la Uingereza ambazo zimeandikwa kwa kiingereza na baada ya nchi yetu kupata Uhuru wa Waingereza kuondoka, bidhaa ya wataalam wa kiingereza walibaki nchini ili kuwafundisha wataalam wetu wa Kitanzania uandishi wa sheria na lugha waliyokuwa wakiitumia ni kiingireza, hata leo hii wataalam wetu wanafundishwa uandishi wa sheria kwa lugha ya kiingereza kitendo kinachowapelekea kutumia lugha hiyo katika kufanya kazi zao.Hadi sasa hivi ninavyojibu swali hili waandishi wa sheria wanapata mafunzo yao ya uandishi wa sheria nje ya nchi na lugha wanayofundishiwa ni kiingereza. Niseme tu kwamba uandishi wa Sheria ni taaluma maalum katika masuala ya Sheria.

(b) Serikali kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaimarisha Idara ya Uandishi wa Sheria kwa kuiongezea wataalam wa kiswahili ili waweze kuandika sheria kwa lugha zote mbili za kiingereza na kiswahili kwa ufanisi na ufasaha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Idara ya Uandishi wa Sheria inafanya tafsiri ya Sheria zetu mbalimbali kwa lugha ya Kiswahili na inaandaa Sheria ndogo zote za Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji na Wilaya kwa lugha ya kiswahili.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA**: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa majibu yake fasaha.

Hata hivyo ninapenda kuuliza swali la ziada. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwamba iko haja ya kuwa na sera au program ya muda mrefu ya jinsi ya kukuza na kutumia Kiswahili ili kusudi kiweze kutumika zaidi na zaidi katika nyanja mbalimbali na siyo tu Bunge lakini pia Mahakama ambayo ni kinyume cha swali langu la msingi kwamba wao huendesha kesi kwa Kiswahili lakini wakaweka kumbukumbu kwa kingereza. Naomba Waziri aniambie kama anakubaliana nami ama sivyo.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mbunge wa Kalenga, kama ifuatavyo:-

Kimsingi nakubaliana naye kwamba ipo haja ya kuwa na program ya muda mrefu ya matumizi ya lugha ya Kiswahili katika Sheria na katika nyanja nyingine. Tunachofanya sasa hivi Mahakama zetu ziendelee kutumia lugha hii ni hizihizi Sheria zenyewe kwamba bado ziko katika lugha ya Kingereza. Kwa hiyo, pamoja na program hiyo ambayo nadhani itajumuisha mambo mengine kutafsiri Sheria zetu zote ziwe katika lugha hii. Lakini program kama alivyosema ni ya muda mrefu na mimi nakubaliana naye kwamba haja ya kuwa na program hiyo ipo kwa nchi yetu.

Na. 36

**Wafungwa Wenye Makosa Makubwa Kuanchiwa Kwa Rufaa**

**MHE. SIJAPATA F. NKAYAMBA (K.n.y. MHE. KAIKA S. TELELE)** aliuliza:-

Kwa kuwa, viongozi wa Taifa letu wamedhamiria kwa dhati kujenga Taifa linaloongozwa kwa misingi ya Sheria na Utawala Bora. Na kwa kuwa wafungwa takriban arobaini (40) waliachiwa kwa rufaa mwaka 2007 kutoka Gereza Kuu la Arusha kati ya mwezi Machi na Septemba licha ya wafungwa hao kukabiliwa na makosa makubwa ya jinai kama unyang'anyi wa kutumia silaha, kuvunja na kuiba, kubaka na kadhalika.

(a) Je, ni sababu zipi za msingi zilizosababisha Majaji wa Mahakama za Rufaa kuwaachia huru wafungwa waliohukumiwa miaka 30 au zaidi ya Mahakama za chini?

(b) Je, kitendo hicho hakitaongeza matukio ya uhalifu nchini na hasa katika miji mikbuwa kama Arusha?

(c) Je, kuna harufu ya rushwa katika Mahakama zetu?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kaika Telele, lenye sehemu a, b, na c kama ifuatavyo:-

(a)Sababu zilizosababisha Majaji wa Mahakama za Rufani kuwaachia huru wafungwa waliohukumiwa miaka 30 au zaidi na Mahakama za chini ni za Kisheria. Mtu anapohukumiwa na kuomba Mahakama za chini anayo haki ya Kikatiba ya rufaa dhidi ya hukumu hiyo kwenye Mahakama ya juu.

Mahakama ya Rufani inayo mamlaka ya kupitia mwenendo wa hukumu ya Mahakama ya chini na kujiridhisha kwamba taratibu zote za Kisheria na Kanuni za ushahidi zilizingatiwa na kufuatwa katika kumhukumu mhusika. Na endapo Mahakama hiyo itabaini kuwa taratibu hizo au Kanuni zimekiukwa, Kisheria lazima mhusika aachiwe huru. Kimsingi ili mtu awe na hatia na kuhukumiwa kifungo au adhabu yoyote ile ni lazima ushahidi uthibitishe kwamba mshtakiwa alitenda kosa hilo bila ya kuacha shaka yoyote hata kama ni ndogo kiasi gani.Mfumo wetu wa Kimahakama unampa mshitakiwa haki ya rufaa kuanzia ngazi ya Mahakama ya Mwanzo, Mahakama ya Wilaya, Mahakama Kuu na hatimaye Mahakama ya Rufani ili kuhakikisha kufungwa kwake ni kwa misingi ya Kisheria. Ngazi yoyote ya rufani ikibaini taratibu za kisheria zilikiukwa haina budi kumwachilia mshitakiwa huru.

(b) Rufaa ni haki ya Kikatiba kwa kila mtu ambaye hajaridhika na uamuzi wa Mahakama. Lengo la rufaa ni kumpa mtu haki yake na siyo kuongeza uhalifu. Hivyo basi kitengo cha Mahakama ya Rufaa kuwaachia huru washitakiwa hakiwezi kuongeza matukio ya uhalifu nchini bali kinadumisha utawala wa Sheria na Haki za Msingi za kila Binadamu kwamba haonewi mtu yeyote kupitia mkondo wa Mahakama.

(c) Chini ya Ibara ya 13 (6) (a) Rufaa ni haki ya Kikatiba kwa kila mtu ambaye hajaridhika na uamuzi wa Mahakama iliyo mhukumu na maamuzi yanayotolewa na Mahakama katika hatua zote hufuata taratibu za Kisheria za nchi yetu.

Kwa hiyo, katika suala hili hakuna harufu ya rushwa, ni Sheria tu imezingatiwa kikamilifu.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja dogo la nyongeza.

Hisia ya rushwa katika kesi za aina hii inatokana na dhana kwamba kesi zinazowahusisha watu wakubwa zinakwenda haraka sana, zinachukua muda mfupi na hatimaye wanaachiwa wakati watu wadogo, walala hoi, wanaweza kusota hadi miaka 10 hata kabla kesi haijasikilizwa.

Je, Serikali iko tayari kufanya utafiti wa kina kutathmini mambo ya aina hii na kuchukua hatua pale inapostahili?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dr. Slaa, Mbunge halali wa Karatu kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, katika kesi za rushwa kinachofanya kesi ziende haraka au kuchelewa ni upatikanaji wa ushahidi na hii siyo katika kesi ya rushwa tu ni katika kesi zote zinazomhusu mtu mkubwa au mdogo, zinazomhusu mtu tajiri au maskini kinachogomba mara zote ni upatikanaji wa ushahidi.

Mheshimiwa Spika, ushahidi ukipatikana kwa haraka kesi itakwenda kwa haraka lakini ushahidi ukichelewa kesi itachelewa pia.

Kwa hiyo, pendekezo lake kwamba tuanye utafiti tuone ni jinsi gani tunaweza kuboresha hali hii ni pendekezo linalokubalika tutaliangalia kwa wakati wake.

**SPIKA:** Ili tuyamalize maswali naona tuende Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa wa Viti Maalum Mkoa wa Mwanza.

Na. 37

**Fedha za Wajasiriamali Kutolewa kwa Uwiano wa Watu na Ukubwa wa Mkoa**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA** aliuliza:-

Kwa kuwa fedha za wajasiriamali (Sh. 1bn/=) zilizotolewa kwa kila mkoa hazikuzingatia uwiano wa watu na ukubwa wa mikoa kama vile Mikoa ya Mwanza, Mbeya, Tanga na kadhalika:-

Je, Serikali haioni kuwa kuna haja sasa ya kutoa fedha hizo kwa kuzingatia wingi wa watu na ukubwa wa mikoa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (K.n.y. WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Esther Kabadi Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipoanzisha mpango wa kuwawezesha wananchi kiuchumi na kuongeza ajira na kutenga Sh. 21bn/= iligawa fedha hizi kwa wastani wa Sh. 1bn/= kila mkoa ili kuwepo na mlingano kwa mikoa yote bila kujali wingi wa watu na ukubwa wa kila mkoa.

Katika kutekeleza mpango huo, Serikali imefanya tathmini za awali zilizolenga kuona mafanikio, upungufu na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa awamu ya kwanza. Baadhi ya mambo yaliyozingatiwa katika tathmini hizo ni pamoja na utoaji wa mikopo hiyo kwa wananchi na urejeshaji wa mikopo iliyotolewa. Tathmini hizo zililenga pia kutaka kufanya maboresho ya mpango huo ili uweze kuwa endelevu na wenye mafanikio.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, kwa kuwa mpango huu ni endelevu Serikali itaendelea kufanya tathmini za mara kwa mara na kwa kufanya hivyo kigezo alichokieleza Mheshimiwa Mbunge cha kutaka mgawo wa fedha za Mfuko huu zitolewe kwa kuzingatia wingi wa watu na ukubwa wa mikoa kitaangaliwa pia.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize maswali madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa utaratibu uliofanyika kwa mwaka jana ambapo ndiyo tulikuwa tunaanza wa kutoa kupitia *NMB* pamoja na *CRDB* na ikizingatiwa kwamba maeneo mengi ya vijijini walipo wananchi benki hizi hazipo. Je, katika kufanya tathmini yao ya kuona upungufu huo wamezingatia taasisi ambazo wamezielekeza sasa ziende moja kwa moja kwa wananchi huko vijijini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kabisa kwamba wamefanya tathmini na kuona kwamba kulikuwa na matatizo ambayo yalisababisha kutotoa fedha hiyo kulingana na wingi wa watu. Je, Serikali sasa haioni

umuhimu kabisa kuzingatia mikoa ambayo ina wingi wa watu kuweka kiwango kikubwa zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (K.n.y. WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge baada ya tathmini ile ya utekelezaji wa mpango wa kwanza, Serikali ilibaini mapungufu yaliyojitokeza pamoja na kukosekana kwa baadhi ya fedha hizi katika baadhi ya mikoa na wilaya. Kwa hiyo kilichofanyika Serikali iliteua asasi zingine za ziada kumi na tatu ambazo sasa hivi zimeshaanza kufanya kazi katika mikoa mbalimbali na kuzingatia zaidi katika maeneo ambayo hayakupata fedha katika mgawo ule wa kwanza.

Asasi hizi zimeshaelekezwa kwamba zijielekeze zaidi vijijini. Kwa taarifa ni kwamba kwa sababu maeneo yale yaliyokuwa yamekosa katika mpango wa kwanza sasa yamepangiwa kila wilaya Sh. 200m/= badala ya Sh. 100m/= ambazo zilitengwa katika maeneo mengine.

Na. 38

**Ajira kwa Vijana**

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliazimia kutoa ajira nyingi hasa kwa vijana kama Mheshimiwa Rais wetu alivyoahidi na kwa kuwa vijana wengi wa Kitanzania wamekuwa wakijitahidi kujitafutia ajira mbalimbali:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali inawasumbua vijana hao wanaohangaika kujitafutia ajira zao?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kutowasaidia vijana hawa ni kuzidi kuwaongezea umaskini?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (K.n.y. WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sevelina Silvanus Mwijage, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali sio kuwasumbua vijana wanaohangaika kujitafutia ajira na badala yake ni kuhakikisha kuwa vijana wengi wanawekewa mazingira mazuri ya kuweza kujiajiri wenyewe. Hata hivyo, katika mkakati wa kutekeleza Sera ya Maendeleo ya Vijana ambayo inalenga kuwa na vijana wenye maadili mema, malezi bora na wenye kuwajibika kwa jamii, taratibu, kanuni, sheria na utawala bora ni mambo ya msingi yanayozingatiwa.

Aidha, Serikali inatambua harakati za vijana wengi kujitafutia ajira mbalimbali ili kuweza kujikimu kimaisha. Hata hivyo, tatizo linalojitokeza hasa maeneo ya mijini ni ukiukwaji wa taratibu, kanuni na sheria unaofanywa na baadhi ya vijana kwa kufanya biashara maeneo yasiyoruhusiwa au kufanya biashara bila kibali au leseni kutoka mamlaka husika.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika ngazi mbalimbali inachukua hatua kadhaa ikiwa ni pamoja na kuwaelimisha vijana kuzingatia kanuni, taratibu na sheria ili waweze kufanya kazi, biashara zao bila kubughudhiwa na pia mamlaka husika kutenga maeneo maalum kwa ajili ya kuwawezesha vijana kujiajiri katika shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ni kujenga mazingira mazuri ya kuwawezesha vijana kimaendeleo na kuongeza nafasi za ajira na usalama wa vijana ili kuondoa umaskini. Aidha, kupitia Sera ya Maendeleo ya Vijana na Mfuko wa Maendeleo ya Mikopo kwa Vijana kupitia *SACCOS* zao. Serikali itaendelea kuwasaidia vijana na kuwapa fursa za kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali ili wajitegemee kiuchumi na kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni vema tukumbuke kwamba masuala ya vijana nchini ni mtambuka ambayo yanahitaji ushiriki na ushirikishwaji wa wadau mbalimbali ambao ni familia, jamii, asasi, taasisi mbalimbali na Serikali kwa ujumla kwenye kuwajengea uwezo vijana kutambua na kuzitumia nafasi zilizopo ili kukabiliana na changamoto zinazowakabili.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa vijana wengi wanajitahidi sana kuwa na ajira zao kwa mfano waendesha baiskeli, pikipiki, Machinga, wote huwa wanajitahidi kupata ajira. Je, ni lini Serikali itajitahidi itaona umuhimu wa vijana hao kuwapitishia sheria yao ya kuweza kuwasimamia kwenye biashara yao wasisumbuke sana? (*Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (K.n.y. WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swali la msingi, Serikali inaandaa mazingira mazuri ikiwa ni pamoja na kuandaa sera na sheria ambazo zinaongoza biashara za wajasiriamali ikiwemo na hiyo aliyoitaja. Kwa hiyo, naomba tu ushirikiano wa kila mmoja wetu. Sheria hizi na kanuni zitapokuwa tayari na kuanza kufanya kazi tushirikiane kuwaelimisha vijana ili waweze kuzitumia ili tuwanufaishe. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na muda wa maswali umepita. Kuna matangazo machache, wageni waliopo Bungeni leo pale *Speaker's Gallery* kuna wageni wa Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzania Bungeni nao ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Profesa Ibrahim Lipumba, Mwenyekiti wa Taifa wa *CUF*, nilimwona pale labda ana udhuru kidogo, aha, ameingia sasa, huyo hapo anatupungia mikono. Ahsante na karibu sana. (*Makofi*)

Yupo pia Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mwenyekiti wa Taifa Chadema. Ahsante sana Mheshimiwa Freeman. (*Makofi*)

Waheshimiwa hawa wamefuatana na viongozi wengine kutoka Vyama vya Upinzani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Said Miraji, Mjumbe wa Baraza Kuu la Taifa, *CUF.* Mheshimiwa Jumanne Doma, Kamisaa wa Mkoa, *NCCR-Mageuzi,* yeye hayupo. Dr. Muchi Haji, Mjumbe wa Baraza Kuu la Taifa *CUF* yule pale na bwana Thomas Mungi, Katibu wa Mwenyekiti wa *CUF.* Karibuni sana tunafurahi sana mnapokuja viongozi wa vyama mbalimbali kushuhudia jinsi Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanavyotekeleza kazi zao. Karibuni sana. Wageni wa Mheshimiwa Jacob Shibiliti ni Khalid Mbitiyaza, Diwani wa Kata ya Misasi, karibu sana Mheshimiwa Diwani na Bi Lucia Kahindi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Chiligati, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo Makazi anaye mgeni wake anaitwa Jeniffer Wright ambaye ni Mtanzania anayefanya kazi Uingereza na amekuja hapa kuwekeza katika sekta ya nyumba, *Real Estate Development Project*, yule pale. Ni Mtanzania, anaelewa Kiswahili. Kwa hiyo, sina haja ya kutafsiri haya ninayoyasema. Mheshimiwa Juma Njwayo, Mbunge wa Tandahimba ana mgeni wake ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mtwara Alhaj Dadi Khamis Mbulu, yule pale anapunga mikono. Karibu sana Mwenyekiti, wapo na mkewe sijui mke wa nani sasa, mke wa Mbunge au? (*Kicheko*)

Samahani, nadhani ni mke wa Mwenyekiti, wamekaa pamoja. (*Kicheko*)

Pia wapo watoto wa Mheshimiwa, Adila Juma Njwayo, yuko kidato cha nne *St. Anthony Secondary School,* Dar es Salaam na Chihindi Juma Njwayo. Huyu mdogo sana hajaanza hata darasa la kwanza, lakini tunamkaribisha. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Miundombinu Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, anao wageni ambao ni mwanawe Gladys na mume wake Wilson Chilewa, wale pale, nilihudhuria harusi yenu wikiendi iliyopita ilikuwa nzuri sana. Hongera sana tunawatakia maisha marefu ya ndoa. Hawa wanaishi Marekani na walikuja likizo kuja kufunga ndoa, pongezi sana wenzenu wengine wanamalizia huko huko, tunashukuru sana ninyi mmerudi nchini kuweza kufunga ndoa mbele ya wazazi na marafiki wa wazazi na ndugu zenu. Ahsante, tunawatakia mema.

Kuna ndugu zao wengine ambao ni Irene Chilewa, dada yake Wilson na Jacob Chibulunje, karibuni sana. (*Makofi*)

Pia kuna tangazo la mkutano, Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini anaomba wajumbe wote wa Kamati hiyo ya Nishati na Madini wakutane leo saa saba na nusu mchana katika ukumbi namba 231, Jengo la Utawala. Nami natangaza pia Makamishna wote wa Tume ya Huduma ya Bunge, tukutane saa saba na nusu katika Ukumbi wa Spika ili kuzingatia masuala muhimu yanayoendelea hivi sasa.

Tangazo kutoka kwa Chama cha Mapinduzi, kama ilivyo kawaida tunapopata wenzetu kuingia katika Kamati mbalimbali au wanateuliwa huwa tunatangaza, basi natangaza kwamba katika uchaguzi wa tarehe 14 juzi, kuwatafuta Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM kuingia katika Baraza kuu la Umoja wa Wanawake washindi waliopatikana wote watatu ni Wabunge. Kwa hiyo, washindi kwa kundi la Zanzibar ni Faida Mohammed Bakari na kundi la Tanzania Bara ni Dr. Aisha Kigoda na Mheshimiwa Waziri Sofia Simba. Hongereni sana. (*Makofi*)

Mwisho wa matangazo, Katibu kwa Shughuli inayofuata kwenye *Order Paper.*

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2007 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2008/2009 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali Kwa Mwaka 2008/2009

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja ilikwishatolewa ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha lakini napenda kuwakumbusha kwamba hoja hiyo ina sehemu mbili kwa maana kwamba ilitolewa hotuba asubuhi siku ya Alhamisi. Hotuba ya Hali ya Uchumi na jioni ikatolewa hotuba ya Bajeti. Kanuni yetu ya 96(7) inasema kwamba Mwenyekiti wa Kamati na Msemaji wa Kambi ya Upinzani wanaruhusiwa kutoa maelezo yao au taarifa kuhusu hotuba dakika thelathini kwa kila hotuba. Kwa hiyo, nitawaita sasa kwa mpangilio tukianza na Mwenyekiti wa Kamati halafu Msemaji wa Kambi ya Upinzani, kwa kanuni hiyo, sasa wanaruhusiwa kuongea kwa kipindi kisichozidi dakika sitini. Kwa hiyo, msishangae hilo. Kwa tangazo hilo sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa taarifa yake kuhusu hotuba zile.

**MHE. ABDALLAH O. KIGODA – MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 96 (6) cha Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kutoa maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2007 na mwelekeo katika kipindi cha muda wa kati (2008/2009 -2010/2011).

Mheshimiwa Spika, Kamati inampongeza Waziri wa Fedha na Uchumi Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkullo, kwa taarifa alizozitoa hapa Bungeni. Kupitia kwake Serikali imekuwa sikivu kwa mengi yaliyoshauriwa na Kamati na kwa kusema kweli Bajeti imegusia maeneo kadhaa ambayo kwa kiwango fulani yamejibu baadhi ya kero za Watanzania. Uamuzi wa kutokuongeza kodi za mafuta utatoa afueni katika maeneo yote ambayo athari zake ni za moja kwa moja.

Kwa mfano bei za mafuta zikipanda, gharama za chakula hasa mijini, uzalishaji, usafiri na kadhalika nazo hupanda. Punguzo la gharama za uzalishaji viwandani (kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye mafuta mazito ya *HFO* kimepunguzwa). Mfumo wa kodi binafsi ya mapato na mapato ya ajira umerekebishwa. Kima cha chini mshahara kimeongezeka, kodi katika baadhi ya pembejeo zimefutwa kabisa au kupunguzwa. Maeneo haya yatapunguza makali ya maisha kwa wananchi kwa kiwango fulani pamoja na sisi wananchi kufanya kazi kwa juhudi na nguvu.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii ya Kamati inaendelea kutoa maoni na ushauri wa ziada katika maeneo kadhaa ambayo tunahakikisha pia Serikali itayaangalia, yenye nia ya kuboresha utaratibu wa uendeshaji uchumi, pamoja na kuibua maeneo mengine ya kuongeza kasi ya kukua kwa uchumi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inawapongeza vile vile Manaibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Yussuf Omar Mzee na Mheshimiwa Jeremiah Solomon Sumari. Aidha, tunawapongeza Katibu Mkuu Ndugu Gray Mgonja, Gavana wa *BoT* Profesa Ndullu, Naibu Magavana Dr. Enos Bukuku na Juma Reli, Kamishna Mkuu wa *TRA,* Ndugu Harry Kitillya, Mwenyekiti wa Bodi ya *TRA,* Dr. Marceline Chijoriga na Wataalam wote tuliobadilishana mawazo katika kuboresha Taarifa hizi mbili zilizowasilishwa na Serikali hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2007 na Mwelekeo katika kipindi cha muda wa kati (2008/2009-2010/2011) pamoja na ile ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2008/2009, Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada zake za kuimarisha na kuboresha uchumi hususan Uchumi Mkuu na hivyo kuwezesha Uchumi wetu kuwa endelevu licha ya changamoto kubwa za upandaji wa kasi wa bei za mafuta pamoja na athari za mabadiliko ya tabia nchi ambayo yalileta ukame na hivyo kupunguza uzalishaji wa chakula si nchini tu bali duniani.

Mheshimmiwa Spika, Pato halisi la Taifa lilikua kwa asilimia 7.1 mwaka 2007 ikilinganishwa na asilimia 6.7 mwaka 2006. Kasi ya upandaji bei imefikia asilimia 9.7 mwezi Aprili 2008, wakati ukuzaji rasilimali umeongezeka na kufikia Sh. 6,209,741m/= mwaka 2007, kutoka Tsh.4,957,781m/= mwaka 2006, ongezeko la asilimia 25.3. Uwiano wa ukuzaji rasilimali kwa Pato la Taifa ulikuwa asilimia 29.6 ukilinganisha na asilimia 27.6 mwaka 2006. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana ulikuwa asilimia 21.4, Desemba 2007, ikilinganishwa na asilimia 22 Desemba, 2006. Mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka kutoka Sh.2,028,294.3m/= Desemba 2006, hadi Sh.2,883,789.5m/= Desemba 2007. Viwango vya riba kwa amana za akiba viliongezeka kidogo kutoka asilimia 2.54 Juni 2006, kufikia asilimia 2.75 Desemba 2007. Riba za mikopo ya muda mfupi na muda mrefu iliongezeka kutoka asilimia 15.44 Juni 2006 hadi asilimia 15.71 Juni 2007.

Mheshimiwa Spika, Deni la Taifa lilipungua kwa asilimia mbili kutoka dola 7,188.4 milioni Desemba 2006, hadi dola 7,041.3 milioni mwaka 2007. Thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje iliongezeka kutoka dola 3,230.2 milioni mwaka 2006 hadi dola 3,703.6 milioni mwaka 2007, ongezeko la asilimia 14.7. Thamani ya bidhaa

zilizoagizwa kutoka nje iliongezeka kutoka dola 3,864.1 milioni mwaka 2006 hadi dola 4,826.9 milioni mwaka 2007, ongezeko la asilimia 24.9. Akiba ya fedha za kigeni iliongezeka kwa asilimia 21.9 kutoka dola 2,260.1 milioni mwaka 2006 hadi kufikia dola 2,755.2 milioni mwaka 2007, sawa na thamani ya uagizaji wa bidhaa na huduma kwa miezi 4.6. Mapato halisi ya ndani kuanzia Julai 2007 hadi Machi 2008 yalifikia Sh.2.65 trilioni ikilinganishwa na Makadirio ya Sh 2.63 trilioni. Hadi kufikia Machi 2008, matumizi yote yalifikia Sh. 4.15 trilioni, ikilinganishwa na makisio ya Sh.4.84 trilioni.

Mheshimiwa Spika, Kamati imehakikishiwa kuwa juhudi kubwa ilielekezwa kwenye udhibiti wa manunuzi, uwezeshaji wa wananchi kiuchumi pamoja na kuboresha uhusiano wetu na wahisani. Aidha, Kamati imeipongeza Serikali kwa dhamira yake ya kupunguza utegemezi wa bajeti ya Wafadhili kutoka asilimia 42 hadi 34 katika kipindi kijacho. Katika mwaka wa fedha 2008/2009, Serikali imepanga kupata mapato ya Sh.7.216 trilioni, mapato ya ndani yakiwa Sh.4.728 trilioni. Huu ni mwelekeo mzuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata taswira hii ya Hali ya Uchumi na Mwelekeo wa Bajeti kutoka Serikalini, Kamati iliibainisha Serikali kuwa changamoto kubwa mbele yake ni kuona ni jinsi gani menejimenti ya Uchumi Kitaifa itawezesha mafanikio haya ya uchumi mkubwa kutiririka vijijini, hususan katika eneo la kuongeza mapato ya wananchi wengi ili kupunguza umaskini wa kipato vijijini na mijini. Tutakapoweza kufanikiwa katika lengo hili, tutakuwa tunazungumzia ukuaji wa uchumi (*economic growth*) unaoendana na maendeleo ya uchumi (*economic development*) hasa ikizingatiwa kuwa uchumi jumla umekuwa na kufikia asilimia 7 na zaidi. Aidha ni dhahiri kabisa kuwa uchumi wa nchi unapambana hivi sasa na changamoto za uendeshaji na usimamizi zinazotokana na mazingira ya kiuchumi ya ndani na nje.

Kwa upande wa ndani, Kamati inaainisha mapungufu ya kutumia fursa zilizopo kikamilifu ili hatimaye tuibue uchumi wetu kupitia matumizi ya tija na ufanisi ya rasilimali zetu. Bado hatujafanikiwa kuendeleza kwa kasi sekta zetu za uzalishaji mali moja kwa moja, hususan kilimo, uvuvi, mifugo na maliasili (misitu). Hali hii ina athari si tu katika ongezeko la pato la Taifa, bali hata katika dhana nzima ya kupunguza umaskini wa kipato, ambao unawafanya wananchi wengi kujikuta wana hali ngumu ya maisha kwa ukosefu wa uwezo au nguvu ya kununua bidhaa zao muhimu *(weak purchasing power)*.

Mheshimiwa Spika, athari hii ikichanganyika na zile za vyanzo vya nje, hasa vinavyotokana na mfumko wa bei kutoka nje (*imported inflation)* inahitaji mikakati ya ziada. Kwa mfano upandaji wa kasi wa bei za mafuta duniani, gharama kubwa za chakula zinazotokana na nafaka sasa kuwa nishati mbadala, pamoja na matatizo ya hali ya hewa duniani yameleta upungufu mkubwa wa chakula, kuzorota kwa utendaji wa taasisi za kifedha duniani, hivi ni viashiria tosha vya haja ya usimamizi mzuri wa kuendesha uchumi wetu ambao haujakomaa sana.

Hapa niseme Kamati imezipokea vyema taarifa zote za Hali ya Uchumi na ile ya mwelekeo wa Bajeti. Taarifa hizi kwa ujumla wake zimebainisha mfumo wa uchumi mkuu na jinsi gani vipaumbele mikakati vinatafsiriwa kupitia utengaji wa rasilimali baina ya sekta mbali mbali. Ni muhimu katika utekelezaji wa mpango na programu mbalimbali, vyanzo vya ukuaji kutoka sekta zinazozalisha na sera za ukuaji zieleweke vizuri katika ngazi zote ili kuweka misingi ya Serikali ya mwelekeo wa ukuaji na kutathmini uwiano sahihi kati ya Pato la Taifa na mwelekeo wa ukuaji katika sekta mbalimbali. Utaratibu huu utasaidia pia kulinganisha ukuaji na sera za kisekta, pamoja na aina za sera za kodi pamoja na utengaji wa bajeti ulivyofanyika katika kila sekta.

Kamati ilipenda kujua ni vipi Bajeti ilivyotengwa baina ya sekta itakuza uchumi kama ilivyooneshwa. Changamoto ni kama malengo yaliyowekwa, yamezingatia hali halisi ya maeneo yanayosaidia kukuza uchumi. Kamati imeishauri Serikali iweke msisitizo wa kuibua vyanzo vya ukuaji wa uchumi, kwa mfano ni jinsi gani sekta mbalimbali zitachangia ukuaji na ni sera gani kwa mfano, sekta binafsi, uwekezaji mitaji, marekebisho ya kimfumo, kodi, bajeti na kadhalika zinazohitajika kwa kuendeleza utendaji wa kisekta. Ni matatizo au vikwazo gani vinavyoathiri utendaji kisekta na Serikali imejiandaa kuchukua hatua gani kupunguza au kujibu athari zitokanazo. Kamati vile vile ilitaka kuelewa kama Serikali imejizatiti na athari zitakazojitokeza kutokana na maeneo makuu ya uchumi nje ya mazingira ya nchi yetu, hususani masuala ya uzalishaji duniani, bei za dunia, viwango vya fedha za wafadhili, juu ya matarajio yanayopangwa ya ukuaji wa uchumi.

Maeneo haya ni changamoto.Kamati imeishauri Serikali kuwa kutokana na kuwepo kwa athari za kiuchumi ambazo ni nje ya uwezo wa nchi yetu, ipo haja ya Serikali kubuni na kujiandaa na utaratibu mbadala wa hadhari ili kupambana na changamoto hizi tulizozielezea pamoja na uwezekano wa uchumi wa dunia kuzorota, mwelekeo wa misaada kutoka nje na mwelekeo wa biashara. Serikali ikifanikiwa katika haya itasaidia kuweka viwango makini vya ukuaji wa Pato la Taifa, rasilimali za ndani na za nje na hivyo kujenga misingi imara ya utekelezaji wa kufikia malengo ya uchumi yaliyowekwa. Kamati imebaini kuwa nia ya Serikali ya kupunguza utegemezi kwa asilimia saba, kuendelea kudhibiti mfumko wa bei na hatimaye kukuza viwango vya ukuaji wa Pato la Taifa na Uchumi ni changamoto inayoitaka Serikali kuwa na:-

(i) Lengo la kudhibiti upanuzi wa mahitaji ya uchumi (*aggregate demand*) na hivyo kupunguza mfumko wa bei.

(ii) Lengo la kusimamisha upanuzi wa programu za umma na badala yake kutumia nguvu kubwa katika kuboresha thamani ya fedha (*Value for Money*) zinazotumika katika matumizi ya Serikali na umma.

(iii) Lengo la kupunguza kutegemea misaada toka kwa wafadhili au kama si tahadhari tu iliyochukuliwa katika mwelekeo wa matumizi ya raslimali za nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, mantiki ya maelezo haya hapo juu ni kusisitiza kuwa dhana nzima ya bajeti hii iweze kutoa majibu au ufumbuzi wa matatizo yanayowasibu wananchi hivi sasa. Tatizo kubwa linalojitokeza ni dhana ya uchumi kukua kutokana na ongezeko

la pato la mtu (*per capita income*) na Pato la Taifa, wakati wananchi wengi wanalalamika kuwa maisha ni magumu, hususan kutokana na kupanda kwa gharama za maisha, kunakogusa maeneo yote muhimu.

Kamati imeishauri Serikali umuhimu wa kuongeza uratibu katika vyombo vyake vya utendaji ili kuboresha eneo la kuendesha uchumi (*economic management*) badala ya kuelekeza nguvu zote kwenye kuendesha au kulinda utulivu wa bei (*price stability management*) unaoathiriwa na mfumko mkubwa wa bei.

Kwa ujumla wake ushauri wa Kamati uliegemea katika maeneo mawili yafuatayo. Kwanza, ni vipi Serikali itatumia vyema fursa ya hali halisi ya uhaba wa chakula duniani kupitia kuendeleza sekta yetu kuu ya Kilimo. Pili, pengo kati ya mapato na matumizi hasa kwa wananchi wa kipato cha chini, litazibwa vipi ili kupunguza makali ya maisha.

Mheshimiwa Spika, Bila ya mikakati madhubuti ya menejimenti ya uchumi, athari zake ni uchumi kushindwa kuibua fursa zilizopo kwenye maeneo ambayo yatazalisha mali moja kwa moja na kwa haraka.

Aidha, hali hii inaweza kupunguza kasi ya kukua kwa uchumi kutokana na kutokuzingatia vipaumbele tulivyojiwekea. Kwa mfano, malengo ya mfumko wa bei kama yalivyoainishwa na MKUKUTA ni asilimia nne. Hata hivyo, mfumko huu umeendelea kuongezeka na kufikia asilimia 6.5 mwezi Machi 2006 na hatimaye kufikia asilimia 9.5 Aprili, 2008.

Hali hii imetokana na kupanda kwa bei za mafuta, chakula hasa mijini, vifaa vya ujenzi, usafiri na kadhalika. Inawezekana kabisa kupitia utaratibu mzuri wa menejimenti ya Uchumi, Serikali ikaangalia mikakati ya kuhuisha na kuboresha aina mbalimbali za kodi zetu, mafuta, udhibiti imara wa ujazi wa fedha katika uchumi na kuchukua hatua za makusudi za kuweka vivutio katika sekta zinazozalisha ili kuongeza tija, pamoja na kuvutia wawekezaji wakubwa kuwekeza hususan katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mikakati na Programu zilizopangwa ili kuendeleza kilimo kupitia *ASDP, PADEPS, DADPS* na kadhalika, bado mchango wa Kilimo katika Pato la Taifa ni mdogo. Taarifa iliyoandaliwa na Benki Kuu ya Aprili, 2008 iliyozungumzia sura mpya ya uchumi wa nchi yetu, mchango wa kilimo uliteremka toka asilimia 30.3 mwaka 1998 hadi kufikia asilimia 25.4 mwaka 2006. Mchango wa viwanda na ujenzi umeongezeka kutoka asilimia 16.7 mwaka 1998 hadi asilimia 20.5, wakati huduma nazo zimeongezeka pia kutoka asilimia 45.2 hadi asilimia 46.9. Katika kipindi cha miaka sita (2001 - 2006), uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia saba kwa mwaka. Sekta zilizoongoza kwa ukuaji ni madini (15.9%), ujenzi (11.0%), huduma za kifedha (9.7%), viwanda (8.2%) na mawasiliano na uchukuzi (8.0%). Kwa upande wa vyanzo vya mauzo nje, mauzo ya bidhaa na huduma nchi za nje yaliongezeka toka US$1,157.4m mwaka 1998 hadi US$ 3,736.1m mwaka 2007. Mchango wa mauzo ya bidhaa za asili ulipungua kutoka asilimia 30.8 ya jumla ya mauzo yote mwaka 1998 hadi kufikia

asilimia 8.5 mwaka 2007. Bidhaa zisizo asilia ziliongezeka kutoka asilimia 69.2 mwaka 1998 hadi 91.5% mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa sura hii ya uchumi inavyojionyesha, inatushawishi kuwa uchumi wetu unategemea sana sekta ya huduma ili kukua. Kwa uchumi ambao haujatengemaa sana kama wa nchi yetu, kutegemea sekta ya huduma ili kukuza uchumi wake, haileti sura na mwelekeo endelevu. Kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali, jitihada zake zielekezwe katika kuinua sekta ya kilimo kwa kuchukua hatua madhubuti na haraka.

Mheshimiwa Spika, kwa maana nyingine, Kamati ilipopata maelezo ya uchumi wa nchi kuchukua sura mpya na hivyo kutegemea vyanzo visivyo vya asili *(non traditional sector)*, kwa mfano madini, utalii na huduma nyingine, ilichukua dhana hii kwa tahadhari kubwa. Uchumi ambao haujatengemaa zaidi kama wa nchi yetu, uchumi ambao kwa njia yoyote utategemea kilimo kwa muda mrefu ujao, hauwezi kuwa endelevu kwa kutegemea sekta ya huduma. Sekta za madini, utalii na kadhalika, zina *risks* nyingi. Kwa mfano, baada ya Marekani kupigwa mabomu na magaidi Septemba 11, utalii uliyumba kwa muda mrefu sana duniani kote.

Hali hii inafanya Serikali iangalie ni jinsi gani itaibua kwa kasi zaidi sekta ya kilimo, uvuvi na maliasili kwa kutumia fursa zote zilizopo.

Kilimo kuchangia asilimia nne ya Pato la Taifa si kigezo cha kuonyesha uchumi wa nchi umeendelea, hususan kama hakijamudu kuzalisha chakula cha kutosha na kuwa na akiba ya Taifa na kama hakijaweza kutoa malighafi kwa viwanda vinavyozalisha bidhaa za kilimo nchini kama vile matunda, korosho, tumbaku, pamba na kadhalika. Nchi nyingi duniani zinaingia katika awamu ya uchumi unaotegemea viwanda *(Industrialized Economy),* baada ya sekta ya kilimo kuwa endelevu na inayojitosheleza. Bado yapo maeneo ya kufanyia kazi hususan Sheria zetu na Kodi ambazo zinatozwa, mazao/bidhaa za kilimo ambazo zinatarajiwa kusaidia viwanda vya ndani ya nchi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Vivutio katika Kilimo; Kamati ina maoni kuwa pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kupunguza mizigo katika shughuli za Kilimo, bado hatua zilizochukuliwa hazijakuwa za kina na mapana ili ziweze kusaidia ngazi zote za wakulima ambao hutumikia sekta inayoajiri takriban asilimia 75 ya Watanzania wote.

Bajeti ya Serikali 2008/2009 imeonyesha kuwa, itaelekeza fedha nyingi katika ruzuku ya mbolea, Hifadhi ya Taifa ya Chakula, utafiti wa mbegu bora na mafunzo. Sekta binafsi itahusishwa katika upatikanaji wa mbolea na matrekta, pamoja na ujenzi wa viwanda vya kusindika mazao. Aidha, maeneo mengine yaliyoguswa ni kuondoa ushuru wa forodha kwenye majembe ya mikono, pamoja na pembejeo za kilimo zinazoagizwa kutoka nje, pamoja na kuondoa ushuru wa forodha wa asilimia kumi kwenye mafuta ghafi ya kula.

Mheshimiwa Spika, Kamati ingeitaka Serikali kuchukua hatua zaidi ili kuleta historia katika kuendeleza kilimo nchini katika kipindi hiki. Katika kipindi hiki, Serikali ichukue uamuzi wa makusudi wa kuweka vivutio katika kilimo vitakavyogusa wakulima wote nchini, kwa maana ya wale wadogo vijijini, wale wa kati na wale wakubwa ili wazalishe zaidi.

Hatua zilizochukuliwa katika bajeti hii, zinaonekana kuwagusa zaidi wakulima wa kati na wale wakubwa. Bado vivutio kwa wakulima wadogo na walio wengi havijatosheleza. Aidha, changamoto nyingine ni uthibitisho na usahihi wa utekelezaji wa hatua zilizoorodheshwa, kwa mantiki ya kuwasaidia walengwa, tofauti na kutotekelezwa kwa hatua husika. Hatua ni nzuri; hoja ni kuwa je, zitatekelezwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuleta mageuzi katika kilimo chetu kupitia vivutio hivi vya makusudi (*purposeful incentives*), Kamati inapendekeza na kuishauri Serikali ichukue hatua zifuatazo;-

Kwanza: bajeti ya kilimo kupitia programu zote za *ASDP, DADPS, MCD,* fedha za umwagiliaji zote zinazoelekezwa kwenye Halmashauri za Wilaya, zisimamiwe kikamilifu ili matumizi ya fedha hizi yalingane na matokeo ya uzalishaji (*Value for Money*). Kamati inashangaa kwamba, fedha nyingi zinaelekezwa kwenye kilimo, lakini uchangiaji wake katika Pato la Taifa unaendelea kupungua mwaka hadi mwaka. Hoja hapa si kuongeza bajeti ya kilimo pekee, bali ni uhakika wa matumizi mazuri ya tija na ufanisi kulingana na fedha zinazotengwa.

Pili: Serikali bila kusita, ipunguze au kufuta kabisa kodi za ushuru wanazolipa wakulima wadogo kwenye Serikali za Mitaa. Nyingi ya kodi au tozo hizi mara nyingine huwa ni kero kwa wakulima wadogo. Takwimu zinaonyesha kuwa, mkulima anatakiwa kulipia mara 17 ya kodi anayolipa mwenye kiwanda (asilimia tano ilikinganishwa asilimia 0.3)

Tatu: Kodi ya ardhi ipunguzwe kutoka Sh. 200 za sasa kwa eka hadi kufikia Sh. 50.

Nne: Kodi na gharama za nyenzo, pembejeo, zana kwa mfano, matrekta na plau, zipunguzwe kwa kiwango kikubwa ili zipate kuwahudumia wakulima wadogo, hususan kwa kupitia taratibu kama vile za "*financial leasing.*"

Tano: Kodi za *VAT,* ajira na mapato wanazopaswa kulipa wakulima wadogo zifutwe. Kwa maana nyingine, kodi zote za dhahiri (*direct taxes*) na zile zisizo za dhahiri (*indirect taxes*), zinazowaangukia wakulima wadogo zifutwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mantiki ya Kamati ni kuishauri Serikali, ichukue maamuzi ya makusudi juu ya hatua hizo hapo juu ili yawapanguzie mzigo wakulima wadogo, wa kati na wale wakubwa (*contract and commercial farmers*). Sekta ya Kilimo pekee, ndio yenye uwezo wa kuondoa uchumi wetu hapa ulipo ikiwa Serikali itatoa kipaumbele na kuweka vivutio vitakavyoweza kuimarisha na kukuza uzalishaji katika sekta hii muhimu.

Kamati inapendekeza eneo hili lifanyiwe uamuzi wa haraka ili kuboresha sekta inayoajiri takriban asilimia 75 ya Watanzania wote. Aidha, kwa dalili za sasa duniani, uzalishaji katika kilimo utakutana na changamoto kubwa, tukizingatia nchi zilizokuwa zinatuuzia chakula kwa mfano, Vietnam, India na kadhalika, hivi sasa zimesitisha kuuza chakula nje. Kama alivyosisitiza Waziri wa Fedha mwenyewe katika hotuba yake ya Bajeti, alisema na ninanukuu: "Ni vizuri tuitumie changamoto ya upungufu wa chakula duniani, kama fursa kubwa ya kuneemeka kwa kuzalisha chakula chetu wenyewe kwa wingi, kwa kuwa ardhi tunayo, watu tunao na hali ya hewa nzuri inaruhusu." Hali hii itawezekana tu, ikiwa tutajiwekea mazingira mazuri ya uwekezaji katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na hali hii, Kamati inatoa angalizo kuwa zoezi zima la kutoa maamuzi (*decision making process*), halina budi kuangaliwa kwa kina, ili kupunguza urasimu, pamoja na gharama za uzalishaji na biashara katika sekta ya kilimo. Kodi na baadhi ya sheria zetu zimedumaza maendeleo ya kilimo, hasa kilimo kikubwa cha biashara kinachohitajika hivi sasa kwa nguvu zote. Sekta ya kilimo nchini inazorota kutokana na ukosefu wa mitaji na Kamati imeisisitizia tena Serikali kutekeleza azma ya kuanzisha Benki ya Maendeleo ya kilimo. Hatua ya Bajeti kutenga shilingi bilioni 21 kwa ajili ya kuimarisha mtaji wa Benki ya Raslimali ni hatua ya kupongezwa. Maeneo mengine ambayo yanahitaji kupimwa tija yake na ufanisi kutokana na gharama inayoingia Serikalini ni pamoja na eneo la ruzuku ya pembejeo kwa wakulima. Umakini mkubwa unahitajika ili pembejeo hizi ziwafikie wakulima kwa wakati na kwa viwango vya bei wanazomudu, ama sivyo pembejeo hizi zinaweza zisilete mafanikio yaliyolengwa katika sekta na hata pembejeo hizi kuuzwa nje ya nchi yetu. Uwakala wa pembejeo zote ufanyiwe tathmini ili ulete tija na ufanisi katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imetafakari kwa kina utendaji wa taasisi za fedha nchini, hususan mabenki ya biashara katika kuchangia kukua kwa uchumi. Takwimu za Benki Kuu, zinaonyesha kuwa mikopo kwa sekta binafsi imeongezeka. Kiuwiano kwa kulinganisha jumla ya amana; mikopo hii ilikua kutoka asilimia 54.6 Juni 2007, hadi asilimia 61.8 Aprili, 2008. Kamati inajiuliza mikopo hii imeelekezwa katika maeneo yapi na matokeo yake ni yapi, ikilinganishwa na ukuaji wa uchumi wa nchi na kasi ya ongezeko la Pato la Taifa? Kwa mfumo wa Benki zetu nyingi (*commercial banks*), hapa nchini, inakuwa ni vigumu kukopesha wakulima kwa vile haziwezi kutoa mikopo ya muda mrefu na yenye riba nafuu. Takwimu zinaonyesha kuwa, kwa wastani, mwaka 2007 jumla ya mikopo yote ni asilimia kumi tu ilienda kushughulikia kilimo na kati ya fedha hizo ni asilimia saba tu zimeelekezwa kwa wazalishaji wa moja kwa moja. Hili ni eneo linalohitaji kufanyiwa kazi na Serikali kwa haraka. Uanzishwaji wa Benki za Uwekezaji, Maendeleo na Kilimo, ufanywe haraka ikiwa lengo ni kufikia ukuaji wa Pato la Taifa kufikia asilimia nane hadi kumi katika kipindi cha muda mfupi ujao.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu baada ya kubadilishana mawazo na Benki Kuu, imejenga dhana kuwa Benki nyingi nchini zina fedha nyingi au ukwasi wa ziada *(excess liquidity)* na hivyo kuzifanya kutokuona umuhimu wa kukopesha wananchi, kutokana na utaratibu wa kununua Amana za Serikali na Hatifungani *(Treasury Bonds* na *Government Securities).* Hali hii imeleta mazingira ya Benki karibu zote, kuwa na faida kubwa katika uchumi huu wenye kiu kubwa ya mitaji kupitia mikopo, hasa kwa

wakulima wadogo. Ugumu wa kupunguza riba za mikopo katika mabenki mengi ni kiashiria kinachoimarisha na kuunga mkono dhana hii ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, ingawa kwa mabenki hali ya ukwasi wa ziada ni faida kwao, kwa upande wa uchumi wa Tanzania, una athari zinazoweza kupunguza kasi ya maendeleo nchini:-

Kwanza, ni tatizo la kutofanyia kazi au kutokuangalia viwango vya tija vya riba na matokeo yake ni kutoza riba ya asilimia 15 – 25 ya riba kwa wanaokopa na hivyo, kuongeza sana gharama ya mikopo. Takwimu zinaonyesha kuwa, Tanzania yenye idadi ya watu takriban zaidi ya milioni 40 ni watu 1,600,000 tu wanaotumia huduma za mabenki. Aidha, viwango vya kuweka amana havijafikia zaidi ya asilimia nne. Kwa hali hii ni vigumu kuona faida na matokeo ya mikopo katika uchumi, licha ya kuwa na Benki zaidi ya 35 hivi sasa.

Pili, hali hii inawezekana kabisa kuchochea *conspicuous expenditure,* baina ya mabenki pamoja na matumizi makubwa ya fedha *(golden packages)* katika taasisi za fedha na hivyo, kuathiri matumizi yanayolenga uzalishaji wa moja kwa moja unaoweza kuibua uchumi.

Tatu, hali hii inaashiria umuhimu wa Benki Kuu, kuimarisha wajibu wake wa kusimamia, kudhibiti na kufuatilia utendaji kazi wa Benki hizi nchini *(supervision role).*

Nne, athari kubwa zaidi ni kuwa ukwasi wa ziada *(excess liquidity)* katika Mabenki hayo, hususan yale ya Kimataifa, yanaweza yakachochea utaratibu wa kuhamisha au kukimbiza mitaji nje ya nchi *(capital flight)*. Ununuzi wa amana za Serikali unaosababisha ukwasi wa ziada, unawezesha Benki nyingi kutengeneza faida kubwa na zisizo za kawaida *(super and abnormal profits)*, kwani upatikanaji wa faida hii kimsingi haukutokana na kuelekeza mikopo katika shughuli za kukuza uchumi wa nchi kama vile kilimo, viwanda vya kati *(SMEs),* shughuli za wajasiriamali *(Entreprenuership),* miundombinu na kadhalika, pamoja na *direct productive sectors;* bali kupitia ununuzi wa amana na hatifungani za Serikali. Ukimbizaji wa mitaji nje unaweza kuwa ni wa kiwango kikubwa. Hili ni tatizo ambalo Serikali inabidi ilisimamie kwa uzito wote.

Tano, Kamati inapata taswira ya kuwa ama tunazo Benki nyingi ambazo hazilingani na uwezo wa wananchi kuzitumia au zisizolingana na uwezo mdogo wa uchumi wetu kujiendesha kwa kutumia taasisi hizi muhimu. Hali hii si nzuri kwa uchumi unaohitaji kukua kama wetu, hasa tukitambua kuwa, bado hakuna jitihada za makusudi za kutumia nyenzo za mikopo, ambazo hazijagusa maeneo mengi kwenye uchumi. Mara nyingi tukiangalia mizania za mabenki yote *(balance sheets),* zinaonyesha kuwa, faida kubwa inatokana na ununuzi wa amana na hatifungani kutoka Serikalini. Benki Kuu itafute mikakati ya haraka, itakayowezesha hatua za kupunguza viwango vya riba vya kukopa. Kwa utaratibu huu, mchango wa Taasisi zote za Fedha katika Uchumi wa Taifa utakuwa ni mkubwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kuondoa fedha zake zinazowekwa katika Benki ya Biashara na kuhamishia Benki Kuu, kama ilivyoahidi katika Bunge hili tokea Juni, 2006. Zoezi hili liwe la haraka kwa faida ya uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati inaamini kuwa, uwekezaji ili ushamiri katika nchi ni lazima ujengewe mazingira mazuri na ya kuvutia. Fedha za kigeni na hata fedha za ndani haziwezi kuingia na kuwekezwa kwa ajili ya kukuza Uchumi, iwapo fursa kubwa inaelekezwa kwenye ununuzi wa Amana na Hatifungani. Mafanikio ya Benki nchini, yanaweza kuonyesha matokeo kuwa shughuli za kibenki na watumiaji wakubwa wa huduma zake, zinafanyika tu baina ya Serikali, Benki ya Biashara na Benki Kuu, badala ya wananchi. Hali hii haitaleta tija inayotarajiwa katika kukuza Uchumi wa Nchi.

Mheshimiwa Spika**,** mwisho wake, uuzaji wa Amana za Serikali kwenye Mabenki, unaigharimu Serikali fedha nyingi hasa kwa upande wa riba na tozo nyingine (*financial charges*). Ni vyema Serikali sasa ili kutumia huduma za mabenki kwa tija na ufanisi na kwa faida ya kukuza Uchumi wetu, iweke masharti mahususi yatakayoimarisha usimamizi na ufuatiliaji mzuri wa Mabenki haya kupitia Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, *TRA* imeendelea kufanya vizuri kama chombo cha kuongeza mapato ya Serikali. Hivi sasa inakusanya zaidi ya Sh. 289.1 bilioni kwa mwezi, kama mapato kutoka vyanzo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutokuchukua hatua za kuongeza kodi katika bidhaa za mafuta, ambazo zimekuwa zikipanda na zinaendelea kupanda kwa kasi kubwa mno. Mara nyingine, bei hizi zinapanda wala si kwa sababu ya kuongezeka kwa gharama za uzalishaji; zipo taarifa za kiuchumi zinazoonyesha kuwa, kwa hali hii ya uchumi wa dunia tunayokwenda nayo, bei ya pipa la mafuta lisilosafishwa litafikia US$ 200, baada ya muda si mrefu. Likitokea hili, athari zake katika uchumi mdogo kama wetu zitakuwa ni kubwa. Uamuzi huu wa Serikali, umesaidia kuondoa ule utaratibu wa bajeti yetu kuwa tegemezi kwa maeneo fulani fulani, mwaka hadi mwaka, yaani *budget based on variables.* Bajeti ya mwaka ujao, imeshaanza kuchukua hatua za kupanua wigo wa kodi, kitendo ambacho Kamati inakiunga mkono. Katika kipindi hiki kwa Bajeti yetu kutegemea kodi za mafuta, kama chanzo kikubwa cha mapato, inaashiria (*presupposes)* kuwa Tanzania tunazalisha mafuta, wakati si kweli.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Serikali wa kutokuongeza kodi za mafuta, umepunguza kwa kiwango Fulani, athari zilizo nje ya uwezo wetu katika mchakato wa kuendesha uchumi wetu.

Kwanza ni mfumko wa bei kutoka nje (*imported inflation*); nchi zinazozalisha mafuta zimepandisha mno bei za mafuta. Tunatumia fedha nyingi za kigeni, wakati bado hatujautengemaza uchumi wetu. Uchumi wetu sio *Commanding Economy* na ndio maana Tanzania ni nchi inayoendelea. Kutokana na hali hii, kama Serikali ingeongeza kodi za mafuta kama njia ya kuongeza mapato, uchumi wetu na wananchi wangelipa kodi mara mbili, yaani *double taxation* na hivyo kuongeza zaidi ukali wa maisha.

Kodi ya mafuta ikiongezeka nchini, haitagusa mafuta tu, bali itaongeza gharama maradufu katika maeneo yote kama usafiri, uzalishaji, ununuzi wa bidhaa na kadhalika. Hali ambayo itazidisha ugumu wa maisha, hasa kwa wananchi wenye kipato cha chini. Aidha, athari za hali hii zitakuwa mtambuka na kugusa tabaka zote za wananchi. Hivi sasa katika uchumi wetu, kutokana na kupanda kwa bei za mafuta katika soko la dunia, tayari kumeathiri na kupunguza uwezo wa ununuzi baina ya wananchi (*low purchasing power*). Serikali kupitia *TRA*, iendelee na zoezi la kutafuta vyanzo vingine vya mapato hususan katika maeneo ya maliasili, utalii, madini vyombo au makampuni ya mawasiliano na simu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza Serikali iandae na mikakati ya kuhimili kupanda kwa bei za mafuta katika soko la dunia. Ni dhahiri kuwa, bei zitakavyoendelea kupanda na dalili zinaonyesha mwelekeo wa kupanda tu na si wa kuteremeka, Serikali italazimika kutenga fedha za kutosha za kununua mafuta ya akiba kupitia *TPDC.* Kamati inadhani utaratibu huu, utapunguza makali ya maisha kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, idadi ya walipa kodi wakubwa imeongezeka hadi kufikia 370 hadi Julai, 2006, ambao hulipa takriban asilimia 74.8 ya mapato ya ndani. Changamoto kubwa kwa Serikali ni ile ya kukusanya kodi katika sekta isiyo rasmi, inayochangia Pato la Taifa kwa asilimia 30. Eneo hili lifanyiwe kazi.

Eneo lingine ambalo linahitaji kufanyiwa kazi ni lile la kupunguza misamaha ya kodi iliyowekwa kisheria kwa asilimia 50 ili kuongeza mapato yatakayoelekezwa katika kujenga uchumi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, makusanyo halisi yalikuwa ni Sh. 883.6 bilioni wakati misamaha ya kodi ilikuwa Sh. 385.4 bilioni au asilimia 44 ya mapato yote. Katika mwaka 2006/2007, makusanyo yalikuwa ni Sh. 1,132.4 bilioni, wakati misamaha ilikuwa Sh. 359 bilioni au asilimia 32. Hii ni kwa upande wa Idara ya Forodha. Kwa Idara ya Kodi za ndani, makusanyo yalikuwa ni Sh. 499.3 bilioni na misamaha ilikuwa Sh. 374.8 bilioni au asilimia 75. Katika mwaka 2006/2007, makusanyo yalikuwa ni Sh. 633.5 bilioni, wakati misamaha ilikuwa Sh.460.9 bilioni au asilimia 73. Kwa upande wa Zanzibar, Idara ya Forodha ilikusanya Sh. 14.5 bilioni na misamaha ilikuwa Sh.11.7 bilioni au asilimia 81 mwaka 2005/2006. Kwa mwaka 2006/2007, makusanyo yalikuwa ni Sh.20.4 bilioni na misamaha ilikuwa ni Sh.19.6 bilioni au asilimia 96 ya mapato yote.

Mheshimiwa Spika, viwango vya misamaha ya kodi ni vikubwa na vinaathiri ujazo wa mapato. Kamati inashauri Bunge lako Tukufu, pamoja na Serikali, kufanya zoezi la kuhuisha baadhi ya sheria zetu, ili kupunguza misamaha ya kodi. Hivi sasa misamaha hii ni asilimia tatu ya Pato la Taifa, badala ya kuwa asilimia moja. Jirani zetu Kenya, Uganda, Msumbiji na kadhalika, ambao ni maskini kama Tanzania, hawana utaratibu wa misamaha ya kodi. Sheria zinazopaswa kuhuishwa na kuangaliwa ni pamoja na zile za Madini, Kituo cha Uwekezaji, *VAT* na kadhalika. Kamati inaipongeza Serikali kukubaliana na ushauri ulioutoa kwa kufanya marekebisho katika Jedwali la

Tatu la Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamini ili kuimarisha usimamizi wa misamaha ya kodi unaotolewa kwa Mashirika yasiyo ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali iendelee na udhibiti wa eneo la *Transit Trade,* hasa katika biashara ya mafuta, elimu kwa walipa kodi, tatizo la barabara/njia za panya, usajili wa magari na leseni za madereva, pamoja na mikakati ya kupunguza gharama za biashara na uwekezaji nchini (*cost of doing business*) ili Serikali ikusanye kodi nyingi. Hili ni muhimu hasa ikizingatiwa kuwa, hivi sasa pengo linalohitajika kuzibwa na kodi katika Pato la Taifa (*tax gap*) ni asilimia 4.9. Pengo hili, linatakiwa kuzibwa lifikie asilimia moja tu. Gharama za ukusanyaji mapato kodi hivi sasa ni asilimia 3.2 na lengo ni kufikia asilimia 2.5 na hatimaye kupunguza gharama hizi kwa kiwango kikubwa. Maeneo yote haya ni changamoto kwa Serikali katika kutafuta ufumbuzi wa kuongeza mapato yanayokusanywa kutoka vyanzo vya kodi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeshtushwa baada ya kupata taarifa kutoka *TRA* kuwa, kwa muda mrefu yapo makampuni makubwa nchini ambayo licha ya kupata faida kubwa, hayajalipa na wala hayalipi kodi. Makampuni haya ingawa yanatoa huduma zake kwa kutoza kodi watumiaji/wananchi, hazilipi kodi Serikalini. Kamati imeshauri Serikali, ikiwa utaratibu huu upo ni vyema makampuni husika yalipe kodi inayojiri kulipwa Serikalini. Hili ni eneo ambalo litaongeza mapato ya Serikali na kusimamia kugharimia maendeleo ya nchi.

Aidha, Kamati vilevile imeishauri Serikali, yale maeneo ambayo hayakuleta na hayaleti tija katika ukusanyaji wa mapato au yale maeneo yaliyojidhihirisha kuwa yameongeza tu gharama za ukusanyaji mapato ya kodi kwa Serikali, kwa mfano, ada za mwaka za leseni za magari na usajili, zingefutwa au zingepunguzwa kwa kiwango kikubwa ili ziweze kuvutia watoaji wengi wa ada kwa kutumia dhana ya *economies of scale.* Kamati pia inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri, kwa kufanya marekebisho mbalimbali katika kodi za magari kwa kupunguza viwango vya ada ya mwaka ya leseni za magari, lakini ingeweza kuendelea zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imebaini kuwa, upo upotevu mkubwa wa mapato kutokana na mfumo wetu wa *D by D*. Mfumo ni mzuri lakini ipo haja ya kuimarisha ufuatiliaji na udhibiti. Karibu asilimia 70 ya Bajeti ya Maendeleo na *OC* inaelekezwa kwenye Halmashauri za Wilaya. Utafiti unaonyesha kuwa, matumizi ya fedha hizi umefunguliwa akaunti lukuki kwenye Halmashauri husika. Zipo Halmashauri nyingine zina akaunti katika mabenki zaidi ya 800. Udhibiti wa akaunti hizi hautakuwa na tija. Hali hii inatoa mwanya mkubwa wa upotevu wa fedha za Taifa, pamoja na mapato ya Serikali. Serikali ichukue hatua za haraka za kupunguza kabisa wingi wa akaunti hizi ili kuziba tundu kubwa la upotevu wa fedha wanazozitafuta na hatimaye kwenda kwa walengwa husika. Aidha, Kamati inaambiwa Serikali Kuu nayo ina akaunti zaidi ya 36,000 katika mabenki mbalimbali yaliyopo nchini. Hizi ni akaunti nyingi sana. Kamati inapendekeza utaratibu huu ubadilishwe haraka, kwani upitishaji wa fedha kupitia akaunti zote hizi una athari kubwa zifuatazo.

Kwanza, kwa vile fedha hizi zinapitishiwa katika mabenki, inawezekana mabenki yakacheleweshe fedha hizi kwenda kwa walengwa na hivyo kutumika katika kuongeza ukwasi katika Benki husika. Pili, kuchelewa kwa fedha hizi kufika kwa walengwa kunacheleweshe utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa walengwa, hususan ile inayodhaminiwa kupunguza umaskini. Eneo hili liangaliwe na Serikali kwa makini sana. *TRA* kama chombo chenye jukumu la kutafuta mapato, inayo jukumu la kufuatilia hili, ili kazi zinazofanywa zilingane na fedha zinazotolewa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali kuelewa kuwa, utaratibu wa sasa wa *D by D* unaishia Makao Makuu ya Halmashauri, kwa maana ya ngazi ya Wilaya. Bado ngazi za Kata na Vijiji, hazijaeleweka vyema na utaratibu huu na hivyo kuondoa kabisa dhana ya mipango shirikishi ya miradi na matumizi ya fedha. Tatizo hili linajenga hisia za matumizi mabaya ya fedha za Serikali, pamoja na kuondoa dhana nzima ya uwajibikaji. Wizara ya Fedha, iangalie utaratibu wa kujenga uwezo wa Halmashauri wa kuhusisha Kata na Vijiji katika kutoa maamuzi ya fedha zinazotolewa ama sivyo, hili ni tundu lingine la kuvujisha mapato na fedha za Serikali. Uimarishaji uwezo wa Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala na Wilaya, Wenyeviti wa Halmashauri za Wilaya na Mameya katika kusimamia utekelezaji wa bajeti kuimarisha utawala bora, uwajibikaji na usimamizi wa fedha za umma katika mamlaka zao, uliotamkwa na Serikali ufanyike kwa vitendo. Serikali inatarajia kupunguza kiwango cha utegemezi kutoka asilimia 42 hadi 34. Hili ni changamoto kubwa. Aidha, Serikali pia imedhamiria kugharimia *OC* kwa asilimia 100. Matumizi yasiyodhibitiwa, ufikiaji wa malengo haya utakuwa ni mgumu.

Maeneo mengine hususan yale yanayohusu *employment allowances,* katika kasma na gharama za uendeshaji wa Serikali, ambayo katika kipindi kijacho zimetengewa Sh.608 bilioni ni baadhi tu ya maeneo yanayohitaji ufuatiliaji wa karibu. Utaratibu wa manunuzi ya vifaa na huduma mbalimbali, unapaswa pia uangaliwe vyema ili kuhakikisha kuwa, fedha zinazopangwa na Serikali zinatumika vizuri na matumizi yake yalingane na matokeo ya thamani ya fedha iliyotumika (*value for money).*

Mheshimiwa Spika**,** eneo lingine litakaloweza kuleta ahueni kama chanzo cha mapato ni lile la *export trade* na maeneo au nchi za jirani. Hili ni changamoto kwa Wizara ya Viwanda na Biashara. Serikali inashauriwa ifuatilie kwa karibu eneo hili, pamoja na kuwa na *regulatory control* hasa kwenye kodi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipoangalia misingi ya uendeshaji uchumi katika kipindi kijacho, hususan baada ya kupitia eneo la majumuisho ya Taarifa ya Hali ya Uchumi ya Mwaka 2007 na Maendeleo ya muda wa kati (2008 - 2010/2011), changamoto zilizoorodheshwa zinahitaji zifanyiwe kazi kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Spika, hakuna nchi duniani inayoweza kuendelea bila ya msukumo mkubwa katika uwekezaji (*Investment Drive*). Hata hivyo, uwekezaji ili ushamiri, unahitaji kujengewa mazingira mazuri. Upo umuhimu mkubwa wa kupunguza gharama za uzalishaji na biashara (*reducing cost of doing business*). Riba kubwa ya mikopo katika uchumi, inaadhibu wawekezaji. Urasimu ni adui mkubwa wa uwekezaji. Ucheleweshaji wa kutoa maamuzi *(delays in decison making process*) ni kero kwa wawekezaji. Urasimu ni adui mkubwa wa uwekezaji. Nyingi ya sheria zetu,

zinakwamisha ari ya uwekezaji nchini, pamoja na kuwa kero. Kwa mfano, utaratibu ambao mwekezaji mkubwa wa kilimo anapaswa aufuate hadi apate eneo la kulima kibiashara, hautoi motisha wala uhamasishaji wa kuwekeza. Ugumu wa kubadili fikra zetu na mtazamo wetu (*change of attitude and right mindset),* kwa baadhi ya watendaji, umekwamisha juhudi nyingi za kujenga uchumi wetu kupitia uwekezaji wa ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, katika karne hii tuliyonayo, Serikali haina budi kumaliza haraka matatizo yaliyotajwa hapo juu ili kuwezesha uchumi kufanya kazi. Kamati ina wasiwasi na misingi ya uchumi iliyoorodheshwa, inaweza kutofikia malengo kutokana na matatizo yaliyotajwa hapo juu. Upo umuhimu wa kuchukua hatua za haraka, pamoja na zile za kuhuisha baadhi ya Sheria kama ilivyofanyika kwa Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348 au Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika uchumi unaenda na muda na muda ni mali. Kikao cha Kimataifa cha Sullivan, kilichofanyika Arusha, hakitakuwa na tija kama mazingira ya uwekezaji hayataendelea kuboreshwa. Ni vyema Serikali ikaendeleza na kuzidisha kasi ya mabadiliko, fikra na tabia katika maeneo yatakayokuza uchumi wa nchi. Haitoshi kusema Tanzania sasa tupo nafasi ya 130 duniani kutoka nafasi ya 170; suala ni kuwa Kenya na Uganda, jirani zetu wapo katika nafasi ya ngapi. Ipo haja ya Serikali vilevile kuifanyia tathmini Programu ya MKUMBITA ili tuone tumefikia wapi. Masuala ya utawala bora vilevile yazingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la miundombinu ni eneo lingine ambalo Kamati imelijadili kwa kina. Katika kipindi cha Bunge lililopita, tulipitisha Muswada unaohusisha uendeshaji bora wa huduma za nishati ikiwemo umeme. Gharama za uzalishaji zinazotokana na umeme ni karibu asilimia 40 hadi 50; eneo hili liangaliwe. Kamati inaishauri Serikali, ijikite katika mkakati wa hatua za kupunguza gharama za nishati ya umeme *(energy cost reduction measures). Capacity charges* zihuishwe ili kuepuka *abnormal profits* kwa watoaji umeme binafsi, *PPA* zihuishwe, viwango vya bei za umeme viangaliwe upya *(restructuring of tariff rates)* ili vyombo vya uzalishaji vipunguziwe gharama za uzalishaji ili viweze kuzalisha maradufu. *Tariffs* za wateja wa kawaida, pamoja na gharama za kuunganisha umeme, ziteremshwe ili kufaidika na *economies of scale.* EWURA kama mdhibiti, isiegemee tu kwenye mapato yatokanayo, ila nayo iwe ni chombo cha kusaidia kutoa ushauri wa jinsi ya kupunguza bei za nishati, hususan ya umeme. *EWURA* kama *regulator,* ijiepushe kuwa kama Polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza umuhimu wa kuchukua hatua za haraka za kuboresha utendaji kazi wa Bandari zetu, yaani za Tanga, Dar es Salaam na Mtwara. Aidha, Bandari zetu za Mwanza na Kigoma, zina uwezo wa kuleta sura mpya ya uchumi wetu kwa muda mfupi sana. Suala zima la *Economic Management* likizingatiwa, litatoa kipaumbele muhimu kwa maeneo haya ambayo *impact* yake haitachukua muda mrefu. Inawezekana kabisa, kuzorota kwa hatua muhimu kuchukuliwa kunatokana na tatizo la maamuzi; Kamati inaikumbusha Serikali kuwa, wakati rasilimali zikiwa chache ni mantiki zikielekezwa kwenye yale maeneo ambayo yanaweza kuibua uchumi kwa muda mfupi *(economic happeners).* Usambazaji wa rasilimali chache katika maeneo mengi, matokeo yake ni udhaifu katika kutekeleza malengo yanayopimwa kwa ubora wake. Suala la uendelezaji wa reli ya Kati na ile ya Tanga, pamoja na Mikoa ya Kaskazini,

lisichukuliwe kama fursa iliyopotea ili kuhamasisha uwekezaji wa ziada nchini na kutumia nafasi za kuhudumia nchi jirani kiusafiri na hivyo kuongeza utajiri wa nchi. Kamati inaiuliza Serikali; ikiwa Bandari yetu ya Dar es Salaam ina tatizo kubwa la msongamano mkubwa wa mizigo, lipo tatizo gani la kuanzisha *Dry Port* katika eneo la Ruvu ili kuongeza tija, ufanisi na mapato kwa Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, deni la Taifa; katika eneo hili ambapo deni la ndani ni takriban dola milioni 1,673.5 au asilimia 23.8 ya deni lote, Serikali ijitahidi kupunguza madeni, hususan yale yanayoandamana na utoaji huduma katika mashule yetu ya sekondari, taasisi za elimu ya juu, pamoja na vyuo vikuu. Huduma hizi ni pamoja na zile zinazojumuisha zabuni za chakula na gharama za umeme. Hali hii itasidia kuondoa kero ya kuharibu ratiba za taasisi hizo kutokana na ukosefu wa huduma hizi muhimu.

Mheshimiwa Spika**,** pamoja na maendeleo mazuri tuliyoyapata katika kuendeleza Sekta ya Huduma za Jamii, Kamati imeikumbusha Serikali kuwa uwingi peke yake si hoja, bali ni vyema vilevile ikaangalia ubora *(quantity visa vis quality*). Pamoja na mashule mengi yanayoendelea kujengwa ni lazima uwepo uwiano wa kuwapata walimu, pamoja na maabara. Vifaa kama nyenzo ya kuendeleza elimu ni muhimu. Mkakati wa kuboresha sekta ya afya ni vyema ukaendana na upatikanaji wa matabibu, waganga na madaktari, pamoja na dawa na zana. Mingi ya miradi ya maji, Kamati imebaini haikutekelezwa kwa tija.

Miradi mingi ya kiwilaya iliyoandaliwa chini ya Programu ya *Quick Wins,* pamoja na ile inayofadhiliwa na Benki ya Dunia, haikufanikiwa vizuri. Hili ni eneo ambalo Kamati imependekeza liangaliwe kwa umakini mkubwa ili Taifa, lisiendelee kubeba mzigo mkubwa wa fedha za madeni, ambazo hazikutoa matunda yaliyotegemewa. Serikali ihuishe utaratibu wa zabuni za makandarasi wanaojitokeza kujenga miradi ya maji. Aidha, eneo hili pia linajumuisha udhaifu unaojitokeza wa utekelezaji mbaya wa makandarasi wengi wanaojiingiza katika ujenzi wa barabara vijijini. Serikali inapoteza fedha nyingi sana katika eneo hili. Maeneo yote haya yanahitaji uimarishaji wa *performance* na hata *forensic audit* ili kujua fedha za Serikali zinatumika kwa tija na ufanisi au la.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ina imani kubwa kuwa maoni ya ziada iliyoyatoa kwa Serikali yatazingatiwa ili kuboresha usimamizi wa uchumi wetu na matumizi ya Serikali hasa kwenye eneo la udhibiti. Pamoja na vipaumbele tulivyojiwekea, Kamati inaishauri Serikali kuangalia kwa karibu kabisa, hatua za kubuni vivutio zaidi kwa sekta ya kilimo ili ichangie kwa viwango vikubwa katika Pato la Taifa na katika kujenga uchumi wetu. Hii itakuwa ni hatua ya kihistoria kwa uendeshaji wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumalizia kwa kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati, kwa kazi nzuri waliyoifanya na ushirikiano wao walionipa. Naomba nitumie fursa hii kuwatambua wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mwenyekiti, Mheshimiwa Hamza Abdallah Mwenegoha, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Elizabeth Nkunda Batenga,

Mheshimiwa Anthony Mwandu Diallo, Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mheshimiwa Athumani Said Janguo, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Eustace Osler Katagira, Mheshimiwa Anna Maulidah Komu, Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba, Mheshimiwa Dr. Binilith Satano Mahenge, Mheshimiwa Monica Ngezi Mbega, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Felix Christopher Mrema, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Damas Pachal Nakei, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mheshimiwa Dr. Omar Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mheshimiwa Suleiman Ahmed Saddiq, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir, Mheshimiwa Devotha Mkuwa Likokola na Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii, kumshukuru Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Makamu Mwenyekiti, kwa kunisaidia kuiongoza Kamati; Mheshimiwa Mustafa Mkullo, Waziri wa Fedha na Uchumi; Mheshimiwa Jeremiah Solomon Sumari na Mheshimiwa Omar Yussuf Mzee; Naibu Mawaziri wa Wizara ya Fedha na Uchumi. Aidha, naomba niwashukuru Watendaji Wakuu wa Wizara, Mashirika, Taasisi na Asasi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi, kwa ushirikiano na mshikamano walioonyesha kwa Kamati wakati wa kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana wewe mwenyewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutupatia miongozo na maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu, ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati zote. Dhana yako ya Kasi na Viwango, inajichimbia vyema kwenye kamati. Aidha, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Kaimu Katibu wa Bunge, Dr. Thomas D. Kashililah, Makatibu wa Kamati; Ndugu Anselm Mrema na Ndugu Michael Chikokoto, kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda.

Ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge; sasa ni zamu ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ambaye si mwingine ni Mheshimiwa Dr. Hamad Rashid Mohamed. Nimemwongezea cheo leo.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED (MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI):** Dua nzuri Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Ahsante.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED (MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba upokee shukrani zetu za dhati, kwa kunipa nafasi hii ili

nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Hotuba ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2008/2009, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, kifungu cha 99(7), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kutoa shukrani zangu za dhati, kwa Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani, kwa ushirikiano wao mkubwa walionipa, wakiongozwa na Mheshimiwa Dr.Wilbrod P. Slaa hadi kuniwezesha kusimama mbele yenu, kuwasilisha hotuba ya maoni ya Kambi ya Upinzani, kutokana na hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha na Uchumi, tarehe 12. Juni, 2008.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wa Upinzani na Wabunge wote kwa ujumla wao, kwa pamoja tuna wajibu wa kushirikiana katika kuwatumikia Watanzania, kwa lengo kuu la kuwaondolea umaskini uliokithiri, maradhi na ujinga, pamoja na kujenga UTAIFA wetu wa dhati. Mwenyezi Mungu, aziweke pamoja nia zetu na kuzibariki katika kuwatekelezea Watanzania azma hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Serikali ni zaidi ya urari wa mapato na matumizi ya Serikali. Bajeti ni tamko la kisera, lenye lengo mahususi katika kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi, kuongeza ajira na kupunguza umaskini miongoni mwa wananchi. Kambi ya Upinzani Bungeni, chini ya uongozi wangu na msaidizi wangu, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mbunge wa Karatu, ambaye naomba kumpongeza kwa kuishinda tena CCM katika kesi ya Uchaguzi; inaundwa na vyama vya CUF, CHADEMA na *UDP*. *(Makofi)*

Naomba kutumia fursa hii, kuvishukuru vyama vyetu kwa kuweza kujenga maelewano ambayo sio tu kusaidia juhudi za Kambi yetu kutoa maoni ya pamoja juu ya Hotuba ya Mipango na Bajeti ya Waziri wa Fedha, bali kuisaidia Serikali katika muono wa pili wa shilingi. Aidha, Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru wapiga kura wa Jimbo langu la Wawi, kwa kuendelea kuniunga mkono katika kazi walizonikabidhi katika kipindi cha 2005 - 2010. Nawaahidi, kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, nitaendelea kuwatumikia kwa uadilifu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 14 Juni, 2006, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alifanya mazungumzo na Wabunge wa CCM na hatimaye Wabunge wa Kambi ya Upinzani. Katika kikao hicho, pamoja na mambo mengine mengi, Rais aliendelea kutoa ahadi yake ya kuumaliza mpasuko wa kisiasa ulioko Zanzibar na kusema: “Tumeshaanza, siyo rahisi sana lakini tutaumaliza.” *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani itaendelea kuunga mkono juhudi za Rais katika kuutafutia ufumbuzi mpasuko wa kisiasa wa Zanzibar, pamoja na kero za Muungano (ambazo Rais Mstaafu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa), aliahidi kuzimaliza katika kipindi cha miezi sita wakati alipoingia madarakani), lakini bahati mbaya hakufanikiwa. Kambi ya Upinzani ingelipenda kuweka bayana kwamba, imani ya Watanzania inaendelea kupungua siku hadi siku, kutokana na kuchelewa kufikiwa kwa Muafaka baina ya CCM na *CUF*. Ni imani yetu kuwa, ahadi aliyotoa hivi karibuni alipokuwa Uingereza, Rais atatumia busara zake, kukamilisha mazungumzo ili nchi yetu iepukane na aibu inayoitwa ya *Ngariba wa Kilwa;* anatahiri watu lakini mwenyewe hakutahiriwa. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kukushukuru wewe, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge na Watendaji wa Ofisi yako, wakiongozwa na Kaimu Katibu wa Bunge, kwa kutupatia fursa mbalimbali Wabunge kujifunza shughuli za Mabunge ya wenzetu. Moja tulilojifunza katika Mabunge mengi, Kambi ya Upinzani huwa inapata fursa ya kutoa bajeti mbadala, kuonyesha upande wa pili wa shilingi. Nia yetu sote ni kumsaidia Mtanzania, aondokane na umasikini wa kila aina.

Mheshimiwa Spika, naomba kumpongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa Mkullo, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Manaibu wake, pamoja na Wakuu wa Vitengo na Asasi zilizo chini yao, kwa kazi nzito ya maandalizi ya Bajeti hii. Kambi ya Upinzani, inafanya uchambuzi wake ikiamini kuwa, Waziri atakuja kutoa ufafanuzi zaidi katika baadhi ya maeneo kwa kadiri tutakavyoainisha. Uchambuzi wetu nitauelezea baadae kwa kifupi na kwa kirefu utaelezwa na Mawaziri Vivuli wa Wizara mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii fupi, kuwakumbusha tena Watanzania kupitia Bunge lako Tukufu kuwa, toka nchi yetu ipate Uhuru (Tanganyika) 1961, kukawa na *Republic of Tanganyika* na baada ya Mapinduzi (Zanzibar) 1964, kukawa na *People's Republic of Zanzibar* na hatimaye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nchi yetu imeongozwa na *TANU* na *ASP* na Hatimaye CCM. Hivyo ni dhahiri kuwa, mafanikio na upungufu wote wa maendeleo ya nchi yetu vimetokana na Uongozi na Sera za CCM.

Mheshimiwa Spika ni wajibu wetu sote kujiuliza; katika kipindi hiki chote cha uongozi wa aina moja; je, sera zilizokuwepo, Mtanzania wa kawaida maisha yake yameboreka; kwamba, sasa anaweza akapata angalau milo miwili bila ya wasi wasi? Je, mwananchi wa kawaida anaweza akasomesha watoto wake na watoto hao wakasoma vizuri na hatimaye wakapata ajira au anaweza kujiajiri kwa kupata mikopo kwa urahisi yenye riba nafuu; na je, anaweza kupata huduma ya kijamii bila ya kulipia kwa gharama kubwa na kama anaweza kupata bei muafaka ya mazao yake kwa kuuza anakotaka kama ilivyokuwa kabla ya Uhuru na Mapinduzi? Je, hata anayefanya kazi amepata mshahara unaokidhi mahitaji yake?

Mheshimiwa Spika, tunapokumbushana haya, hatusemi kwamba, Tanzania hakuna maendeleo au mabadiliko, lakini je, maendeleo hayo ni endelevu kiasi cha kumhakikishia Mtanzania kwamba baada ya "Sera ya Kilimo ni Uhai" ya Mwaka 1976; tunajitosheleza kwa chakula cha kutosha na hata ukame ukitokea tuna chakula cha akiba au chakula kinapokuwa bidhaa adimu duniani tunaweza kuuza na kubakiwa na akiba; au bado tunaendelea kuhemea chakula? Kwamba tuliwahi kuwa na hekta 450,000 za umwagiliaji sasa zipo 298,888 tu, hayo ni maendeleo endelevu?

Kwamba Mwalimu alituambia "kupanga ni kuchagua" Je, kununua ndege kwa pesa taslimu Sh. 42 *billion,* inayoweza kutua katika viwanja visivyozidi vitano katika nchi nzima na hata kushindwa kutua Dodoma ambayo ni Makao Makuu ya nchi na ya Bunge; ndege inayotumia wastani wa Sh. 6 *million* kwa saa ya kuruka na kuwa na ndege nyingine mbili ambazo hata bajeti ya mwaka huu zimeshindwa kutengewa fedha za

matengenezo na kuacha kuwatengenezea barabara wanachi wa Mikoa ya Kusini, ambao ni wazalishaji wakubwa wa Korosho, Muhogo, Ufuta na rasilimali za misitu na au kuacha kujenga zahanati, shule japokuwa wananchi wanafanya kazi hiyo ya kujenga na msaada wa Serikali ni kama tone kwenye bahari; hivyo, fedha hizo si zingesaidia kuwanufaisha wananchi walio wengi bila ya wao kujitolea?

Kwamba unaweza kutumia rasilimali nyingi za nchi, kusafiri kutafuta wawekezaji bila ya kuwa na mipango ya kuwarasimisha wananchi, hivyo kuwafanya wawe omba omba au ndio ule msemo wa kiswahili kwamba "Punda afe lakini mzigo wa bwana ufike." Kwamba huku unataka kumwondolea umaskini, upande wa pili unamwongezea kodi kwa mlango wa nyuma, bei za mafuta ya petroli na dizeli, bei za mafuta ya taa ni 1,182.22 kwa lita huku petrol ikiwa 934.97 na dizeli 1,027.40 na hali ya bei hizo kwa hapa nyumbani ni tofauti haswa ukizingatia ya kuwa kodi na tozo mbalimbali kwa lita, yaani shilingi 59.10 mafuta ya taa, 545.1 petrol na 520.80 dizeli.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona kwamba, katika kuonyesha umakini wa kuinua uchumi wetu, hizo kodi za ndani zinazotozwa kwenye mafuta, tunatoa punguzo la shilingi 250.00 kwa lita moja ili kukabiliana na bei ya soko la dunia. Hii ndio njia pekee ya kuufanya uchumi wetu ukue.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Taifa ni chombo pekee muhimu cha kutafsiri na kutekeleza Sera za Chama Tawala na Serikali kwa vitendo. Katika Bajeti ya Serikali; Serikali inapata fursa ya kupanga matumizi ya fedha kidogo zilizopo katika maeneo na sekta zinazohitajika kupewa kipaumbele ili malengo makuu ya Serikali yatekelezwe. Aidha, Rais Mstaafu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa katika hotuba zake za kila mwezi alisema: "Bajeti ni kipimajoto cha uhai wa mtu na afya ya uchumi wa Taifa; Daktari mzuri wa uchumi ataitumia bajeti kutoa tiba ya kupambana na umaskini na kuongeza kasi ya kukua kwa uchumi."

Katika nchi maskini kama Tanzania, malengo ya Sera za Serikali yanapaswa kuwa ya kujenga mazingira mazuri ya kukuza uchumi na kuongeza ajira ili kupunguza na kutokomeza umaskini. Katika kuendeleza uchumi, matumizi ya Serikali yanapaswa kuwa na malengo matatu makubwa:-

(a) Matumizi ya Serikali, yalingane na uwezo wa mapato ya Serikali. Matumizi ya Serikali, yawe endelevu, pasiwe na nakisi kubwa ya bajeti inayojazwa kwa kuchapisha fedha, kukopa ndani au kukopa nje. Bajeti ya Serikali, lazima ilenge katika kupunguza kutegemea misaada na mikopo.

(b) Bajeti ya Serikali igawanywe katika sekta mbalimbali, kwa lengo la kuongeza ufanisi na kutoa kipaumbele katika maeneo yanayokuwa chachu katika kukuza uchumi, kuongeza ajira na kupunguza umaskini.

(c) Matumizi ya fedha za Serikali katika sekta zilizopewa fedha hizo, yaendeshwe kwa ufanisi na kwa kuongeza tija. Darasa linalogharimu shilingi milioni moja, lisijengwe kwa gharama kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM, Mipango na Ubinafsishaji ilipanga mkakati wa kutekeleza Sera za Uchumi kama ifuatavyo:-

(a) Kuona kuwa uchumi unakua kwa viwango na kasi kubwa ukilinganisha na mwaka uliopita.

(b) Mikakati ya kupunguza umaskini hasa usio wa kipato.

(c) Kuratibu mipango Kitaifa, uwekezaji na ubinafsishaji.

Mheshimiwa Spika, je, misingi hii imeheshimiwa na Serikali? Sote ni mashahidi wa wafanyakazi wetu waliolitumikia Taifa hili kwa maagizo na miongozo ya Serikali yao, wanavyosumbuka na kutaabishwa katika kudai haki zao zilizotokana na ahadi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya CCM kudai kuwa, katika kuendeleza, kuufufua na kuujenga uchumi wa Taifa, Serikali ya CCM itaongozwa na Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, inayolingana na wakati tulionao. Shabaha ya Ujamaa katika kipindi hiki ni kuwafanya wananchi wenyewe, kuwa ndio wamilikaji wakuu wa uchumi wa dola, kuwa zaidi mhimili wa uchumi wa Taifa. Je? Ubinafsishaji umewafanya Wananchi wa Tanzania kuwa wamilikaji wakuu wa uchumi? Je, rasilimali za nchi zimerasimishwa kwa Wananchi wa Tanzania, haya ni maswali ya kujiuliza wakati tunaangalia Sera za CCM.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya mwaka 2008/2009 ni Bajeti ya tatu ya Serikali ya Awamu ya Nne. Lengo letu kama Kambi ya Upinzani ni kupitia utekelezaji wa Bajeti ya mwaka unaokwisha, kwa shabaha ya kuonyesha mafanikio na upungufu na kisha kupendekeza njia muafaka ya kuwa na Bajeti bora, itakayoleta unafuu wa maisha kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, ili kutathmini maendeleo ya uchumi, tunahitaji tuwe na takwimu sahihi za Pato la Taifa. Ni jambo la kawaida, kufanya marekebisho katika takwimu za Pato la Taifa, kwa madhumuni ya kuziboresha. Kwa kawaida, marekebisho hayo huwa hayabadilishi muundo halisi wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, vigezo vingi vya kupima mafanikio ya uchumi kama ukuaji wa uchumi, ukusanyaji wa mapato ya Serikali, ubora wa mfumo wa fedha *(financial deepening),* pato la wastani la mwananchi na kadhalika, vinatumia takwimu za Pato la Taifa. Takwimu mpya za Pato la Taifa, zimeonyesha kuongezeka kwa ukubwa wa pato hilo katika miaka ya 1998 – 2006, kwa wastani wa asilimia 21.3. Ghafla Watanzania wanaelezwa kwamba, Pato la Taifa halisi lilikua kwa wastani wa asilimia 7.2 kati ya mwaka 2002 – 2006 na siyo asilimia 6.3 kama takwimu za zamani zilivyoonyesha.

Mheshimiwa Spika, takwimu mpya zinaonyesha kwamba, ukame na ukosefu wa umeme wa mwaka 2006, uliotuletea kadhia ya ufisadi wa Richmond, eti haukuathiri uchumi wa Tanzania, kwani uchumi uliendelea kukua kwa asilimia 6.7. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, marekebisho yaliyofanywa hivi karibuni, yanatia mashaka makubwa, kwani yamebadilisha kabisa muundo wa uchumi. Takwimu za zamani zinaonyesha kuwa, katika mwaka 2005, Sekta ya Kilimo ilichangia Pato la Taifa kwa asilimia 46.1. Takwimu mpya zinaonyesha katika mwaka huo huo wa 2005, Sekta ya Kilimo imechangia asilimia 29 tu. Mchango wa Kilimo umepungua kwa asilimia 17.1. Ikiwa takwimu mpya za Pato la Taifa ni sahihi, basi mipango yote ya Serikali ya kukuza uchumi kwa ujumla na kisekta, haina maana kwani imejikita katika takwimu ambazo hazielezi hali halisi ya uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri ameeleza kuwa, takwimu za Pato la Taifa za sasa zimezingatia taarifa mpya kama zile zilizotolewa na utafiti wa bajeti ya kaya *(Household Budget Survey*) ya mwaka 2000/01. Tathmini hii ya mapato na matumizi ya kaya, inaonyesha kuwa asilimia 84.2 ya nguvu kazi ya Tanzania, inaajiriwa katika Sekta ya Kilimo. Kwa takwimu za zamani, nguvu kazi hii ilichangia asilimia 44.7 ya Pato la Taifa. Kwa takwimu mpya kilimo na uvuvi, vimechangia asilimia 30.7 tu mwaka 2001. Ikiwa mchango wa Sekta ya Kilimo ni mdogo kiasi hicho, wakati asilimia 84.2 ya nguvu kazi ya Tanzania iliajiriwa katika kilimo mwaka 2001 ni dhahiri kuwa, umaskini umeongezeka sana na hasa vijijini. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali ikiri kuwa umaskini vijijini ni wa kutisha zaidi kuliko ilivyokadiriwa mwaka 2001. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mtanzania wa kawaida haamini kuwa uchumi unakua kwa sababu haoni matunda ya kukua uchumi. Waheshimiwa Wabunge, ambao ndio wawakilishi wa wananchi na wapo karibu nao, wanapata shida kupata picha halisi ya ukuaji huu, kwa sababu maisha ya Mtanzania wa kawaida, yameendelea kuwa duni siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika, Ripoti ya Umaskini na Maendeleo ya Watu ya 2007 imebaini kuwa, Watanzania wengi wanaona kuwa maisha yao yanazidi kuporomoka siku hadi siku. Wananchi wengi hawaamini kuwa, uchumi unakua na maisha ya mwananchi wa kawaida yanaboreka. Wananchi wengi wanaamini kuwa, misaada ya nje inawanufaisha wakubwa na vigogo wa Serikali na wananchi wa kawaida wanaambulia patupu.

Mheshimiwa Spika, wananchi vijijni wanalalamika kuhusu hali mbaya ya barabara, ukosefu wa maji safi na salama na gharama kubwa za huduma za afya. Ahadi ya Serikali kuwa watoto na wazee wa miaka 60 na zaidi, watapata huduma za afya bure katika Zahanati na Hospitali za Serikali haitekelezwi na wala haitekelezeki, kutokana na ukosefu wa mipango na miongozo madhubuti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna udhaifu mkubwa katika ukusanyaji wa takwimu za Pato la Taifa. Katika Jumuia ya Kimataifa, Tanzania ni maarufu kwa kutokuwa na takwimu za uhakika *(World Development Indicators 2007).* Wafanyakazi na Wataalam katika Taasisi ya Taifa ya Takwimu, wana motisha zaidi wa kukusanya takwimu za miradi

maalum, inayofadhiliwa toka nje kama vile tathmini ya bajeti za kaya, kwa sababu ina posho na marupurupu mengi.

Mheshimiwa Spika, shughuli za kila siku kama vile kuandaa Takwimu za Pato la Taifa, hazipewi kipaumbele kwani hazina posho na magari ya mradi. Mipango yetu ya kukuza uchumi ni dhaifu, kwa kutokuwa na takwimu sahihi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inapendekeza kuundwa Jopo la Wataalam wa ndani na nje, kutathmini usahihi wa takwimu mpya za Pato la Taifa na kupendekeza taratibu za kuboresha ukusanyaji wa takwimu hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, tathmini ya Kambi ya Upinzani kwa ufupi juu ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2007/2008 na baadaye nieleze misingi na shabaha ambayo kama Serikali ingalizingatia Mapato na Matumizi ya Serikali ya mwaka 2008/2009, yangaliboreka zaidi.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha na Uchumi, amelieleza Bunge lako Tukufu kuwa na ninanukuu: "Kwa ujumla, bajeti ya mwaka 2007/08, imetekelezwa kwa msingi wa sera mbalimbali zilizotangazwa wakati wa kuwasilisha bajeti hiyo Bungeni mwezi Juni, 2007. Mapato ya kodi yanakusanywa kama yalivyolengwa na matarajio ni kwamba, tutafikia malengo ya makusanyo ya mwaka mzima wa 2007/08 bila wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya Serikali yanaendelea kulingana na bajeti na inatarajiwa kwamba, bajeti ya 2007/08 itakuwa imetekelezwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Waziri pia aliwasilisha Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa katika mwaka 2007. Nawaomba Wabunge, watazame Jedwali Namba 26 katika kurasa za 75 na 76, linaloonyesha mgawanyo wa matumizi yote ya Serikali katika huduma na sekta mbalimbali. Jedwali hili ndiyo taarifa pekee inayotolewa na Serikali kuhusu mgawanyo wa matumizi halisi.

Mheshimiwa Spika, Waziri ameeleza kuwa, maeneo makuu ya kipaumbele katika matumizi ya Serikali ni Elimu, Afya, Kilimo, Miundombinu, Maji na Nishati. Sekta zote hizo zimetengewa fedha nyingi zaidi katika mwaka 2008/09, ukilinganisha na mwaka 2007/08, isipokuwa Sekta ya Maji.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ongezeko la bajeti ya sekta hizi ni ya maneno tu, kwani matumizi haya hayatekelezwi kwa vitendo. Katika mwaka 2007/08, Sekta ya Elimu ilitengewa shilingi trilioni 1.086.0, miundombinu ya barabara ilitengewa shilingi bilioni 777.2, Sekta ya Afya ilitengewa shilingi bilioni 589.9, Sekta ya Kilimo ilitengewa shilingi bilioni 379.0 na Sekta ya Maji ilitengewa shilingi bilioni 354.0.

Mheshimiwa Spika, matumizi halisi ya sekta hizi katika mwaka 2007/08, kama yalivyochambuliwa katika Hali ya Uchumi wa Taifa, Jedwali Na. 26, Elimu imetumia Shilingi bilioni 552.7, sawa na asilimia 51 tu ya fedha zilizotengwa. Sekta ya Ujenzi imetumia Shillingi bilioni 596.3, ikilinganishwa na shilingi bilioni 777.2 zilizotengwa

kwa Sekta ya Miundombinu ya Barabara pekee, sawa na asilimia 76.7. Sekta ya Afya imetumia shilingi bilioni 373.9, ikilinganishwa na shilingi bilioni 589.9 zilizotengwa, sawa na asilimia 63.4. Sekta ya Kilimo imetumia shilingi bilioni 151.4, ikilinganishwa na shilingi bilioni 379 zilizotengwa, sawa na asilimia 39.9. Sekta ya Maji imetumia shilingi bilioni 208.3, ikilinganishwa na shilingi bilioni 309.1 zilizotengwa, sawa na asilimia 67.4.

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu za Hali ya Uchumi wa Taifa; mwaka 2007, Sekta zimekadiriwa kutumia kama ifuatavyo: Elimu asilimia 9.1 badala ya asilimia 18 zilizotengwa katika bajeti; Sekta ya Afya imetumia asilimia 6.2 badala ya asilimia 9.7 na Sekta ya Kilimo asilimia 2.5 badala ya asilimia 6.2 ya bajeti yote ya mwaka 2007/08. Kwa utaratibu huu, pamoja na Bunge lako Tukufu kuonekana linasimamia kidete matumizi ya Serikali, lakini bado Serikali inatumia fedha za wananchi maskini wa Tanzania bila umakini. Serikali imeandaa makadirio ya bajeti na Bunge likayapitisha kama ilivyotakiwa, lakini haiheshimu bajeti yake yenyewe. Sekta zilizopewa kipaumbele, zinatumia nusu mpaka theluthi mbili tu ya fedha zilizotengwa katika bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa Serikali wa kutumia kulingana na mapato yaliyoko *(cash budget*), unafanya zoezi la kutayarisha bajeti kuwa la mzaha, kwani haiongozi matumizi ya Serikali, matokeo yake shule za sekondari za Serikali za bweni (*boarding*), zinafungwa kwa kukosa chakula, zahanati na hospitali hazina dawa na wakulima hawapati mbolea na huduma za ugani.

Mheshimiwa Spika, tunawadanganya Watanzania kuwaeleza kuwa, tumeongeza Bajeti ya Elimu, Afya, Kilimo na Miundombinu ya barabara ikiwa bajeti haiongozi matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inataka ili kuliwezesha Bunge lako liweze kuisimamia Serikali katika utekelezaji wa bajeti, Waziri wa Fedha na Mipango, atupe taarifa kamili ya makadirio yaliyoidhinishwa na matumizi halisi ya kifungu kwa kifungu ya mwaka wa fedha 2005/06, 2006/07 na 2007/08 ili tuweze kuhakiki kwa kiasi gani matumizi yanayopitishwa na Bunge lako ndiyo yanayoiongoza Serikali katika utendaji wake wa kazi. Kambi ya Upinzani, inataka kupata taarifa ya matumizi kwa kifungu. Hii ni kazi rahisi, kwa kuwa matumizi na mapato ya Serikali, yanatumia teknolojia ya habari na mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2007/08, Serikali ilipanga kutumia jumla ya Sh. 6.066 trillion na 2008/09 Sh.7.216 trillion. Ongezeko la Sh.1.150 trillion. Aidha, Serikali mwaka huu imepanga kupunguza utegemezi kutoka asilimia 42 ya mwaka jana na kuwa asilimia 34, punguzo la asilimia 8. Kambi ya Upinzani mwaka jana ilipendekeza punguzo la kutoka asilimia 42 hadi asilimia 31.8. Kambi ya Upinzani inasisitiza malengo ya kufikia asilimia 31.8, bado yafikiwe kwa uhai wa Taifa letu. Tunaishukuru pia Serikali kwamba, imeona mapendekezo yetu ya mwaka jana yalikuwa ni ya kweli.

Mheshimiwa Spika, Ili tupunguze umaskini vijijini, kilimo kinastahili kikue kwa wastani wa asilimia 6 – 8 kwa mwaka katika kipindi cha mpito. Kilimo chetu bado

kinatumia zana duni na kutegemea mvua. Wakulima wadogo ndio tegemeo la kilimo cha Tanzania, lakini hawajasaidiwa kuboresha kilimo chao. Wakulima wadogo wa China na Vietnam wenye wastani wa mashamba chini ya hekta moja, ndio wanaotegemewa katika Sekta ya Kilimo kwa kuwa wakulima hawa wamejengewa na Serikali mazingira mazuri ya kupata mbolea, mbegu bora, utaalam, miundombinu ya umwagiliaji maji na barabara bora za vijijini zinasaidia kufikia masoko.

Mheshimiwa Spika, pamoja na MKUKUTA kuweka lengo la kukuza Sekta ya Kilimo hadi kufikia asilimia 10 kwa mwaka na Ilani ya Uchaguzi ya CCM kueleza kuwa kilimo kitakuwa kwa asilimia 20, ukuaji wa kilimo kati ya mwaka 2000 – 2006 ulikuwa wastani wa asilimia 4.5. Malengo yaliyomo ndani ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM yalikuwa ni ya kisiasa tu.

Mheshimiwa Spika, hakuna nchi ambayo imefanikiwa kukuza kilimo kwa asilimia 20. Kwa kawaida, kilimo ndicho kinachokuwa kwa kasi ndogo kuliko sekta nyingine kama vile viwanda, mawasiliano na huduma za biashara. Ikiwa Sekta ya Kilimo itakua kwa asilimia 20, Pato la Taifa litakua kwa zaidi ya asilimia 20. Baadhi ya malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ni ya kusadikika, hayawezi kufikiwa na kwa hiyo hayawezi kuongoza uandaaji wa mipango ya uchumi na bajeti ya nchi; nitatoa mifano kadhaa ya kasoro hizo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Nne, iliahidi kutoa kipaumbele katika suala la kilimo cha umwagiliaji maji, kwa kuchimba mabwawa ya umwagiliaji maji 160, wastani wa mabwawa 32 kila mwaka. Hali ya uchumi wa taifa, haielezi mabwawa yoyote yaliyochimbwa kwa sababu hakuna lililofanyika.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Nne, iliahidi kuwa itaongeza uzalishaji wa korosho toka tani 90,000 kufikia tani 180,000 mwaka 2010. Uzalishaji wa korosho, umepungua toka tani 122,287 msimu wa mwaka 2000/01 na kufikia tani 90,741 mwaka 2005/06. Kufuatana na Ilani ya CCM, uzalishaji wa kahawa unategemewa kuongezeka kufikia tani 120,000 mwaka 2010. Uzalishaji wa kahawa umepungua toka tani 76,428 msimu wa mwaka 2002/03 na kufikia tani 54838 mwaka 2006/07. Ni wazi, malengo ya Serikali ya Awamu ya Nne hayatafikiwa, kwa sababu hakuna sera sahihi za kilimo na wala hayakuwekewa mpango mkakati wa utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfumo wetu wa Bajeti bado hauko wazi, kiasi cha Wabunge kushindwa kufuatilia kwa undani, vifungu vya mapato na matumizi. Waziri alipokuwa akiwasilisha mtazamo wa Bajeti kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi, tatizo hili lilijitokeza. Hatuwezi kufuatilia na kujua fungu linaloitwa *Other Charges* na *Employment Allowance,* lina vifungu vingapi vidogo vidogo. Aidha, baadhi ya Wizara kama Elimu, Kilimo na Afya, fedha zao zinatoka katika mikondo zaidi ya minne, hivyo Wahasibu hasa wa Halmashauri, wanashindwa kufuatilia kwa undani, fedha zinazoingizwa katika Halmashauri zao, hasa kutokana na Halmashauri moja kuwa na Akaunti za Benki zaidi ya 500 huku tukielewa uwezo wa kiutendaji wa Halmashauri zetu. Ni dhahiri kuwa, mapato mengi ya Serikali yanazinufaisha zaidi Benki za Biashara kwa kuzifanyia biashara ya kununulia hati fungani na amana za fedha za Serikali, huku Halmashauri zikishindwa kutimiza majukumu yake. Haya tuliyasema mwaka jana, Kamati zimeyasema na hata

Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, sasa hivi nimemsikia akiyasema. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kurekebisha kasoro hizi ili kudhibiti mapato ya Serikali yawe kwa manufaa kwa wananchi wote. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Utaratibu huu unasababisha kujirudia *(double accounting),* kwa mapato na matumizi. Kambi ya Upinzani inaona huu ni upungufu mkubwa. Hapa kwetu mafungu ya Bajeti yanachukuliwa kwa ujumla jumla tu, hivyo kuwafanya Wabunge kutokufahamu kwa kina, matumizi ya mafungu hayo. Hii ni tofauti na nchi nyingine nyingi kama Zambia, Mauritius, Uganda na India kutaja chache tu, zinazofuata mfumo kama wa kwetu wa *CPA,* ambapo hata Mshahara wa Rais unaonyeshwa na Ziara za Rais, kwa mwaka zinajulikana. Aidha, ziara zote za Mawaziri, Wabunge na Watumishi wote zinaorodheshwa na hivyo kuifanya kazi ya Wabunge ya kuisimamia Serikali, kuwa rahisi lakini pia kuondoa mianya yote ya matumizi hewa. Kambi ya Upinzani inaona huu ni upungufu mkubwa unaohitaji kurekebishwa mara moja, kwani uwezekano wa kuwa na matumizi mabaya na au ubadhirifu na wizi wa mapato ni mkubwa.

Mheshimiwa Spika, bado Serikali inakusudia kutumia zaidi katika matumizi ya kawaida (Sh.4.726 trillion), kuliko matumizi ya maendeleo (Sh.2.489 trillion.). Zaidi ya hapo, katika miaka 12 ya Bajeti za nyuma, matumizi halisi ya maendeleo yamekuwa madogo kuliko yalivyoidhinishwa katika Bajeti. Hii ni kama tulivyowahi kusema kuwa, ukubwa wa Serikali utasababisha matumizi makubwa ya kawaida. Kambi ya Upinzani, inaona kuna kasoro kubwa ya kiuwiano kati ya matumizi ya kawaida na yale ya maendeleo, hivyo kuchelewesha ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini. Fedha nyingi zinatumika katika uendeshaji wa Serikali kuliko katika maendeleo na huduma za jamii na hivyo kupanda kwa Pato la Taifa, kutokuwa na manufaa ya moja kwa moja kwa mwananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali *(CAG),* katika Wizara na Idara za Serikali tulizochambua, mathalani tumebaini kuna upungufu wa makusanyo ya mapato, mrabaha usiokusanywsa kutoka Kampuni ya Almasi ya *Williamson Diamond Ltd.* ni shilingi 841,137,251 na *Tansort*, Sh. 206,662,556. Aidha, misamaha ya kodi nayo imekuwa ya kutisha, kwani hadi kufikia mwezi huu wa Juni, 2007, kiasi cha Sh. 819.9 *billion* zilikuwa zimesamehewa kama kodi. Kwa Zanzibar, misamaha ya kodi ilikuwa Sh. bilioni 19.6, wakati makusanyo yalikuwa Sh. bilioni 20.4. Misamaha mikubwa ya kodi ya Zanzibar ni ya vyakula hasa mchele; cha kushangaza bei ya mchele kabla ya msamaha ilikuwa shilingi 850 kwa kilo na baada ya msamaha ikawa ni shilingi 1,250. Je, misamaha hii inamnufaisha nani? *(Makofi*)

Huku misamaha hii mingi ukiondoa ya mashirika ya dini ikiwa haijamnufaisha mwananchi masikini, hiki ni kiasi kikubwa kwa nchi inayoomba misaada kila kukicha. Kambi ya Upinzani, inaona huu ni upungufu mkubwa wa mapato ya wanyonge wa Tanzania, kwa kuyatupa bila utaratibu wa wazi na unaoeleweka.

Mheshimiwa Spika, tunaomba kumalizia tathmini yetu kwa kukumbusha kwamba, Kambi ya Upinzani mwaka jana ilikataliwa ombi lake la kuunda Kamati ya Bunge kuchunguza *EPA, Twin tower*, *Mwananchi Gold Mine* na MEREMETA. Kambi ya Upinzani, inamtaka Waziri tena kutoa ufafanuzi, kuhusu mambo yafuatayo:-

(i) Waziri alieleze Bunge lako Tukufu, thamani halisi ya gharama za ujenzi wa majengo ya Benki Kuu *(Twin Tower),* ambayo kwa taarifa ya Benki Kuu, gharama imeshazidi *USD 500 million* au wastani wa Sh. 600 billion. Mjenzi bado hajakabidhi rasmi majengo, pamoja na kwamba, lilifunguliwa na Rais Mstaafu, Benjamin Mkapa mwaka 2005 kabla ya kustaafu. Aidha, kuna wasiwasi kuwa matumizi haya pia yalisababisha mfumko wa bei; tunataka maelezo. Pia tunamtaka atupatie taarifa ya uchunguzi uliofanywa na Benki Kuu yenyewe ili tuweze kulinganisha na taarifa tulizonazo.

(ii) Bunge lililopita tuliomba Bunge lako Tukufu lipewe maelezo juu ya uwekezaji wa BoT katika *Mwananchi Gold Mine* wa Dola za Marekani 5,512,398.55 hadi tarehe 30 Juni, 2006 kwamba, je, BoT iliendelea kuwekeza katika kampuni hiyo binafsi na kiasi gani cha mapato yaliopatikana hadi sasa? Tunataka Serikali itupatie maelezo ya kina, ambayo tunatumaini yatakuwa tofauti na ya mwaka jana, yatakuwa si majibu ya kisiasa. *(Makofi*)

(iii) Katika kikao cha Bajeti cha 2006, Bunge lilielezwa kuwa ule Mradi ulioasisiwa na Marehemu Baba wa Taifa wa kuwapatia wanajeshi wetu fedha kwa ajili ya kuendeshea Mradi wa Nyumbu, *MEREMETA Gold Mine*, ambayo ilikuwa chini ya uongozi wa *Time Mining* ya *South Africa* na kudhaminiwa na BoT kwa *USD 100 million*, ipo katika hatari ya kufilisika, lakini tukaambiwa kuwa BoT ilikuwa ikifanya tathmini. Kambi ya Upinzani, inataka kupata taarifa ya kina kuhusu tathmini iliyofanywa na BoT, juu ya mradi huo. Aidha, tunataka kupatiwa taarifa rasmi juu ya umiliki wa mgodi huu sasa. *(Makofi*)

(iv) Kuhusu *EPA,* tumeambiwa kuwa, Serikali itatoa taarifa rasmi Bungeni. Tunasubiri kwa hamu, Taarifa ya Serikali katika Mkutano huu wa Bunge.

(a) Katika Kamati tuliomba kupewa taarifa juu ya Tume ya Fedha ya Muungano *(JFC),* Waziri katika majibu yake (mwaka jana 2007/2008), kwa Kamati ukurasa wa pili alijibu, wakati uamuzi kuhusu mapendekezo ya Tume unasubiriwa, Bajeti ya 2007/08 imetenga mgao wa Zanzibar kwa utaratibu wa asilimia 4.5 ya misaada ya kibajeti. Mwaka huu Waziri katika hotuba yake, ukurasa wa 20 amesema, Tume ya Pamoja ya Fedha, inachambua maeneo ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi ya ziada ili kuziwezesha Serikali hizo mbili, kufikia maamuzi kuhusu mapendekezo ya Tume. Kambi ya Upinzani, mara hii inataka kupata terehe ya kuanza Mfuko huu. Hatuko tayari kuendelea kushiriki kuvunja Katiba ya Nchi. (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Spika, wakati Bunge lako likipitisha Muswada wa Sheria ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, Mheshimiwa Nimrod Mkono, aliomba ufafanuzi juu ya

mipaka ya kutumika kwa sheria hii na kusema kuwa, Zanzibar inapata fedha kutoka Serikali ya Jamhuri, lakini *CAG* hawezi kuzikagua. Waziri katika majibu yake, alikubaliana na hoja ya upungufu wa Sheria na Katiba.

(c) Mheshimiwa Spika, kwanza Serikali ikubali kuwa, yenyewe ndio iliyosababisha matataizo haya kutokana na kuvunjwa kwa Katiba, pale miaka yote ilipochelewa kuanzisha Tume ya Pamoja ya Fedha na baada ya kuanzishwa kushindwa kwa Tume hiyo hadi Mwenyekiti wake amemaliza muda wake bila kutekeleza mapendekezo ya Tume. Pili, sio kweli kwamba, Zanzibar inafadhiliwa na SMT, bali inapewa kidogo kuliko haki stahili ambayo ingepata, kama ingelikusanya kodi zake yenyewe, kuomba misaada na kukopa bila ya kupitia Serikali ya Jamhuri na hatimae kuchangia katika Mfuko wa Pamoja wa Muungano kama Katiba mbili zinavyoelekeza katika Katiba, ibara ya 135(1) na 136(1).

Ushahidi wa hayo ni pale SMZ ilipotoa bila ya malipo, MIG 7 za kivita, mizinga ya masafa marefu na mafupi kadhaa, magari ya TATA, fedha Taslim *USD 15 million*, ambazo hazikulipwa hadi leo na kadhalika. Hatuna haja ya kusema mengi, tatizo ni kutokutekelezwa Katiba, juu ya tafsiri sahihi ya mchango wa Mfuko wa Pamoja wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano. Wachangiaji ni nani kwenye Mfuko huo?

(d) Kambi ya Upinzani, mara hii inataka kupata tarehe ya kuanza Mfuko huu, hatuko tayari kuendelea kushiriki kuvunja Katiba ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, wakati tukiwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani katika Bajeti ya 2004/05, 2006/07 na 2007/08, tuliulizia juu ya kukiukwa kwa utaratibu wa kumpata mzabuni wa kuchunguza mauzo ya dhahabu, unaofanywa na Kampuni ya Alex Stuart Asseyers, mwaka huu tulitegemea Serikali ingelisema ni kiasi gani cha mapato kimepatikana kutokana na taarifa *ya* Alex Stuwart Asseyers, baada ya Serikali kuilipa kampuni hiyo si chini ya USD 65,000,000 sawa na Sh. Bilioni 85, inayotokana na mapato ya mrabaha wa asilimia 1.9 kati ya asilimia 3 inayopata Serikali. Kiasi hiki kingeweza kukopesha wanafunzi 20,000 wa Vyuo Vikuu, ambao leo tunawataka walipe kwa viwango mbalimbali. Kutokana na umaskini uliokithiri hivi sasa vijana wetu wengi wanashindwa kulipa hata zile asilimia wanazotakiwa kulipa, wakati rasilimali zao zinatolewa sadaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani na Watanzania kwa ujumla, tunaona huu ni upungufu mkubwa katika matumizi ya rasilimali na zaidi pale Serikali inaposhindwa kulieleza Bunge lako Tukufu, mapato yaliyopatikana kutokana na kazi ya Alex Stuwart Asseyers, badala yake imeunda Kamati ya Bomani, ambayo ni ya sita katika miaka mitano kuhusu jambo hilo hilo moja. Je, huku ndiko kuwaridhisha Watanzania na rasilimali zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Bajeti ya mwaka 2007/08, ukurasa wa 59, Serikali ilikusudia kuanzisha utaratibu wa kupitisha moja kwa moja *(fast tracking),* bila ukaguzi wa bidhaa zote zinazoagizwa.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu ni mzuri kama upo uadilifu wa kutosha wa walipa kodi na wakusanyaji wa kodi. Serikali ilipoona kuna udhaifu katika utekelezaji Bandarini, iliamua kukodisha shughuli za bandari kwa makampuni mbalimbali. Kambi ya Upinzani, ilitegemea Serikali kuja na tathmini ya utekelezaji wa makampuni hayo ili iwe rahisi kwa Bunge lako Tukufu kuamua juu ya utaratibu uliopendekezwa na Serikali, kama usimamiwe na *TRA* au kampuni binafsi, kwani kuna mashaka kwamba, makampuni yaliyoko bandarini yameshindwa kufanya kazi zao kama ilivyotakiwa.

Mheshimiwa Spika utaratibu wa *fast tracking,* unaweza kutumiwa kuficha udhaifu wa makampuni yaliyopewa kutekeleza shughuli za bandari. Aidha, utaratibu huu, unaweza kuwa njia moja ya kuipunguzia mapato Serikali. Kambi ya Upinzani, inamtaka Waziri atupe tathmini ya mpango huu, kwa kungalia makusanyo ya kodi kwa walipa kodi hao hao, wakati walipokuwa wakikaguliwa na sasa ambapo hawakaguliwi Bandarini.

Mheshimi Spika, inaeleweka kuwa, sehemu kubwa ya mapato ya bidhaa zinazoagizwa kutoka nje zinatokana na bidhaa za Petroli na Mafuta. Serikali imeweka viwango vya juu vya kodi katika mafuta hivyo, kufanya gharama za usafiri wa abiria na bidhaa kuwa kubwa na kumwongezea mzigo, Mtanzania anayeishi kijijini na kuyafanya maisha yake kuwa magumu zaidi. Kwa mfano, kodi zote kwa jjumla katika Petroli ni Sh. 545.10 kwa lita na kwa dizeli Sh. 520.80 kwa lita. Bei za mafuta ya dizeli kwa makao makuu ya mikoa kwa tarehe 16 - 31 Mei, 2008 ilikuwa kama ifuatavyo kwenye baadhi ya mikoa: Dar es Salaam Sh. 1,654.09 petrol na Sh.1,884.89 kwa dizeli kwa lita, huku mafuta ya taa yakiwa Sh.1,488.24 kwa lita; Kagera Sh.1,748.93 petrol na Sh.1,979.73 kwa dizeli kwa lita, huku mafuta ya taa yakiwa Sh.1,583.08 kwa lita; Kigoma Sh.1,930 petrol na Sh.2,080 dizeli kwa lita, huku mafuta ya taa Sh.1,550 kwa lita; na hali katika Mkoa wa Mbeya Sh.1,850 petrol na Sh.2,000 dizeli kwa lita, huku mafuta ya taa Sh.1,500 kwa lita; kati ya wastani wa bei ya Sh.1800 kwa lita. Hizi ni bei za mijini; vijijini ambako kuna umaskini uliokithiri na mahitaji ya nishati kwa ajili ya usafiri, kilimo na kadhalika, wastani wa bei ni Sh.2,200 kwa lita. Hivyo hivyo, kwa bei za bidhaa nyingine kama *cement*, mabati na kadhalika. Je, umaskini utapungua wakati sehemu kubwa ya jamii inaishi vijijini? *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi kama India, bei za vijijini na mijini ni tofauti na ndio maana wamemudu kuzalisha chakula cha kutosha. Ili kuendana na dhana nzima ya kukua kwa uchumi, kupunguza umasikini na kutekeleza programu nzima ya MKUKUTA na uzalishaji, kuna haja ya kufidia bei za bidhaa maalum vijijini. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali iondoe misamaha ya kodi kwa mafuta wanayotumia wazalishaji wa makampuni ya madini katika migodi mikubwa na ya kati na mapato yatakayopatikana yaanzishiwe Mfuko Maalum wa Kutoa Ruzuku kwa ajili ya nishati ya mafuta ili bei iwe sawa kwenye Mikoa yote *(Price Stabilization*).

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2008/09, kama nilivyoeleza wakati ninachambua matumizi ya Serikali ya mwaka 2007/08, matumizi halisi yaliyoainishwa katika hali ya Uchumi wa Taifa na Bajeti iliyopitishwa na Bunge ni vitu viwili tofauti. Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, hakufanya uchambuzi wa matumizi halisi kisekta au kwa kila fungu. Hatuna sababu ya kuamini kwamba, katika

Bajeti hii, matumizi yatafuata makadirio yatakayopitishwa na Bunge, hasa ukizingatia kuwa, Serikali bado haijasisitiza kuendelea na utaratibu wa *cash budget* wa kutumia tulichonacho.

Mheshimiwa Spika, tukizingatia umaskini wa Tanzania, umuhimu wa elimu na afya katika maendeleo na ujenzi wa nguvu kazi iliyo na tija, nafasi ya mapinduzi ya kilimo katika kuchochea kukua kwa uchumi, kuondokana na baa la njaa na kuutokomeza umaskini na ulazima wa miundombinu hasa barabara na nishati katika kuiwezesha sekta binafsi kuwekeza na kuzalisha bidhaa na huduma, mfumo wa Bajeti utakaokidhi mahitaji ya maendeleo ni kuitengea Elimu asilimia 22, Afya asilimia 11, Kilimo asilimia 12, Miundombinu asilimia 20, Maji asilimia 10, Nishati asilimia 8 na mambo mengine asilimia 17 ya Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa wastani Bajeti ya Serikali itumie asilimia 25 ya Pato la taifa. Asilimia 20 ya Pato la Taifa likusanywe kama kodi na mapato mengine ya ndani ya Serikali na asilimia 5 ya Pato la Taifa itokane na misaada. Kwa kuanzia, ikiwa misaada toka nje itakuwa mikubwa, Bajeti ya Miundombinu iongezwe ili kuongeza kasi ya kukua kwa uchumi. Uchumi unavyokua, mapato ya Serikali yataongezeka na kutegemea misaada ya nje kutapungua. Matumizi ya Serikali hayafuati mwongozo huu.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha na Uchumi, kaeleza kuwa, mapato ya ndani yamelengwa kufikia shilingi bilioni 4, 728.595 (trilioni 4.728), sawa na asilimia 18.5 ya Pato la Taifa (kwa takwimu za sasa). Hili ni ongezeko la asilimia 31 kutoka mapato yaliyotegemewa kukusanywa mwaka 2007/08. Mapato ya kodi yanakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 39, ukilinganisha na makadirio ya mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, Waziri hakufafanua maeneo yatakayoongeza mapato hayo. Ni vyema, angalau Waziri akatueleza vianzio vya mapato, haidhuru kwa mafungu makubwa kama vile kodi ya ongezeko la thamani *(VAT),* kodi ya ushuru wa forodha, kodi ya mauzo na *excise duty*, kodi na tozo ya mafuta, kodi ya mapato na kadhalika. Muswada wa Fedha vilevile haukutoa mwelekeo wowote katika maeneo mengi ya kodi. Ukiusoma Muswada wa Fedha, unaona kabisa Waziri anaomba *Blank Cheque* ya Bunge impe ili aweze kukusanya kodi. Hili ni tatizo kubwa. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri, atoe maelezo kwani hata kwenye *Finance Bill* nayo haifafanui vyanzo hivyo vya mapato ni vipi. Hili linatutia wasiwasi kuwa, Bunge halitaweza kujua vyanzo vya mapato kwa ajili ya Bajeti hii, kama ilivyo kwenye *Finance Bill, 2008;* vifungu vya 20, 21, 23, 24, 26 na vinginevyo, ambavyo havionyeshi kuwa vyanzo vya mapato hayo ni kitu gani, badala yake vifungu hivyo vinampa Waziri, mamlaka ya kuamua aina na tozo za Kodi kwenye mamlaka mbalimbali za Serikali bila hata kulitaarifu Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali ifanye utafiti wa kina, kuhusu vianzio vya kodi na kutoza kodi ambazo hazitabadilika badilika kila mwaka. Kwa mfano, mwaka

2007, Serikali iliongeza kodi ya mafuta mazito ya mitambo (*HFO*) kutoka shilingi 109 kwa lita hadi shilingi 117 kwa lita. Mwaka huu, imepunguza kiwango cha Ushuru wa Bidhaa kwenye mafuta mazito ya *HFO* kutoka shilingi 117 kwa lita hadi shilingi 97 ili kupunguza gharama ya uzalishaji viwandani na kuongeza uwezo wa ushindani wa bidhaa zetu katika soko. Je, mwaka 2007 ilikuwa haijulikani umuhimu wa mafuta haya katika uzalishaji viwandani?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa, Serikali haina mipango wala vipaumbele hivyo na ndiyo sababu kubwa kuwa viwanda si suala la muhimu, jambo lililopelekea hata *NDC* kutopewa fedha wakati ndiyo chombo cha Serikali kilichoundwa kuratibu na kuingia ubia na wawekezaji mbalimbali hasa wa viwanda na nishati. Hakuna nchi duniani inayoweza kuendelea bila ya sekta ya viwanda kuwa imara.

Mheshimiwa Spika, viwango vya ada za leseni za magari viliongezwa mwaka jana toka shilingi 20,000 na kuwa na viwango vinavyoanzia shilingi 80,000 hadi 230,000 kwa mwaka. Hata hivyo, Waziri alieleza kuwa, kwa magari yenye ujazo wa injini unaozidi CC5,000, kiwango cha ada kitakuwa shilingi 100,000 kwa mwaka. Haya ni magari ya mizigo na mabasi ya abiria. Mwaka huu, Waziri anaeleza kuwa, magari yenye ujazo wa injini unaozidi CC5000 yamepunguziwa kiwango cha ada kutoka shilingi 175,000 hadi shilingi 150,000. Kwa kuwa mwaka jana Waziri alilieleza Bunge kiwango cha ada kiwe shilingi 100000, mwaka huu anapendekeza kiwe shilingi 150,000; je, hili ni ongezeko au punguzo? *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mtazamo wa Kambi ya Upinzani Juu ya Vipaumbele vya Bajeti; kupunguza Bajeti tegemezi kutoka asilimia 42 mpaka asilimia 34. Katika jambo hili, Kambi ya Upinzani haina budi kuikumbusha Serikali, kile ambacho tulikisema kwenye Bajeti ya mwaka 2007/08 kuwa tuliweza kupunguza utegemezi wa Bajeti hadi kufikia asilimia 31.8. Tunaishukuru Serikali kwa kuyafanyia kazi mapendekezo yetu, japo haikuweza kufikia lengo tulilokuwa tumeliweka mwaka jana, kwani Serikali imeweza kupunguza utegemezi hadi kufikia asilimia 34 tu kwa makadirio ya Bajeti ya mwaka huu. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Katika mkutano uliopita wa Bajeti, tulisema sana juu ya jambo hili la kutegemea wafadhili katika maendeleo yetu. Kambi ya Upinzani, inaipongeza *TRA* kwa kukusanya mapato kwa kiwango marudufu, kulingana na miaka iliyopita. Lakini pia tulisema kuwa, uwezo wa Serikali kukusanya mapato ni mkubwa zaidi, ila kuna uzembe mkubwa na kutojali, ubadhirifu na ufisadi kama inavyodhihirishwa na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali mwaka hadi mwaka. Madhara ya Bajeti ya namna hii ni kwamba, tunapopata matatizo, inabidi kupitapita na kupunguza matumizi kadhaa ili tu kuweka hali sawa ya madhara yaliyotokea. Hii ni hatari kwa Maendeleo ya Watanzania kwa kiasi kikubwa, kwani hata Bajeti ya mwaka huu, baadhi ya Wizara zilipunguziwa fedha bila mpangilio. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, katika kuinua uchumi wa nchi na mwananchi, imeibua vyanzo vipya vya mapato. Vile ambavyo mwaka jana tulivisema na

baadhi kufanyiwa kazi na Serikali kwenye Bajeti yake ya 2008/2009, vingine imeshindwa kuvifanyia kazi. Viwango hivyo ni kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Uvuvi katika Bahari Kuu ni moja ya maeneo ambayo kama Serikali ingelikuwa makini na kuchukua maamuzi tunayopendekeza, mapato ya Serikali yangeliongezeka marudufu bila kugusa mafuta. Maeneo yenyewe ni kama yafuatayo:-

(i) Kuongeza ada ya leseni kwa meli za nje zinazovua katika Bahari Kuu hadi kufikia USD 50,000 kutoka inayotozwa sasa ambayo ni USD 18,000 kwa mwaka. Kulingana na takwimu zilizopo ni kuwa, kuna meli 140, japo Kumbukumbu za Bunge, Kikao cha Tatu, Tarehe 5 Februari, 2004, Serikali ilisema kuwa, imetoa leseni 193 za Meli za Uvuvi za nje, zilizopatiwa leseni za uvuvi katika Bahari Kuu ya Tanzania. Kwa maoni haya, mapato yatakuwa Sh. 9.5 bilioni, ambayo sasa hayakusanywi.

(ii) Kuongeza tozo la mrabaha wa mauzo la asilimia 10 katika bidhaa za samaki zinazovuliwa katika Bahari Kuu. Kila meli kwa mwezi, inavua wastani wa tani 2,000 za samaki, kwa makisio ya chini sana, japo kwa kawaida wanavua tani 1,500 kwa siku. Bei ya soko kwa kilo ya samaki ni USD 2.5. Kwa wanaojua biashara ya sekta hii, kiwango cha uvuvi ni kikubwa zaidi. Kwa maoni haya, mapato yatakuwa Sh. 370 bilioni, ambayo sasa hayakusanywi na Serikali.

(iii) Katika kuhakikisha kuwa, sekta hii ya uvuvi inaleta mabadiliko ya kiuchumi kwa nchi na wananchi kwa ujumla, Bandari za Mtwara, Dar es Salaam, Tanga na Zanzibar zinashauriwa zitenge maeneo ya bandari za samaki *(Fish Ports and Fish Processing Plants*) ili meli zote za uvuvi wa Bahari Kuu zilazimike kununua mahitaji yao yote ya mafuta, maji, chumvi na vyakula, wanapokuja kukaguliwa kwa ajili ya kukusanya mapato. Vyombo vyetu vya ulinzi, vikishirikiana na *TRA* na Mamlaka ya Uvuvi, kudhibiti mapato haya, kwa uamuzi huu mapato yatakuwa Sh. 3 bilioni, ambayo nayo sasa hayakusanywi na Serikali.

(iv) Uvuvi katika Maziwa ya Victoria na Tanganyika, haujadhibitiwa vizuri. Hivi sasa, kuna uvunaji haramu wa wastani wa tani 36,000 kwa mwaka. Uvunaji huu haramu ukidhibitiwa, Serikali inaweza kujipatia kiasi cha shilingi bilioni 45 kwa mwaka. Pia uvunaji huu haramu katika Maziwa hayo, matokeo yake viwanda vyetu vinakosa malighafi. Tunataka hatua ya dharura kuikabili hali hii, kwa kutumia vyombo vya ulinzi na *TRA* ili kuongeza mapato na ajira. Zoezi hili litaongeza wingi wa samaki, hivyo, viwanda vya samaki vitaongeza uzalishaji na kodi itaongezeka. Serikali imeshindwa kushughulikia jambo hili hadi leo.

Mheshimiwa Spika, maoni haya Kambi ya Upinzani, sio tu yamepanua wigo wa kodi, lakini pia kwa hatua hizo, tutakuwa tumedhibiti uvunaji wa rasilimali zetu ambapo sasa hazivunwi kikamilifu.

(b) Mheshimiwa Spika, chanzo kingine kikubwa ambacho vilevile mapato yake hayakusanywi sasa na Serikali ni katika sekta ya maliasili na hasa bidhaa za magogo na mbao. Kutokana na ripoti za kiutafiti kutoka kwa kundi la wahisani na pia asasi kadhaa zisizo za Kiserikali kama *TRAFFIC*; 2005/06, Serikali ilikusanya asilimia nne tu

ya mapato kwa mwaka 2004, yaliyopaswa kukusanywa kutoka katika bidhaa za magogo na mbao. Wanunuzi wakubwa ni China, India na Japan. Katika utafiti huo, katika kipindi cha 2001 – 2005, China peke yake ilinunua cubic mita 18,316 x $150 kwa rekodi za Maliasili Tanzania, kwa bei ya wastani wa *USD 2.7 million*, sawa na Sh. 3.5 bilioni na cubic mita 108,605 kwa rekodi za Forodha za China. Kwa maana hiyo, ama kwa ufisadi au vyenginevyo, Serikali imekosa mapato ya cubic mita 90,289 x $450 = $40.6 *million,* sawa na Sh.52.8 bilioni. Utafiti huu ulihusu magogo na mbao zinazotoka Mikoa ya Kusini tu. Taarifa hii, inathibitisha Taifa lilikoseshwa fedha kwa kuuza kwa Dola 150 tu, wakati bei halisi China ilikuwa Dola 450. Pia kiwango kilichouzwa kimefichwa. Huu ni Ufisadi.

Mheshimiwa Spika ,Kambi ya Upinzani, inataka majibu ya timu ya aliyekuwa Waziri wa Utalii na Maliasili, aliyosema kuwa ataituma China kwenda kuchunguza jambo hili ndani ya wiki mbili, ila hadi leo hatuna majibu ya timu hiyo. Pia Bajeti ya Waziri, haionyeshi kama kuna mapato yoyote yatakayopatikana kutokana na chanzo hiki.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inashauri hatua zifuatazo zichukuliwe: Halmashauri za Wilaya zilizo katika maeneo ambayo bidhaa hizi zinapatikana, ziwe mawakala wa kukusanya mapato kutokana na bidhaa za maliasili. Uamuzi huu, utapunguza kwa kiasi kikubwa ufisadi uliopo sasa katika Wizara ya Maliasili. Kila Halmashauri inayokusanya kodi, ipatiwe gawio kutoka sehemu ya makusanyo; Mapato yote yakusanywe na *TRA,* kwa kutumia stakabadhi za *TRA* kupitia Halmashauri za Wilaya kama ilivyoelezwa hapo juu; Mtu yeyote atakayekamatwa kwa kutorosha maliasili, afilisiwe kwa mujibu wa sheria, kama haipo itungwe; na *TRA* mbali na kukusanya mapato, ishirikiane na Bodi ya Mauzo ya Nje, kuhakiki bei za bidhaa zetu zinazouzwa nje ili kupata mapato halali ya rasilimali zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hatua hizi, mapato ya maliasili misitu, yataongezeka kwa asilimia 90 ya mapato ya sasa, makusanyo halisi yatakuwa Sh. 100 bilioni ambazo hazikusanywi sasa. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inaona kuwa, inakusanya mapato kwa wingi hadi kufikia asilimia 16.8 ya Pato la Taifa katika Sekta ya Utalii. Hata hivyo, Serikali imeshindwa kufikia malengo ya watalii milioni moja kwa mwaka, kama ilivyokuwa imepanga. Idadi ya watalii wanaokuja nchini ni wastani wa 719,031, isitoshe, Serikali imekuwa ikipoteza mapato kutokana na watalii kulipia gharama za safari zao na baadhi ya huduma kwa *Tour Operators* huko huko kwao kwa wastani wa USD 200 - 300 kwa mtu mmoja kwa siku. Mtalii anapofika Tanzania, huwa analipa wastani wa USD 80 - 150 tu. Hivyo, kuzipunguzia mapato hoteli zetu na kwa maana hiyo na Serikali. Kama watalii hawa wangelikuwa wanakuja katika *Package Tour* na kuwa tunakusanya wastani wa USD 100 kwa siku kwa kila mmoja kwa muda wa siku saba, ukiacha mapato yasiyo ya moja kwa moja, katika eneo hili Serikali ingelikusanya asilimia 30 kama kodi ya mapato, sawa na Sh. 67.5 bilioni, ambazo hazikusanywi hivi sasa.

(d) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu za Maliasili, kuna vitalu 152 vya uwindaji. Kwa wakati huu, Serikali inakodisha kwa wastani wa USD 7,500 kwa mwaka (mara nyingi wamiliki nao hukodisha kwa wenye fedha kwa wastani wa USD

100,000 kwa mwaka). Hii inatokana na ukweli kwamba, Tanzania ndiyo nchi pekee, yenye wanyama wengi na wa kila aina na pia itawaongezea Watanzania, umiliki wa mali yao. Katika eneo hili, Serikali ingekusanya mapato si chini ya bilioni 45, kama mapendekezo yetu yangefanyiwa kazi. Ili kuongeza mapato ya Serikali, Kambi ya Upinzani, inataka hatua zifuatazo zichukuliwe ili kuongeza mapato kama ifuatavyo:-

- Kuwajasirimisha Watanzania vitalu vyote vya uwindaji;

- Ili kupata thamani halisi, washauriwe kuingiza Vitalu hivyo katika soko la mitaji kwa kutumia *eletronic commerce;*

- Kupandisha viwango vya Kodi ya Uwindaji; na

- Kutoza asilimia 30 ya mapato yatokanayo na Mtanzania atakayekodisha kwa mtu mwingine.

Mheshimiwa Spika , Kambi ya Upinzani, inaamini kuwa, hatua hizi zinawezekana kwani Tanzania ni nchi ambayo imejaliwa wanyama wengi zaidi kuliko nchi nyingine za Bara la Afrika. Wanyama wanene zaidi na ambao wanaishi kwenye mazingira halisia na hivyo kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kipekee na kuwavutia wawindaji kutoka sehemu mbalimbali za ulimwengu, kutaka kuja na kuwekeza kwenye Sekta ya Uwindaji. Kwa hatua hii, Watanzania watakuwa wamewezeshwa kumiliki rasilimali zao wenyewe na pia kwa kuongeza viwango vya kodi ya uwindaji, makusanyo yanakisiwa kuwa Sh. 85 bilioni, ambayo hayakusanywi hivi sasa.

(e) Mheshimiwa Spika, mapato katika Sekta ya Madini; kulingana na ukaguzi uliofanywa na Kampuni ya Alex Stuart, kwa kipindi cha miaka mitatu, Serikali imepoteza shilingi 1.3 trilioni. Hii imetokana na Serikali kutokuwa makini katika kufuatilia nyaraka halali zinazotumiwa na makampuni ya kuchimba madini. Ili kuifanya sekta hii ya madini kuwa na manufaa kwa Taifa na Watanzania wote, hatua zifuatazo zikichukuliwa sekta hii itachangia zaidi:-

(i) Kufanya mapitio ya sheria ya madini na kupandisha asilimia ya mrabaha toka 3 hadi 5 kwa kuanzia;

*(ii)* *TRA* kuimarishwa kiutendaji na kukusanya kodi zote katika Sekta ya Madini;

(iii) Katika mpango wa maendeleo wa kampuni husika, maendeleo ya jamii zinazozunguka migodi yaonekane wazi wazi na kuingizwa katika mpango wa mwekezaji;

(iv) Kati ya asilimia 5 za mrabaha utakaotozwa, asilimia 2 ibaki katika Halmashauri ya Wilaya/Mji ambamo mgodi upo;

(v) Katika masharti ya kuwekeza kwa wageni ni lazima waingie ubia na Mtanzania au Halmshauri angalau kwa asilimia 10, ikiwa ni pamoja na thamani ya ardhi;

(vi) Kuweka sharti ndani ya Mikataba na kubadilisha Sheria kwamba, atakayekiuka mkataba au kusafirisha mali itokanayo na rasilimali za nchi, kampuni husika itafilisiwa; na

(vii) Kuhakiki madeni waliyokopa wawekezaji ili kupata kiasi halisi walichokopa, ikiwa ni pamoja na *Tax Holiday*, kwa lengo la kufuatilia muda wa Kusamehewa kodi.

Mheshimiwa Spika, Rais Kikwete, aliunda Kamati ya kupitia Mikataba ya Madini, mwezi Novemba, 2007 kufuatia Hoja Binafsi ya Buzwagi. Kamati imetoa mapendekezo; swali la kujiuliza ni je, mapendekezo ya Kamati yamezingatiwa vipi kwenye Bajeti hii ya mwaka 2008/2009? Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali, kuiwasilisha Ripoti hiyo ndani ya Bunge mapema iwezekanavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna taarifa kuwa, Serikali imepoteza zaidi ya shilingi 883 bilioni katika kipindi cha miaka 10, kutokana na sheria mbaya ya kodi ya mapato katika Sekta ya Madini iliyotungwa na Bunge mwaka 1997.

Kupitia *Financial Laws (Miscellaneous Ammendments*) *Act*, 1997, nafuu ya ziada ya uwekezaji asilimia 15 iliwekwa na kuleta upotevu huo wa mabilioni ya fedha za kodi. Sheria hii bado ipo katika sheria za nchi, kwa kampuni zote zenye Mikataba (*MDA*), kabla ya mwaka 2001. Kambi ya Upinzani Bungeni, ilitarajia kuwa Serikali ingefuta sheria hii na kuangalia uwezekano wa makampuni ya madini kulipa fedha hizi, kwani nafuu haikuwa na ulazima wowote na haimo katika kanuni za kodi. Kambi ya Upinzani, inategemea kukusanya mapato haya kwa kiasi cha shilingi 88.3 bilioni. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa, msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwenye mafuta kwa makampuni ya madini ufutwe. Mwaka 2007/2008, Serikali kupitia msamaha huu, haikukusanya shilingi 59 bilioni kutoka kwenye makampuni sita ya madini. Waziri wa Fedha, hajagusia kabisa msamaha huu ambao unalitafuna taifa, kulikosesha mapato na hivyo kupunguza faida ya ukuaji wa Sekta ya Madini katika uchumi. Kambi ya Upinzani, inataka msamaha wa kodi ya ushuru wa mafuta kwa makampuni ya madini ufutwe mara moja. Katika eneo hili, Serikali ingekusanya shilingi 59 bilioni, ambazo hivi sasa zinatolewa sadaka. Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali, iondoe misamaha ya kodi kwa mafuta wanayotumia wazalishaji wa makampuni ya madini katika migodi mikubwa na ya kati na kuanzisha Mfuko Maalum wa kufidia punguzo la mafuta yanayopelekwa vijijini. *(Makofi*)

Aidha, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali ilieleze Bunge lako Tukufu, pamoja na wananchi kwa ujumla, juu ya hali ya uchimbaji wa madini mbalimbali katika machimbo ya Kabanga Nikel yaliyoko Mkoani Kagera, Wilaya ya Ngara na uhalali wa wachimbaji walioko kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni, inaona kuwa Serikali inafanya mzaha na umuhimu wa Sekta ya Madini katika mapato ya Serikali na kwamba, kitendo cha Waziri kutokuzungumzia chochote juu ya Mapendekezo ya Kamati ya Rais na utekelezaji wake ni dalili tosha kuwa, Serikali inatilia maanani zaidi maslahi ya wawekezaji kuliko ya Watanzania. Serikali ituambie kwa nini wawekezaji wa madini wanaogopwa?

(f) Mheshimiwa Spika, Taarifa mbalimbali za kitafiti zinaonyesha kuwa, Tanzania inapoteza mapato mengi sana katika madini ya vito, kwa sababu ya uzembe, kukosa udhibiti na ufisadi. Kwa mfano, Katika soko la dunia, mauzo ya *Tanzanite* mwaka 2005 yalikuwa na thamani ya Dola za Kimarekani 400 milioni. Hata hivyo, rekodi ya Tanzania ni Dola 16 milioni tu. Tuna taarifa kuwa, Kenya ilipata tuzo kwa kusafirisha *Tanzanite* nyingi duniani wakati hawana *Tanzanite.*

Kwa kutumia vito vyetu vya aina mablimbali, kama vile *Tanzanite, Alexadrite, Safaya, Ruby* za aina zote na kadhalika, Serikali ingeliweka usimamizi madhubuti, tungeweza kulipatia taifa fedha kwa ajili ya kuendesha uchumi na kuwanufaisha wananchi wengi zaidi, kuliko hali ilivyo hivi sasa kuwa wananufaika zaidi wawekezaji wakubwa tu huku wananchi wa maeneo yenye vito hivyo, wakibakia kwenye lindi la umaskini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali ingekubaliana na ushauri wa Kambi ya Upinzani, Serikali ingepitia upya kabisa mwenendo mzima wa biashara ya madini haya ili kuwa na chanzo kimoja tu cha mauzo. Udhibiti huu ungeipatia Serikali mapato ya jumla ya Sh. 200 bilioni, ambayo hayakusanywi hivi sasa.

(g) Mapato katika kodi nyingine:-

(i) Misamaha ya Kodi; eneo lingine ambalo tumekuwa tukipoteza fedha nyingi sana ni eneo la misamaha ya kodi. Kama ilivyo katika taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge, inakadiriwa kuwa, takribani shilingi 819.9 bilioni zilitolewa kama misamaha ya kodi katika mwaka wa fedha unaomalizika. Aidha, hali ya misamaha ya kodi kwa upande wa Zanzibar, ilikuwa ni ya kutisha kwani mwaka 2006/07, *TRA* ilikusanya kiasi cha shilingi 20.4 bilioni, huku misamaha ya kodi mbalimbali ikifikia shilingi 19.6 bilioni; hili ni jambo la ajabu sana, kwani misamaha hii ukiondoa ile inayolenga mashirika na madhehebu ya kidini, haiwanufaishi wananchi maskini wa taifa hili. Ili kuongeza mapato yetu ya ndani, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali, ipunguze misamaha ya kodi kwa asilimia 50. Uamuzi huu utaweza kuongeza mapato ya Sh. 409.95 bilioni, ambazo hazikusanywi hivi sasa.

(ii) Kodi katika Posho *(allowances*); kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato Na.11 ya Mwaka 2004, kifungu cha 7(1) na (2), kila atakachokitoa mwajiri itabidi kikatwe kodi, isipokuwa kama mfanyakazi atatumia fedha zake na mwajiri akamrudishia. Kwa mujibu wa Sheria hii, posho zote za warsha, semina, makongamano, mikutano na vikao, zinapaswa kukatwa kodi ya mapato. Hii pia inajumuisha posho

wanazopata Waheshimiwa Wabunge, kutokana na vikao hapa Dodoma na Dar es Salaam. Ikirekebishwa Sheria ya Kodi ili kutoza kodi mapato haya kwa kiwango cha *VAT*, yaani 20, hatua hii pia ingelenga kupata manufaa yafuatayo:-

(a) Mifuko ya Pensheni itapata wanachama zaidi.

(b) Kodi ya Serikali ambayo ni ya uhakika (P.A.Y.E. itapanda maradufu, kwani *employment allowance* haitozwi).

Mheshimiwa Spika, uamuzi huu Serikali ingepata mapato ya Sh. 8 bilioni, mbazo hazikusanywi hivi sasa.

(h) Mheshimiwa Spika, eneo lingine linaloinyima Serikali mapato yake ni uuzwaji wa hisa zake kwa bei isiyokuwa ya soko. Kwa mfano, hisa asilimia 25 za Serikali za Williamson Diamond ziliuzwa kwa USD 183,000 tu na pia kuna taarifa kuwa, asilimia 25 za Serikali zilizokuwa zimebakia zimetolewa bure kwa mwekezaji; tunataka maelezo kutoka Serikalini juu ya taarifa hizi. *NIC,* ilitaka kubinafsishwa kwa thamani ya Sh. 3 bilioni tu, hadi Kamati ya Fedha na Uchumi ilipodai tathmini mpya, kulingana na tathmini mpya iliyofanywa na Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi, thamani imepanda hadi shilingi 6 bilioni.

Mheshimiwa Spika, hisa za *NMB* zinatarajiwa kuuzwa kwa Sh. 58 bilioni. Kiwango hiki ni cha chini, kulingana na ukweli kuwa, *NMB* ni benki inayopata faida sana na imeweza kutoa gawio kwa wanahisa wake. Kambi ya Upinzani, tunaitaka Serikali kuuza hisa zake za NMB kwa bei ya soko.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekubali maoni ya Kambi ya Upinzani, kuhusiana na thamani ya hisa za Benki ya *NMB.* Mwaka 2007/2008, Serikali ilikadiria kupata 15 bilioni kwa kuuza hisa za Benki ya *NMB.* Kambi ya Upinzani, tukasema thamani ya hisa ilishushwa makusudi. Sasa Serikali imekadiria kupata Sh. 58 bilioni. Hii inaonyesha jinsi Kambi ya Upinzani, inavyojali maslahi ya wananchi na tunaitaka Serikali itekeleze maoni yetu yote kwa manufaa ya wananchi na sio hilo moja tu. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaamini kuwa, thamani halisi ya hisa za Serikali za *NMB* ni shilingi 120 bilioni, badala ya shilingi 58 bilioni za Serikali.

Mheshimiwa Spika, bado kuna makampuni ambayo Serikali ina hisa, ambayo sasa ingefaa hisa hizo kuuzwa kwa wananchi lakini Serikali ipo kimya katika hili. Kwa mfano; kwa nini Serikali haiuzi hisa zake zilizoko katika Benki ya *CRDB* na Kampuni ya Simu ya *CELTEL* katika soko la hisa, ili ipate mapato ya kuendesha uchumi? Iwapo Serikali ingeuza hisa zake, ingeweza kupata fedha kulipia punguzo la kodi ya mafuta kwa wananchi na wazalishaji katika mwaka wa fedha 2008/2009. Kenya wameuza hisa zao za Safaricom na zimekuwa *over-subscribed.* Soko la Hisa la Dar es Salaam, lapaswa kuboreshwa kwa kuingiza makampuni mengi zaidi ili kumilikisha wananchi hisa za makapuni na kufanya biashara ya hisa kuwa nzuri na yenye kuweza kutabirika.

(i) Mapato kutokana na Bandari ya Mtwara na Tanga; Mheshimiwa Spika, Eneo lingine ambalo bado halijatumiwa vizuri ni la kuuza mauzo nje ya nchi na hasa nchi jirani *(Bonded Goods).* Kama Bandari ya Mtwara, ingejengewa maghala ya kuhifadhia mazao na bidhaa kwa kufanya mauzo ya bidhaa zetu za viwandani kama vile *cement*, mifugo, mchele na bidhaa nyingine katika nchi ya Comoro, ambayo matumizi yao ni saruji tani 70,000, mchele tani 40,000 kwa mwaka na ng'ombe ni 4,000 kwa wiki. Comoro inaitegemea sana Tanzania, katika vyakula na vifaa vya ujenzi. Aidha, tutasukuma uuzaji wa bidhaa zetu nje kama muhogo, korosho, ufuta na samaki. Uimarishaji huu, utaweza kutuingizia kiasi cha shilingi bilioni nne kutokana na kodi peke yake, ambayo sasa haikusanywi.

(j) Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa, mfumo wa leseni za madereva uboreshwe kwa kutoa leseni mpya, kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya kompyuta. Leseni hizi zitakuwa na uwezo wa kuhifadhi taarifa zote muhimu za madereva. Hii itasaidia kupunguza uhalifu na hasa ajali za barabarani na pia itakuwa ni sehemu ya kitambulisho. Mradi huu uendeshwe kwa utaratibu wa *PPP.* Kwa makisio ya chini, madereva laki mbili na nusu; mwaka huu wa fedha na ada ya leseni kuwa Sh. 50,000, tutakusanya jumla ya shilingi bilioni 6.25, ambazo sasa hazikusanywi.

(k) Mheshimiwa Spika, kutokana na dhamira yetu toka mwaka 2003 kwamba, ununuzi wa ndege ya Rais ni anasa na gharama zisizo na msingi, kwa sasa Serikali inatumia shilingi milioni sita kwa saa ya kuruka ndege hii. Kambi ya Upinzani, bado inaendelea na ushauri wake kwamba, ndege hii kama alivyofanya Rais wa Ghana, Bwana John Kufouri, iuzwe kwa mnada. Kwa uamuzi huu, Serikali itapata mapato ya shilingi bilioni 30. Pia hatua hii, itaiwezesha Serikali kupata fedha za kutengenezea ndege zake.

Mheshimiwa Spika, ushauri huu uliotolewa na Kambi ya Upinzani, kama Serikali ingekubali kuufanyia kazi kuhusu sera ya mapato, yangeipatia Serikali jumla ya mapato ya ziada ya Sh. 2,234.348 bilioni. Ushauri wa mapato haya yote ni kutokana na kuboresha vianzio vilivyopo na Kubuni vipya, ambavyo Serikali haikuviona.

Kuwarahisishia Watanzania, kwa kuifanya mamlaka ya manunuzi nchini ijitegemee, kwa kutumia utaratibu wa manunuzi wa mtandao (*e-Procurement),* kwa ajili ya kusajili makampuni katika ngazi za Wilaya, Mkoa hadi Taifa na nje, zinazotoa huduma kwa Serikali. Kuiboresha mamlaka hii ili isaidie kupunguza rushwa katika manunuzi na kuipunguzia Serikali bei ya manunuzi kwa wastani wa si chini ya asilimia 15 ya manunuzi yake yote. Njia hii itatuingizia mapato kiasi cha shilingi 250 bilioni.

Mheshimiwa Spika, muhtasari, wa ushauri wetu juu ya vyanzo vipya vya mapato ya Serikali ni kama ifuatavyo:-

Leseni za meli zinazovua kwenye Bahari Kuu shilingi bilioni 9.5; mrabaha kutokana na uvuvi katika Bahali Kuu shilingi bilioni 370; mapato kutokana na mafuta kwa meli za uvuvi shilingi bilioni 3.0; mapato kutokana na bidhaa za misitu shilingi bilioni 100; mapato kutokana na Bandari ya Mtwara na Tanga shilingi bilioni 4.0; mapato kutokana na punguzo la asilimia 70 ya misamaha ya kodi ni shilingi bilioni 409.9; kodi

ya asilimia 20 kutokana na posho za semina na kadhalika shilingi bilioni 8.0; mauzo ya hisa za Serikali kama *NMB* shilingi bilioni 120; ukusanyaji wa kodi isiyokusanywa kwenye madini shilingi bilioni 88.3; ushuru wa mauzo kutokana na madini ya vito shilingi bilioni 100; mapato kutokana na vitalu vya uwindaji wa kitalii ni shilingi bilioni 85; mrabaha wa asilimia tano katika madini shilingi bilioni 41.8; mauzo ya ndege ya Rais shilingi bilioni 30; mapato kutokana na leseni za madereva shilingi bilioni 12.5; mapato kutokana na utalii shilingi bilioni 67.5; kodi isiyokusanywa *Williamson Diamond Ltd.* shilingi milioni 841; mapato kutokana *Tansort* shilingi milioni 206.6; *e-procurement* shilingi 250 bilioni, ushuru wa mafuta, makampuni sita ya madini shilingi bilioni 59; mauzo ya hisa *CELTEL* shilingi bilioni 243 na fedha *(commitment)* za *EPA* shilingi bilioni 131.8. Jumla ni shilingi tilioni 2.2.

Mheshimiwa Spika, kwa ushauri wa mapendekezo yetu ya mapato, tungeweza kukusanya jumla ya shilingi trilioni 5.7 kama mapato ya ndani. Makusanyo haya yangekuwa ni ziada ya makusanyo, ambayo Serikali imepanga kuyakusanya kwa kiasi cha shilingi trilioni 4.7. Tofauti ya zaidi ya shilingi trilioni 1.030 na bila kumuumiza mwananchi wa kawaida. *(Makofi*)

Mheshimiwashimiwa Spika, tukizingatia kuwa, nchi yetu itapata misaada na mikopo kutoka nje kama jinsi ambavyo imeainishwa katika Makadirio ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2008/9, Makadirio ya Mapato ya Bajeti hii yangefikia jumla ya Sh. 8.166 trilioni.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kambi ya Upinzani kuainisha vyanzo vipya mbalimbali vya kodi, ambavyo havimuumiza mwananchi wa kawaida na pia baada ya mapato ya Serikali kuongezeka kutokana na vyanzo hivyo; tunaitaka Serikali ichukue hatua zifuatazo ili kuweza kuinua uchumi na kukuza ukuaji wa Pato la Taifa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuongezeka kwa mapato ya ndani, Kambi ya Upinzani inashauri kiwango cha chini cha mshahara wa wafanyikazi wa umma kiwe Sh. 250,000 kwa mwezi; na kwa ngazi nyingine mshahara ungepanda kwa asilimia ambayo italeta uiwiano baina ya kipato cha chini na cha juu. Ufafanuzi wa kina utatolewa na Waziri Kivuli wa Utumishi wa Umma. Kiwango hiki hakitatozwa kodi ili kuweza kumfanya mtumishi wa ngazi ya chini, aweze kumudu gharama za maisha, japo hatua hii itapunguza mapato ya Serikali kwa kiasi fulani.

Mheshimiwa Spika, elimu ni kipaumbele chetu kikuu katika matumizi ya Serikali. Kwa maoni ya Kambi ya Upinzani ni kuwa, Serikali imejikita zaidi katika hatua ya awali; kuwa na shule nyingi na idadi kubwa ya wanafunzi, jambo ambalo limefanikiwa kwa kiasi kikubwa. Kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na Kambi ya Upinzani ya kutafuta mapato zaidi, muono wetu ni kuimarisha hatua iliyofikiwa kwa kuelekeza matumizi yetu katika kuboresha viwango vya elimu ili kuwa na elimu bora. Hivyo, tunashauri kuwa, tuhakikishe mkazo mkubwa unawekwa katika kuwaelimisha walimu, katika ule mtindo wa zamani. Pia Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali, kuondoa kodi kwenye vifaa vyote

vya elimu kama vitabu, madaftari, kalamu na kadhalika. Hatua hii itawawezesha wananchi kuweza kumudu gharama za kusomesha watoto wao na kuliendeleza taifa .

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kupunguza kodi kwenye mafuta ya petrol na dizeli, kwa kiasi cha shilingi 250 kwa kila lita moja ya mafuta hayo. Hali hii itamwezesha mwananchi maskini kuweza kumudu gharama za maisha na hata kuweza kukuza uchumi wa wananchi maskini.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuondoa ushuru mpya uliopendekezwa kwenye vinywaji na hasa bia, ambazo malighafi inayotumika kuzitengeneza, inapatikana hapa nchini na hii inalenga kuwanufaisha wakulima ambao wanazalisha malighafi hizo. Pia vinywaji baridi kama soda, ushuru unaopendekezwa na Serikali hakuna budi uondolewe.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali, kuondoa kodi zote za vifaa vya kilimo kama vile majembe ya trekta, vipuri na kadhalika. Hatua hii itamwezesha mwananchi maskini, kuweza kumudu kutumia zana za kisasa katika uzalishaji na kukuza tija ya kilimo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuondoa kodi kwenye malighafi ya kutengenezea Majiko ya Moto poa. Hii ni hatua muhimu ili kuhakikisha kuwa, wananchi wanaweza kumudu gharama za kununulia majiko hayo. Serikali isiondoe kodi kwenye mafuta tu, kwani wananchi watashindwa kumudu kuwa na uwezo wa kupata mashine hizo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuondoa ushuru uliopendekezwa kwenye magari yote yenye CC zaidi ya 5000, kwani magari haya ni malori na mabasi kwa ajili ya abiria. Hatua hii, itawawezesha wananchi kuweza kumudu gharama za nauli na pia kuweza kusafirisha vyakula kwa kutumia malori hayo hadi kwenye masoko na hili litapunguza bei kubwa ya kununua vyakula.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kambi ya Upinzani, juu ya utaratibu wa mgao wa kutumia fedha; kama tulivyoshauri katika hatua mbalimbali za maoni yetu, katika kutekeleza mipango ya Serikali na kuwafanya watekelezaji wa mipango hiyo waweze kutekeleza vyema, utaratibu wa *Cash Budget* haufai. Utaratibu uliokuwa unatumika zamani wa *Warrant System* urudiwe. Aidha, fedha badala ya kutolewa kwa mtindo wa kila mwezi, utaratibu wa kutoa fedha kwa kipindi cha miezi minne minne utumike.

Kwa mujibu wa vipaumbele tulivyoshauri, viwango vyetu vya mgao vitakuwa kama ifuatavyo: Elimu asilimia 22 sawa na Sh. 1,796.5564 bn; Miundombinu asilimia 20 sawa na Sh. 1,633.2332 bn; Kilimo asilimia 12 sawa na Sh. 979.9398 bn; Afya asilimia 11 sawa na Sh. 897.2782 bn; Nishati asilimia 8 sawa na Sh. 653.2932 bn; Maji asilimia 10 sawa na Sh. 816.61656 bn; na matumizi mengine asilimia 17 sawa na Sh. 1388.2481 bn.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kambi ya Upinzani juu ya sura ya Bajeti ni kama ufuatao: Mapato ya Ndani Sh. 5,736.9306, mikopo na misaada ya nje ikijumuisha *HIPC/MDRI* Sh. 2,429.535 bn; jumla ya mapato yote ni Sh. 8,166.1656 bn. Matumizi ya Kawaida Sh. 3,940.213; Deni la Taifa Sh. 648.284 bn; Wizara, Mikoa na Halmashauri Sh. 2,907.929 bn; na matumizi mengine Sh. 384.0 bn. Matumizi ya Maendeleo Sh. 4,225.952 bn; jumla ya matumizi yote Sh. 8,166.1656 bn.

Viwango vyake vya fedha vimebadilishwa. Kutokana na mchanganuo huo, tofauti za kimsingi kati ya Waziri wa Fedha na Ushauri wa Kambi ya Upinzani ni kama ifuatavyo: Ushauri wa Kambi ya Upinzani kupitia Bajeti hii Kivuli, utaiwezesha Serikali kutumia fedha za ndani kwa miradi ya maendeleo hata kama wafadhili wataondoa fedha zao, tutaweza kutekeleza miradi yote ya sasa, fedha za wafadhili zitakuwa ni ziada tu. Hivi sasa, bajeti yetu ya maendeleo inategemea wafadhili kwa asilimia 63. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kambi ya Upinzani kufuatia Bajeti hii Kivuli, utaiwezesha Serikali kutumia kiasi kisichopungua asilimia 51 ya bajeti yote, kwa ajili ya maendeleo, badala ya asilimia 34 tu iliyowekwa na Serikali. Ushauri wa Kambi ya Upinzani kupitia Bajeti hii Kivuli, utaiwezesha Serikali kupunguza bajeti tegemezi, mikopo na misaada kutoka kwa wahisani; aslimia 30 ya bajeti nzima kivuli, badala ya utegemezi wa asilimia 34 ulioainishwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, mlinganisho wa kati ya ushauri wa Kambi ya Upinzani kupitia bajeti yake kivuli na sura ya Bajeti ya Serikali, umo katika kiambatanisho cha hotuba hii. Lengo kuu la ushauri wa Kambi ya Upinzani, kupitia bajeti hii kivuli niliyoiwasilisha ni kuchochea ukuaji wa uchumi, kuondokana na bajeti tegemezi kama Taifa na kuwa na Taifa lililoelimika na lenye utawala unaoheshimika. Katika hotuba yetu, nimeonyesha wazi wazi kuwa, tunazo fursa kubwa za kupata mapato ya ndani, tatizo ni mtazamo wa kifikra *(mindset)*. Changamoto kubwa tuliyonayo kama Taifa ni kwa viongozi kuwa tayari kujifunza kutoka kwa wengine, bila kujali itikadi za kisiasa, ili kwa pamoja tuwaondolee umaskini Watanzania waliokalia rasilimali zinazozidi mahitaji yao.

Lazima sote tujiulize; kwa nini wageni na wajanja wanatajirika, lakini wakulima na wafanyakazi wetu ni maskini? Taifa hili ni letu, tusemezane, tujadiliane na hatimaye tusonge mbele. Tuliyosema yanawezekena, yanahitaji viongozi na watumishi kuweka maslahi ya Taifa mbele. Rasilimali tulizonazo zinatosheleza kama zitasimamiwa na kutumika kwa maslahi ya watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tena kukushukuru na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wote, kwa kunisikiliza. Mungu ibariki Tanzania. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Msemaji kwa Sekta hii ya Fedha na Uchumi na Kiongozi wa Upinzani Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, nimepokea majina 62, muda tunao, wote watapata nafasi tu. Naomba niwatamke watano wa kwanza ili wajipange na wawepo ukumbini. Kwa Hotuba hii ya Bajeti ya Serikali, msemaji wa kwanza ni Mheshimiwea Victor Mwambalaswa, wa pili Mheshimiwa Mgana Msindai, wa tatu Mheshimiwa Esther Nyawazwa, wa nne Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, halafu Mheshimiwa Suleiman Saddiq ndiye wa tano. Kwa hiyo, nitaanza sasa na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, nitaomba afuatie Mheshimiwa Mgana Msindani na wakati huo huo Mheshimiwa Esther Nyawazwa ajiandae.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru sana kwa kunipa nafasi kama mchangiaji wa kwanza wa hoja hizi mbili ambazo ziko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumpongeza sana Waziri wa Fedha na Serikali kwa ujumla, kwa kushusha utegemezi katika bajeti kutoka aslimia 42 mpaka asilimia 34. Ninaiomba Serikali itumie nafasi hiyo, kutumia mikopo na misaada tunayoipata kutoka kwa wahisani, ilenge katika nyanja ambazo zitaiongezea nchi kujitegemea zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri, mimi naichukulia kama kihenge. Umejenga kihenge chako kizuri, kuta zako imara, umeezeka vizuri sana na magrili mengi, umeweka na mlinzi wa kulinda usiku na mchana ili kulinda nafaka kwenye kihenge chako, lakini mwaka unaisha, watoto hawanenepi, wala familia hainenepi na nafaka inapungua kwenye kihenge! Hii ni kwa sababu, kwa maoni yangu nii kwamba, pamoja na kuweka kihenge kizuri, kuezeka vizuri na magrili, lakini hukuweka sakafu imara. Kwa sababu hiyo, kuna panya buku ambao wanakula nafaka; nafaka inapungua bila kuona, kwa hiyo familia hainufaiki na nafaka zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwangu mimi hii nafaka ni sawa sawa na bajeti. Bajeti ya Serikali ni shilingi trilioni 7.2, ipo ndani ya kihenge; katika hiyo, matumizi ya kawaida ni shilingi trilioni 4.7 na matumizi ya maendeleo shilingi trilioni. Panya buku tuliyenaye ni manunuzi ya umma. Katika hiyo shilingi trilioni 4.7 ya matumizi ya kawaida ya Serikali, asilimia 70 inakwenda kwenye manunuzi ya umma. Katika matumizi ya maendeleo shilingi trilioni 2.5, asilimia 100 inaenda kwenye manunuzi ya umma, ambayo ina maana katika hiyo shilingi trilioni 7.2; shilingi trilioni 6 inaenda kwenye manunuzi ya umma.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya manunuzi ya umma ni panya buku ambaye tumempuuzia. Tumejenga kihenge kizuri, bajeti ipo pale, tumeweka magrili na nondo, kuna Mdhibiti Mkuu wa Serikali tumempa na sheria mpya wiki iliyopita, ndiyo nondo hizo. Wizara ya Fedha, imeweka Hazina Ndogo katika kila Kanda na katika kila Mkoa.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006, Wizara ya Fedha iliajili na kufundisha Wahasibu ikawapeleka kwenye Halmashauri, yote hiyo ni katika kujenga kuta nzuri na kuezeka vizuri, lakini manunuzi ya umma tumeyasahau.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, katika bajeti hii, Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri sana kwamba, kuanzia mwaka huu, kwa sababu ya ubovu waliouona kwenye manunuzi ya umma, wanahamisha kitengo cha ununuzi kutoka Wizara ya Miundombinu kwenda Wizara ya Fedha. Vilevile ujue kwamba, miaka yote Kitengo cha Ununuzi kipo Wizara ya Miundombinu na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ipo Wizara ya Fedha. Ukienda pale Wizarani, hakuna Mkurugenzi anayeshughulikia manunuzi, wala anayeshughulikia sera, kwa sababu tumeyapuuzia manunuzi ya taifa na huyo ndiyo panya buku ambaye anakula fedha za wananchi na ndiyo maana wananchi hawanenepi. Kwa hiyo, naiomba Wizara, pamoja na kukihamisha kitengo hiki cha manunuzi kwenda Wizara ya Fedha, wakiimarishe vizuri sana kama walivyoziimarisha sekta nyingine.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Ugavi ipo Wizara ya Miundombinu na Bodi ya Ugavi ndiyo hii ambayo inasimamia wataalam wa ugavi na ununuzi na ndiyo hawa ambao wanamiliki manunuzi ya umma kwa wingi. Ningeomba sana, Mheshimiwa Waziri, aiangalie Bodi ya Ugavi nayo. Kama amehamisha kitengo cha ununuzi kwenda Wizara ya Fedha, basi na Bodi ya Ugavi nayo ihame kutoka Wizara ya Miundombinu, iende Wizara ya Fedha ili Mdhibiti awe mmoja.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee Bohari ya Taifa. Bohari ya Taifa ipo chini ya Wizara ya Miundombinu na hiyo nayo inahusika na manunuzi. Katika Bajeti ya mwaka juzi na mwaka jana, tumejaribu kushauri kwamba, Bohari ya Serikali *(Government Stores)*, labda nayo ndiyo isimamie kununua vitu ambavyo vinafanana; kama *stationery* na magari. Inunue Bohari ya Serikali, halafu ivigawe kwa kila Wizara ili kupunguza kila Wizara kununua kitu hicho hicho ambacho kinafanana. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, Bohari ya Taifa nayo aihamishie Wizara ya Fedha, kama alivyohamisha kitengo cha ununuzi na vilevile angalie utendaji wake. Mwaka jana niliona kama Serikali ilikuwa na mchakato wa kutaka kuajiri Mtendaji Mkuu wa Bohari ya Taifa, lakini naona imefifia kimya kimya. Naomba sana, Serikali iiangalie sana Bohari ya Taifa *(Government Stores)*.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee Mamlaka ya Udhibiti *(PPRA)*. Kama nilivyosema hapo awali, kitengo cha ununuzi kilikuwa Wizara ya Miundombinu, *PPRA* ipo Wizara ya Fedha. *PPRA* ndiyo Mamlaka ya Kudhibiti Manunuzi yote ya Umma, lakini ipo chini ya Wizara ya Fedha na Wizara Fedha ni *Procuring Entity*; ni mnunuzi huyu. Sasa naona *PPRA* watakuwa na kigugumizi kumsimamia bosi wao ambaye yeye ni *procuring entity*. Inatakiwa umsimamie, lakini ndiye bosi wako! Kwa hiyo, naiomba sana Wizara, inapodurusu Sheria ya Manunuzi, ifikirie sana kuiwezesha *PPRA* iwe na uwezo wa namna fulani kwamba, isiiogope Wizara kama bosi wake, wakati inatakiwa kusimamia kama *procuring entity*.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee Sheria ya Manunuzi. Ukichukua hadithi ya mayai ya kuku na ya bata, binadamu wengi wanakula mayai ya kuku lakini ya bata hawali. Siyo kwamba ni mabaya hapana ni kwa sababu kuku anatangaza biashara yake; anapotaka kutaga anapiga kelele, akishataga anapiga kelele, lakini bata anataga kimya kimya, utaona tu ameibuka na watoto.

Mheshimiwa Spika, sasa Sheria ya Manunuzi; mwaka 2004 nilihudhuria kesi moja ya *arbitration* ya wafanyabiashara, wamewakilishwa na wanasheria maarufu. Pale imetajwa Sheria ya Manunuzi, wale wanasheria maarufu nchini, wanasheria ya manunuzi ya 2001, hii ya 2004 hawana! Nadhani kuna *problem* mahali, labda baada ya kutungwa sheria hii haikutangazwa vizuri. Kwa nini wanasheria maarufu wasiwe na Sheria hii ya Manunuzi ya mwaka 2004?

Mheshimiwa Spika, ninaweza kukwambia, inawezekana katika Wabunge wako wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, kuna wengine ambao hawaijui Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004, ambayo inawezekana hata kwenye Halmashauri zetu hii haipo. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri, Sheria ya Manunuzi ya 2004 ni ya muhimu sana; huyu anayehusika na kuitangaza, aitangaze ili wananchi wote waifahamu kwa sababu hii ndiyo inasaidia kudhibiti manunuzi katika sekta za umma zote.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee misamaha ya kodi. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, ameongea kwa kirefu sana kuhusu misamaha ya kodi, sitaki kurudia aliyoyaongea. Misamaha ya kodi ya asilimia 25 ni kiasi kikubwa sana. Kama tunasema bajeti yetu ni tegemezi kwa aslimia 34, lakini misamaha ya kodi ni aslimia 25, hiyo ni mingi mno. Naomba Wizara iangalie kwa kufuata sheria ambazo zimeweka misamaha ya kodi ili misamaha ya kodi ifikie walau asilimia 10 ili Taifa liweze kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, katika hilo, naomba ninukuu hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuhusu hiyo misamaha ya kodi kipengele fulani tu; ukurasa wa 46 amesema nanukuu: “Kurekebisha kifungu namba 10 cha jedwali la 3 ili kuyataka mashirika yanufaike na msamaha wa kodi, kuwasilisha kwa Mamlaka ya Mapato maelezo ya utekelezaji wa mipango yao ya kazi ya mwaka yakiainisha manufaa kwa jamii. Aidha, *TRA* itatoa hati ya stahili ya msamaha *(Tax Clearance Certificate),* itakayowezesha taasisi husika kuendelea kupata msamaha wa kodi.”

Mheshimiwa Spika, hili ni wazo zuri sana, lakini ninavyoliona ni kwamba hii inahusika zaidi na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Ukimpa Mamlaka ya Mapato kwamba ndiye atoe *Certificate* hiyo, ina maana aende kudhibiti na aende kukagua. Ukisema aende kukagua, utampunguzia *core business* yake ya kukusanya mapato ya Serikali kwa sababu itabidi aende akakague na adhibiti, ili aweze kutoa hiyo *Clearance Certificate*. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, labda hili la kukagua liende kwenye Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, lakini baadaye *TRA* ndiyo iweze kutoa hiyo *Certificate*.

Mheshimiwa Spika, nadhani suluhisho la kuweza kusaidia kudhibiti manunuzi ya umma ambapo hela nyingi zinapotelea huko, labda tungerudi kwa zamani. Kwa sababu zamani, nakumbuka kulikuwa na *Crown Agency,* ambao walikuwa wanafanya manunuzi kwa niaba ya Serikali, baada ya hapo ndiyo ikaja *Central Tender Board* ambayo tukaona kama ni dude kubwa mno likavunjwa, ndiyo ikaja sheria mpya ya manunuzi ambayo imeweka manunuzi katika kila Wizara, Idara na kila Halmashauri. Labda ingeundwa

*Procurement Agency,* ambayo itakuwa inanunua kwa ajili ya Serikali, inanunua *on commission* na inanunua wazi wazi ili manunuzi ya fedha za umma yawe ya wazi ili kuweza kuwanufaisha Watanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nakushukuru sana kwa niaba ya Wananchi wa Chunya, wa Jimbo la Lupa na Jimbo la Songwe, kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwambalaswa, ahsante sana kwa mchango wako. Kama nilivyotangaza, namwita sasa Mheshimiwa Mgana Msindai, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Nyawazwa, wakati huo huo Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah ajiandae.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie bajeti. Kwanza, nimpongeze Waziri wa Fedha, Naibu Mawaziri wote, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Mkuu wote, wenzetu wa *TRA* na wengine wote, waliosaidia kutengeneza bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, niipongeze sana Serikali ya Awamu ya Nne, kwa kazi nzuri inayofanya. Kwa kweli toka waingie madarakani, tunaona mabadiliko yanakuja na mabadiliko ni kwa faida ya Wananchi wa Tanzania. Wanasema Roma haikujengwa siku moja, lakini tunakokwenda kuna mwanga. Sasa hivi barabara zetu nyingi ni nzuri na zinaendelea kutengenezwa. Sasa hivi elimu yetu imepanda. Kwa mfano mwaka huu tunaanza kujenga zahanati kwenye kila kijiji. Hayo ni baadhi ya maendeleo ambayo yanakuja na sisi sote lazima tukubaliane nayo.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nasubiri kuchangia kwenye Wizara, lakini kitu kimoja kikanigusa ambacho chenyewe ni lazima nichangie hapa. Mheshimiwa Spika, mimi ni mtoto wa mkulima na mimi mwenyewe najitahidi kulima na wananchi wanalima. Tunashukuru Serikali inajitahidi kutusaidia kwenye sekta ya kilimo. Mimi nichangie ukurasa wa 45 ambao unaanza 43, inakosema sheria ya forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, na hapo nichangie kipengele cha 7.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/05 na 2005/06, tulikuwa tunavutana na Serikali juu ya mafuta ya kula yanayotoka nje. Serikali ikakubali kuweka ushuru wa aslimia 10 ili kumsaidia mkulima wa alizeti na kumsaidia mzalishaji wa mbegu zinazotengeneza mawese aweze kupata bei nzuri.

Mheshimiwa Spika, wakati huo, mafuta yalikuwa yamejaa humu ndani toka nje ya kila aina na tulikuwa tunahoji ubora wake, leo Serikali ikamsaidia mkulima wake kwa kuweka huo ushuru. Mimi nataka nipate majibu, nini kimewafanya huo ushuru uondolewe; na kwa faida ya nani? Sasa hivi wakulima wetu wamelima alizeti nyingi sana. Nenda Mikoa ya Dodoma, Singida, Shinyanga, Tabora na Manyara, kwa kweli wananachi hii hawakuipokea vizuri na tunaomba Serikali irudishe huu ushuru kwa faida ya wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, huu ushuru ukirudi, haichukui mwezi mafuta yatajaa kila mahali humu. Wananchi watabaki na mbegu zao, kwa hiyo, tunawarudisha nyuma, siyo kuwaendeleza. Kwa hiyo, naomba Serikali ilichukulie hili kama ni jambo la haraka na muhimu kwa wakulima wao, irudishe huo ushuru wa asilimia 10.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunataka wananchi wetu waendelee; wajenge nyumba bora na wasomeshe watoto wao. Mpaka sasa hatujajua bei ya saruji na bati ni shilingi ngapi? Wakulima wanasubiri na hiyo ni kitu muhimu sana ni lazima itamkwe tujue, wananchi wetu wanahangaika sana. Mabati hayashikiki, sasa hivi tunashindwa kujenga madarasa, tutashindwa kujenga hata zahanati kwa jinsi bei ya sementi na ma bati kuwa kubwa. Kwa hiyo, sisi tunaomba Serikali iangalie hili. Sasa hivi mafuta yanapanda kila siku duniani kote na bei ya chakula imepanda, tunaomba Serikali ijiandae mapema jinsi ya kukabiliana na hayo kwa faida ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo niliona nitangulie kuyazungumzia kwa sababu yanagusa wananchi wetu. Lingine, sasa nianze kuipongeza tu Serikali. Naipongeza Serikali kwa kuhamisha kitengo cha manunuzi kutoka Miundombinu kwenda Hazina. Naiomba sasa ihamishe kitengo na wale wafanyakazi wazuri, wale wabovu wote wabaki huko huko na waajiriwe wataalam wanaoiweza hii kazi ya manunuzi.

Mheshimiwa Spika, vilevile naipongeza Serikali kwa kutaka kuleta Sheria ya Serikali za Mitaa Na. 290 na Sheria ya Fedha 348 ili zifanyiwe marekebisho; Mlipaji Mkuu wa Serikali pamoja na Mhasibu Mkuu waweze kusimamia na kudhibiti matumizi ya fedha za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi si Halmashauri zote zinazotumia hela zao vizuri, Halmashauri nyingi bado zina upungufu na upungufu huu unawaletea hasara wananchi wa Halmashauri mbalimbali. Kwa hiyo, napongeza kwa hilo. Vilevile hapo hapo, bado nashauri hawa *Internal Auditors* hebu waundiwe kitu ambacho kitawasimamia. *Internal Auditors* kuwa chini ya Wakurugenzi, kwa kweli hata siku moja hawatafanya kazi yao vizuri, kwa sababu kwanza; hawana vitendea kazi na yule ndiye bosi wao, anaweza akawasurubu kiasi anachopenda, washindwe kutekeleza madaraka yao vizuri.

Kwa hiyo, tungeomba na tunaendelea kuomba, hiki kitengo cha ukaguzi wa ndani, Serikali itafute njia ili waweze kujitegemea, wawe na vitendea kazi vyao na usafiri wao, watafanya kazi nzuri kuliko sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, lingine ni juu ya kuhamisha madaraka kwa umma *(D by D)*. Naipongeza sana Serikali na ninaomba sasa Wizara hizi zilizotajwa, kuna Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Maliasili na Utalii; Nishati na Madini; Viwanda, Biashara na Masoko; na Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, kwa kweli umefika wakati hizi Wizara zirudi kwenye Halmashauri za Wilaya. Sasa hivi hizi Wizara hazina wawakilishi kule. Wizara yenye wawakilishi kule na wanakwenda vizuri na Halmashauri zetu ni Wizra ya Elimu peke yake.

Sasa tunaomba Serikali isifanyie mchezo, imeamua kurudisha madaraka kwa umma nayo ianze kujitoa, ipeleke nguvu nyingi kule Wilayani. Bado narudia, tuige wenzetu wa Uganda; Madaktari, Maprofesa, Maafisa Kilimo na Wahasibu Wakuu, wapo kwenye Kata na fedha zinakwenda moja kwa moja kwenye Kata.

Kwa hiyo, mimi naiomba Serikali izingatie hilo na vilevile iendelee kutoa. Hii *D by D* leo kuna mtu kasema kwamba, bado inaishia Wilayani, haijafika kwenye Kata na Kijiji ambako ndio lengo letu kumwendeleza mwananchi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, mimi niseme tu kwamba, bajeti hii ni nzuri na niiombe Serikali, ijitahidi kufuata matumizi bora ya fedha ilizotenga. Siyo humu kwenye vitabu ionekane fedha zipo, lakini ukienda kukagua unakuta fedha zimetumiwa vibaya.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu nitachangia kwenye Wizara, nirudie tu kuomba na kumwomba Waziri wa Fedha, ile asilimia 10 ya ushuru wa mafuta ghafi, urudi mapema.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi ili niweze kuchangia bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba tu nieleze kwamba, kabla ya utangulizi wa mambo yote ambayo nataka kuchangia, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ni ya muda wa miaka mitano kuanzia 2005 mpaka 2010.

Mheshimiwa Spika, halafu lingine, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, mapato na matumizi yanaishia mwezi Machi, 2008, naomba wananchi muelewe hivyo. Naomba tusiwapotoshe wananchi, mapato yetu na matumizi yanaishia mwezi Machi, 2008. Kwa hiyo, bado tuna miezi mitatu zaidi ambayo Mheshimiwa Waziri, atalieleza Bunge baada ya kukusanya.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee sasa na mchango wangu. Kupanga ni kuchagua; naipongeza sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, kuamua tangu mwaka jana kuweka vipaumbele. Mwaka jana, tuliweka kama tulivyoweka mwaka huu; elimu, miundombinu, afya, kilimo, nishati na maji. Mwaka huu vilevile tumeendeleza hivyo hivyo kuhakikisha kwamba, vipaumbele hivi vinatekelezeka na ushahidi tunao, barabara zinaonekana, afya ndiyo tuna mkakati huo sasa wa kila kijiji tuweke zahanati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tu wananchi wetu watuelewe kabisa, Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni sikivu, inatusikia sisi Wabunge wa CCM pamja na Wabunge wa Vyama vya Upinzani. Lengo letu ni moja kuhakikisha kwamba, tunasimamia maendeleo ya Wananchi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba basi mwaka ujao, baada ya kuangalia vipaumbele hivi sita ambavyo tumeainisha toka mwaka 2005 mpaka mwaka huu, niombe

labda mapendekezo yangu kwamba, mwaka kesho sasa 2008/09, tujaribu kuweka kipaumbele cha kwanza kiwe maji.

Mheshimiwa Spika, maji kwa kweli kuna maeneo mengi, nikitoa mfano Wilaya ya Geita tuna tatizo la maji. Kwa hiyo, nitaomba maji kwa mwaka 2009/10 tuweke maji, kilimo kifuatie na afya ambayo tutakuwa tunaendelea tu kuweka dawa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa suala la elimu na kila mtu analiona, shule zimeboreka za msingi na za Sekondari. Nitaomba sana Wananchi wa Kata ya Ngula, wametengeneza sekondari yao nzuri kabisa, maabara imekamilika, nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Elimu atakaposoma bajeti yake, anieleze ni lini atapeleka walimu wa sayansi katika Kata hiyo?

Napenda nichukue nafasi hii, kuwapongeza sana wakisimamiwa na Mbunge wa Jimbo la Sumve, Mheshimiwa Richard Ndassa, kusimamia ujenzi wa maabara Kata ya Ngula.

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa uchumi unategemea mambo mbalimbali, nitazungumzia suala moja. Mkoa wa Mwanza una Uwanja wa Ndege na katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba, kuna mfuko ambao umetolewa na Rais wa Marekani wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege.

Mheshimiwa Spika, nitaomba sana, Waziri atakapokuja kueleza mkakati wa upanuzi wa Uwanja wa Mwanza, auone una kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, nauzungumzia upanuzi wa Uwanja wa Mwanza, kwa sababu moja; Ndege nyingi zinatua *KIA*. Ukiangalia Mkoa wa Mwanza, uwanja ule ukipanuliwa, utakuwa karibu na Serengeti, Soronera, pamoja na Lubondo.

Mheshimiwa Spika, wengi hawajui kwamba kuna watalii ambao wanatakiwa waende sehemu zetu za kule Geita pale Lubondo. Kwa hiyo, tukipanua uwanja wa ndege wa Mwanza, utaukuza uchumi kwa haraka sana na wawekezaji watakuja kwa wingi sana.

Mheshimiwa Spika, nitamwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*windup***,** aje na mkakati wa namna kupanua uwanja wa ndege wa Mwanza ili na wenyewe uingie katika kukuza uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia suala la kulinda mazalio ya samaki katika Ziwa Victoria. Ziwa Victoria kuna samaki wengi sana ambao wanavuliwa pale lakini sijaona mikakati yoyote ya kuhakikisha kwamba mazalio ya samaki katika maeneo ya Kanda ya Ziwa yanahifadhiwa. Mwanza, tuna viwanda vingi sana vya samaki lakini samaki wanakwisha.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, ihakikishe inaweka mikakati ya kuwekea mazingira mazuri ya mazalia ya samaki hawa. Hivyo basi, naomba Waziri anayehusika na Wizara hiyo ambayo ni Maliasili, ahakikishe maeneo ambayo yana mazalio mazuri ya samaki yanahifadhiwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumzia suala la asilimia ambayo imepungua sana katika mambo ya uvuvi katika Bahari ya Hindi pamoja na Maziwa tuliyonayo Tanzania. Ni kwa nini imeshuka kutoka 5% hadi 4.5%.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie suala la *UKIMWI* katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, warsha, semina na makongamano, sasa imetosha. Ninalizungumzia hili kwa sababu fedha nyingi sana zimekuwa zikitumika kwa ajili ya mambo haya. Sasa ni bora tubadilishe mtazamo badala ya kufanya makongamano, watu ambao wameathirika kwa *UKIMWI,* wapelekewe lishe, madawa, pamoja na mikopo. Naomba Serikali sasa wajipange vizuri kuhakikisha kwamba fedha za *UKIMWI* zinawafikia walengwa.

Mheshimiwa Spika, Waziri ametusomea idadi ya Watanzania tunavyozidi kuwa wengi, sioni mahali popote tumeweka mikakati ya kupunguza kuzaa. Bila ya kuwa na mkakati, ingawaje labda tutamlaumu Mwenyezi Mungu lakini ni lazima tuwe na mkakati wa uzazi wa mpango.

Mheshimiwa Spika, Waziri ametueleza kwamba kufikia mwaka 2025, tutakuwa milioni 63, vitu vyote tulivyonavyo sasa hivi havitatosheleza. Ni lazima tuwe na mkakati maalumu, wananchi na Serikali tukae chini, tushirikiane kwa pamoja kulizungumzia suala hili vinginevyo jitihada zinazofanywa na Serikali, hatutaziona. Hilo ni pendekezo langu kwamba wananchi washirikishwe katika maamuzi haya ya uzazi wa mpango.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la ushirikishwaji wa wananchi katika maeneo ya uwekezaji. Katika suala la madini, wananchi wanaozunguka maeneo ya madini wamekuwa wakilalamika sana kupunjwa na kunyang'anywa maeneo. Naomba Serikali yangu, iwashirikishe wananchi katika kupanga vipaumbele katika maeneo yanayozungukwa na madini. Kama kweli tuna nia njema ya kuwasaidia Watanzania wanaozungukwa na madini hayo kwa nini basi tusiweke mikakati ya kuzungumza na wawekezaji wanaokuja katika maeneo hayo? Kwa nini wananchi wanaozunguka maeneo hayo wasikopeshwe mitambo ya kuchimba madini hayo kuliko kuwapa fedha ndogo ndogo ambazo haziwezi kuwasaidia?

Mheshimiwa Spika, naomba wananchi katika maeneo ya machimbo wapewe nafasi wao wenyewe waamue wanataka nini na wasaidiwe katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ya kilimo, pia tungeweka utaratibu mzuri zaidi kama vile kuwakopesha wananchi wa maeneo yale wanaotaka kulima, vifaa vya kufanyia kazi kama vile matreka au treka ndogo ndogo ambazo zinaweza zikawasaidia.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni maeneo yanayopitiwa na bomba la gesi. Mimi ni mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini. Tumetembelea Songosongo pale, kuna gesi nyingi sana lakini katika kupeleka gesi hiyo Dar es Salam, imepitia maeneo ambayo wananchi wamejenga katika maeneo hayo. Ndiyo maana nikaomba Serikali yetu iwashirikishe wananchi wanaoishi katika maeneo ambayo yamepitiwa na bomba la gesi, wazungumze nao na kuona kwamba wanataka maendeleo ya kitu gani.

Mheshimiwa Spika, nimesikitika sana nilipopata taarifa kwamba kuna wananchi wa Kijiji cha Bungu ambao wanatoka Wilaya ya Rufiji na bomba la gesi limepita maeneo yale, wao walikuwa wanahitaji kujengewa nyumba za bei nafuu lakini wananchi hawakushirikishwa vizuri matokeo yake wakajengewa vyoo. Inasikitisha, unapoamua kumjengea mwananchi vyoo badala ya nyumba ya bei nafuu, hii yote ni kutokana na kutomshirikisha katika kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba wawekezaji wanapokuja katika maeneo ya aina hii, basi wananchi wapewe nafasi ya kukaa nao na washirikiane katika kutoa maamuzi kwamba wao wanataka kipaumbele gani katika maeneo yao. Tutashukuru sana kama watajengewa nyumba za bei nafuu kwa mkopo, hii itakuwa ni mafanikio kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba niende katika suala la jinsia. Napenda nichukue nafasi hii, kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, juzi na katika *speech* ya Waziri, ameeleza kwamba asilimia 50 ya jinsia itazingatiwa na tarehe 12/6/2008, Mheshimiwa Rais ameapisha Majaji 11 na 7 kati yao ni Wanawake.

Mheshimiwa Spika, hatuombi upendeleo bali tunaomba usawa kwa sababu uwezo, elimu na juhudi tunazo. Kwa hiyo, suala la kusema wanawake wanaomba upendeleo, liishe. Tunaomba usawa. Kwa hiyo, bado namwomba Mheshimiwa Rais itakapofika mwaka 2010, ile azima ya kuweka asilimia sawa, itekelezeke, nami nimeona ana nia nzuri.

Mheshimiwa Spika, nimezungumzia suala la wanawake kwa sababu wanawake wanafanya kazi zote kama uvuvi, wakulima, ni wajasiriamali wazuri, kwa hiyo naomba hiyo asilimia izingatiwe.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichukue nafasi hii nzuri kabisa, kuwapongeza wenzetu wa Mamlaka ya Mapato (*TRA),* kwa kazi nzuri sana wanayotufanyia Tanzania. Ni vema Serikali yetu ilipoamua kutumia mapato yetu ya ndani, itasikisha sana, hata wewe kwenye mji wako ukitegemea kwamba uombe hela kutoka kwa jirani ndiyo ilishe watoto, ni wazi maendeleo ya familia hiyo, hayawezi kupatikana. Kwa hiyo, naomba sana *TRA,* ingawa ni kazi ngumu lakini Mwenyezi Mungu atawasaidia, tutaweza kukusanya fedha ambazo tumebajeti kwa mwaka 2008/09 ili tuweze kufanikisha malengo yetu ya kuhakikisha kwamba tunatumia fedha yetu ya ndani.

Mheshimiwa Spika, nasikitika sana tukiwa ndani ya Bunge hili, unapojaribu kusema kwamba Serikali yetu ina fedha nyingi, Serikali ya Chama cha Mapinduzi tutakusanya mapato yetu trilioni nne lakini wenzetu wa Upinzani wanasema trillioni tano, tunamuumiza nani kama si mwananchi huyu? Ninaomba tuwe na nia moja kama kweli tunataka kuwasaidia Watanzania. Bajeti ya Serikali iliyowekwa, itawasimamia Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie urasimu…

*(Hapa Kulikuwa na Minong'ono)*

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, naomba unilinde lakini ukweli ndiyo huo naona kuna minong'ono mingi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu bajeti hii haijagusa petroli, mafuta ya taa, ninaomba *EWURA, SUMATRA, TPDC,* wasimamie upandaji holela wa bei za usafiri. Serikali imeangalia suala hili ndio maana haikugusa vitu ambavyo vinamgusa moja kwa moja Mtanzania lakini kuna watu wajanja ambao watatumia nafasi hiyo itakapofika tarehe moja tu utaona *petrol*, mafuta ya taa na nauli zimepanda.

Mheshimiwa Spika, *EWURA*, *SUMATRA, TPDC,* tumewapa nguvu hapa Bungeni ya kusimamia maslahi ya Watanzania, mtusaidie sana kuhusu upandaji wa bei holela.

Mheshimiwa Spika, fedha nyingi zimeenda kwenye Halmashauri za Wilaya, ninaomba Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, atusaidie kuhakikisha hela hizi zinazopelekwa kwenye Halmashauri zetu za Wilaya zinawafikia walengwa ili zitekeleze mambo yote ambayo tumeyazingatia hapa na fedha zionekane zimetumika kama tulivyoamua sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, sitaki tena nigongewe kengele, kwa mara nyingine, naomba nikupongeze sana wewe kwa kutusimamia sisi Wabunge kwa kusema haki ili wananchi wetu watusikie na Mungu atubariki Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nichangie yaliyomo katika bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nimpongeze Waziri pamoja na Manaibu Mawaziri kwa kuweza kuwasilisha bajeti ya mwaka 2008/09. Ninaamini kila mwaka bajeti ya nchi hii inaendelea kuboreka lakini bado haitoshelezi matakwa ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, katika utangulizi wa maelezo ya Mheshimiwa Waziri katika bajeti yake, ukurasa wa nne, alisema kwamba bajeti yetu iliendelea kuwa tegemezi kwa misaada ya nje kwa kiasi kikubwa licha ya mapato ya ndani kuendelea kukua. Kwa hiyo,

changamoto ya kwanza, mwaka 2008/2009, ni kuongeza mapato ya ndani na kudhibiti kukua kwa haraka kwa bajeti ya kawaida ili tuanze kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, katika mapato, ukurasa wa 25, Mheshimiwa Waziri anasema:-

"Wigo wa kodi utapanuka kutokana na kasi ya kukua kwa uchumi hasa katika sekta ambazo zinatoa mchango mkubwa wa mapato ya Serikali. Usimamizi na udhibiti mzuri wa misamaha ya kodi pia utaongeza wigo wa kodi".

Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye lakini nianze kuchangia katika ukurasa wa 45(vii) ambacho kinasema:-

"Kuondoa ushuru wa forodha wa asilimia 10 kwenye mafuta ghafi ya kula. Mafuta yaliyosafishwa kidogo (*semi-processed*) yataendelea kutozwa ushuru wa asilimia 10. Hatua hii itaviweka viwanda vya mafuta hapa nchini katika nafasi nzuri ya kiushindani na vile vya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki".

Mheshimiwa Spika, hapa tumeponzwa na hili suala la Afrika Mashariki lakini katika mikakati ya Serikali ya kuwahimiza wakulima waendelee kulima nafaka ambazo zitawaletea maisha bora, kwa mfano Kigoma, wana michikichi, ukienda Singida wanalima alizeti na maeneo mengine mengi ambayo tunapata mafuta ya kula kutokana na mazao haya, kitendo cha Serikali kuondoa asilimia 10 na ile mikakati ya Serikali kuongeza kipato kwa wananchi, tayari tunakwenda nje ya mstari.

Mheshimiwa Spika, ukiondoa asilimia 10 ya mafuta ghafi kutoka nje, tayari umefaidisha soko la nje, umefaidisha watu wa Malyasia na umemuua mkulima anayelima alizeti, mchikichi, kuweka asilimia 10 katika *semi-processed,* umeendelea kumuua mwananchi yule. Tatizo, hivi wataalamu wetu wanaweza wakajua *semi-processed* na ambayo ni *processed* au ghafi, tunao utaalamu huo wa kutosha? Kwa sababu sasa hivi mafuta ambayo ni *semi-processed* yanapoingia hapa nchini, yanaingia moja kwa moja katika mageleni na yanauzwa madukani.

Mheshimiwa Spika, sikubaliani kabisa na ushuru huu. Ninaiomba Serikali, ushuru wa mafuta ghafi iwe ni asilimia 25 na isiwe sifuri na hii *semi-processed* pia iwe asilimia 25 ili tuue soko la nje ambalo linatuletea wafanyabiashara wadanganyifu, wanaokuja kusema uwongo na wanapitisha mafuta yao moja kwa moja katika magaloni na *process* ile inakuwa ni fupi lakini huku nyuma tumewaua wakulima wa michikichi na alizeti na yale mazao yote ambayo yanawaongezea kipato wananchi wetu. Tutaua kabisa soko la mazao haya wakati sisi huku tuna mpango wa kuhamasisha wakulima hawa wazalishe kwa wingi hatimaye viwanda vyetu hapa viweze kupata mali ghafi kwa wingi na hatimaye tupate mafuta ya kula. Kwa utaratibu huu, naona tunaua soko letu la ndani na hasa wakulima wanaolima mazao haya.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nikirudi katika kupanua wigo wa kodi na hasa tukizingatia sasa hivi mafuta ya *petrol*, *diesel* na mafuta ya taa au nishati kwa ujumla yanaendelea kupanda. Sasa hivi *barrel* moja ya mafuta, imeshafika dola 136 hadi 137. Nakuhakikishia Mheshimiwa Waziri, tutakapomaliza bajeti hii, *barrel* moja ya mafuta itafika dola 200 wala siyo Desemba.

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wangu ni kwamba hivi Serikali mta-*compensate* vipi kwa sababu hii inahitaji umakini wa uhakika kwa sababu sisi hatuna uwezo nayo, lakini mta- *subsidise* vipi? Mimi nashukuru kwamba hamkugusa mafuta lakini tukumbuke vilevile kwamba mafuta yanapanda bei na yale mafuta yatakayopanda bei katika soko wananchi bado wataendelea kuumia.

Mheshimiwa Spika, nina ushauri ufuatao; sisi tuna visima vya gesi, tuna Mnazi *Bay*, Songosongo na sasa tuna Mkuranga, tuna gesi nyingi ajabu na Serikali inajua na watalaamu wanajua, hivi tunapunguzaje mzigo kwa wananchi angalau basi mafuta ya *petrol,* ukiacha *diesel* na mafuta ya taa, tuweze kupata mafuta ya *petrol* kutokana na gesi yetu wenyewe? Mkataba wa Songas, nasema ni mbaya sana hautusaidii. Mkataba uliopo Mnazi *Bay* ule, ni mkataba halisi na mzuri, *30%* na *70%* Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika mkataba kama ule wa Msimbati Mnazi *Bay*, naishauri Serikali sasa ianze kuifanyia mkakati, gesi ile tunaifanyaje ili tupate mapato kwanza kwa Serikali na pili tuweze kupata *petrol* kutokana na gesi ile tupunguze mzigo kwa wananchi angalau *petrol* sasa, tununue *petrol* kutokana na kubadilisha gesi iwe katika utaratibu wa *liquid hydrocarbon*.

Mheshimiwa Spika, lakini utaalamu sasa hivi umethibitisha kabisa kwamba *liquid hydrocarbon,* unaweza ukaitumia katika mashine za *diesel direct* na *TPDC,* wamekwishafanya utafiti huo, wamekwenda China lakini wameomba pesa kutoka Wizara ya Fedha, hamkuwapa, sasa tunafanyaje?

Mheshimiwa Spika, nitoe takwimu katika visima vya *Mnazi Bay,* kwanza niseme ni *best contract* halafu *reserve* ya gesi iliyopo katika vile visima vilivyochimbwa ni *1.2 trilion cubic ft.,* lakini gesi iliyeko pale inatutosheleza sisi *for the next 600 years.* Hivi tuna tatizo gani sisi ya kuuza gesi ile? Wacha imalizike *100 years* lakini tuiuze na nyingine tutumie kwa manufaa yetu hapa nchini tupate *revenue* ili isaidie bajeti ya nchi hii! Gesi iko pale, imelala, hatuitumii, mimi nasema Msimbati tu wacha Songosongo, wacha Mkuranga, tunafanyaje?

Mheshimiwa Spika, pale kuna visima vinne, visima viwili vina 20 *million cubic ft.* na kingine kina 30 *million cubic ft.,* kingine kina 50 *million cubic ft.* inaweza ku-*produce per day,* hizi ninazosema ni *production per day* na inatoka pale *naturally, Compressed Natural Gas* (*CNG*), 98% *content of Methane* haina uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, leo ukimwambia M-Japan, nina gesi, atakuja mwenyewe kuichukua. Tatizo letu sasa ni kuiandaa Bandari ya Mtwara, ni *natural harbor*, bomba la

gesi limefika mpaka kwenye mitambo ya kuzalisha umeme kutoka pale mpaka bandarini, haizidi hata kilomita tatu, *capacity* ya mashine inayosafisha ile gesi, *is under utilized,* uwezo wake ni 25 *million cubic ft. per day,* inatoa 970 *thousands cubic ft*., kwa ajili ya *generator* mbili pale na *the rest* imelala pale na sisi tumeukalia ule uchumi. Mheshimiwa Waziri unataka pesa zitoke wapi wakati pesa ziko pale? Hebu waambieni hawa wataalamu watusaidie, wapeni pesa, *reseach* walishafanya lakini tatizo pengine kuna watu wengine hawataki kuiendeleza miradi hii kwa sababu hakuna maslahi kwake, hajapata 10 *percent. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tuna Kamati zetu, mbona sisi hutupati-*briefing* katika Kamati ili tukusaidie wewe, tuwatambue hawa ni akina nani, kwa kweli tunawapa mzigo wananchi bila sababu yoyote. Mimi nazungumzia gesi tu ukiacha maliasili na mengine ambayo yanaliingizia pato Taifa, nazungumzia kisima cha Msimbati tu ambacho mimi nimekwenda, nimeona na nimeuliza maswali mengi sana, kwa sababu baadhi ya maeneo mengine mikataba ni mibaya. Tumeambiwa kwamba mnawalipa *Songas* 4.8 *bilion capacity charge,* ni kwa sababu ya mikataba mibaya, hatuwezi kufika, twendeni kwenye gesi yetu ambayo mkataba wake ni mzuri.

Mheshimiwa Spika, tukii-*convert* sasa hivi gesi katika *liquid hydrocarbon,* magari yetu yatatumia gesi hiyo, magari ya *petrol, diesel* na malori yote yanayosafirisha mizigo, treni, mitambo yetu ya umeme, yote itatumia gesi hiyo kwa utaratibu wa *liquid hydrocarbon* na teknolojia hiyo *is very simple.* Tuwaambie wanaotaka kununua gesi, yetu ile ni hazina yetu ya kutosha ukiiwekea dhamana kwamba tunataka tujenge bandari kwa ajili ya kuingia zile *super tanker,* ni kupanua mita 30 ziweze kuingia Mtwara. Gesi yenyewe italipa kila kitu, viwanda vitajengwa kwa kutumia hiyo gesi, sasa mimi nashangaa wataalamu wetu wanatusaidia nini, mimi napata taabu sana na tunachekwa. Juzi ametoa *speech* Balozi wa Uingereza, ametutukana kabisa kwamba bajeti yetu sisi ni theluthi moja ya takataka zilizotupwa kwenye *dustbin* kule Uingereza, si matusi haya?

Mheshimiwa Spika, wataalamu wamenisikia na mimi naunga mkono hoja hii, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Rished, napenda niamini kwamba ajenda yako ya kudumu ya kivuko kipya cha Pangani sasa imekwisha labda kipo njiani maana umeiacha kuisema. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, nitakuwa sijamtendea haki Mheshimiwa Saddiq kwa sababu dakika zilizobaki ni dakika saba na hata angeanza ingebidi kukatiza kwa mujibu wa Kanuni. Kwa hiyo, kwa kuwa muda uliosalia hauwezi kumwezesha msemaji anayefuatia kuweza kuongea, basi nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa kumi na moja jioni.

*(Saa 06.56 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)*
*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo na namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa mtu wa kwanza katika kuchangia bajeti mchana wa leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na pongezi zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Waziri Mustafa Mkulo, Manaibu wake na timu yake yote kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya katika kutuandalia bajeti yetu. Hongereni sana. (*Makofi*)

Lakini pia nimpongeze sana ndugu yangu, kaka yangu, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, ni Mwenyekiti wangu wa Fedha na Uchumi, amewasilisha taarifa nzuri sana. Mengi aliyowasilisha, ni yale tuliyokubaliana kwenye kikao. Kwa kweli, ni matumaini yangu makubwa, maoni yaliyowasilishwa na Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Dr. Kigoda, yatafanyiwa kazi na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya mwaka huu, naweza nikasema ni bajeti nzuri, bajeti ambayo imejali zaidi wananchi wenye kipato cha kati na chini, lakini zaidi imetokana na nini tujiulize? Bajeti hii kwa maoni yangu imetokana na misingi imara ya uchumi wa Taifa ambayo ilijengwa tokeo enzi ya Awamu ya Tatu, chini ya uongozi wa Rais, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia *graph* ya pato la Taifa, ukiangalia ukuaji wa uchumi na ukiangalia jinsi mapato yalivyokuwa yanakusanywa kuanzia mwaka 1996 mpaka 2005, utajua kweli Rais wa Awamu ya Tatu na Mawaziri wake wote, walifanya kazi nzuri sana na wanastahili kupongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi ule waliotujengea, leo ndiyo Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, anauendeleza kwa kuleta matunda mazuri kwa kuweka misingi imara ya uchumi lakini kuleta maendeleo katika nchi yetu. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais Mkapa na nampongeza sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kazi kubwa waliyofanya kwa pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mazuri ni mengi na mazuri mengi ni msingi imara. Leo tunazungumzia mafanikio ya elimu lakini vile vile tunazungumzia mafanikio ya barabara katika Taifa letu. Leo tunazungumzia mkakati mzuri wa huduma ya afya katika nchi yetu kuanzia vituo vya afya, zahanati na hospitali lakini leo hospitali za Wilaya na za Mikoa zimejikomboa kwa kiasi kikubwa kwa kuwa na zana za kisasa. Lakini yote haya ni maelekezo mazuri ya Chama cha Mapinduzi chini ya Ilani ya Uchaguzi ya 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Chama chochote kile cha Siasa kinakuwa na utaratibu wake. CCM tulikuwa na Ilani yetu na Ilani yetu haikuwa Ilani ya Kisiasa kama mmoja wetu alivyosema leo. Ilani yetu ya CCM ilikuwa ni Ilani yenye malengo ya kuwasaidia

wananchi wake. Haya mazungumzo yanayoendelea, wengine hawajui mambo ya *EPA*, hawajui mambo mengine yote, wao wanachojua Serikali ya CCM inawasaidia kuwaletea maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi, mimi ni Mbunge wa Jimbo la Mvomelo, nawawakilisha wananchi wa vijijini. Huko vijijini wananchi wameelewa nini maana ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niingie katika mada yenyewe ya bajeti. Sasa hivi tumezungumzia mambo mengi lakini lipo suala ambalo leo asubuhi limezungumzwa. Kuna mwenzetu mmoja amependekeza tuondoe ushuru wa mafuta kwa shilingi 250, hivi nchi gani itakwenda bila ya kodi? Ushuru wa mafuta ni ushuru ambao unasaidia kujenga barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama mdau, naomba ni-*declare interest* yangu katika sekta ya mafuta, yapo matatizo kwenye sekta ya mafuta tunaweza tukayazungumza na yakapunguza gharama. Sasa hivi bei ya soko la dunia inapanda kila kukicha ambapo sasa pipa moja la mafuta ni dola 140, muda si mrefu litafikia dola 180 hadi dola 200. Sasa Serikali lazima iweke mikakati maalum kuhakikisha kwamba suala la upandaji wa mafuta tunaliangalia kwa macho mawili, lakini pia tunapitia na gharama ambazo zipo ndani ya sekta ya mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kampuni inayoagiza mafuta kutoka nje mbali ya kulipa kodi ya *TRA,* inalipa 1.2% kwa ajili ya *TBS,* meli inayokuja ni moja, *sample* inayochukuliwa ni moja lakini kama ni kampuni 10 basi kampuni zote 10 zinatozwa 1.25 kwa ajili ya *TBS*. Kwa nini *TBS* wasipunguze gharama ili iwe ndogo na wananchi waweze kupata nafuu katika mafuta? Hii 1.2% ni gharama kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo *TISCAN*, *SGS* wanatoza tena na wao 1.2% kwa kila mzigo wa mafuta unaokuja. Hapo hapo *EWURA,* wanachukua 6% kwa kila lita moja ya mafuta. Leo tunasema mafuta yanapanda, gharama ni kubwa. Utakuta mlolongo ni mkubwa sana toka *depot* mpaka yananifikia mwenye kituo ili niweze kumuuzia mlaji. Sasa mimi nikilalamika kwa muagizaji, muagizaji anasema angalia gharama hizi hapa. Sasa Serikali ifike mahali sasa kutokana na soko la dunia linavyokwenda, liangalie na hizi gharama za *TBS*, *TISCAN* pamoja na *EWURA*. Tunahitaji *EWURA*, tunahitaji *TBS*, tunahitaji *TISCAN* lakini ni vema wakapunguza gharama zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo kwenye mafuta, magari yetu yanaharibika kwa ajili ya wafanyabiashara wachache wenye uchu wa kutaka kutajirika, wanachanganya na mafuta ya taa. Mafuta ya taa, Serikali kwa nia njema kabisa imeweka kodi ya chini na sasa hivi utakuta kutoka Kibaha kuja Chalinze vituo vya mafuta vinavyojengwa na ma-*godown* yanayojengwa nyuma, ile yote ni dalili ya kuchanganya mafuta, magari yanaharibika lakini Serikali haijachukua hatua yoyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili tumelizungumzia Bunge la mwaka jana, *EWURA* wako hapa walifanyie kazi hilo. Unapojenga kituo cha mafuta na *godown* nyuma, la nini kama siyo kufanya chakachua? Serikali inapoteza mamilioni ya kodi, sisi wengine tunapata hasara, tunaweza tukalipishwa faini kwa sababu labda Dereva alicheza, lakini Dereva anapata ushawishi, tunabadilisha Madereva kila siku kwa sababu Madereva wengine siyo waaminifu, tatizo Serikali *TRA* yenyewe, *EWURA* na Polisi haijawa makini, eneo ni dogo, Kibaha - Chalinze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, muda unakwenda kweli kweli, naomba niende haraka, sasa niingie kwenye eneo ambalo linakugusa wewe Naibu Spika, mimi Mvomelo, Mheshimiwa Waziri Mkuu Mizengo Pinda kule Mpanda, Sumve kwa Mheshimiwa Richard Ndassa, wote tunawategemea Madiwani, sisi tuko Bungeni Madiwani wanatusaidia. Naomba kutoa hoja Serikali iangalie ni namna gani itaongeza posho ya Madiwani. Madiwani ndio wasaidizi wakubwa wa Wabunge, leo Madiwani hawana hata vyombo vya usafiri. Serikali ifanye kila iwezalo Madiwani wakopeshwe pikipiki, Madiwani waongezewe posho, Madiwani ndiyo wasaidizi wakubwa wa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi Jimbo langu lina Kata 17. Kuna Kata moja ina vijiji tisa, ni Kata ya Mvomelo, Diwani wake ni Sosa, anatembea zaidi ya masaa nane kumaliza Kata moja. Hivi bila ya kumwezesha, ataweza kutoa huduma? Naomba Madiwani watazamwe kwa jicho la huruma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niingie kwenye barabara. Barabara ni sehemu kubwa ya uchumi. Katika Ilani yetu ya CCM kulikuwa na ahadi ya kujenga barabara ya Korogwe-Handeni-Turiani-Mvomelo-Mikumi. Naomba Serikali sasa kwa makusudi kabisa ikumbuke kwamba hii ni ahadi yake na naomba sasa maelekezo rasmi yatolewe ili mikakati ya kuanza ujenzi wa barabara hii ianze mapema. Ni ilani yetu, wananchi tumewaahidi, wakati muafaka umefika, sasa uchumi unakua, bajeti siyo tegemezi sana, bajeti inategemea zaidi pato letu la ndani, barabara ziweze kutengenezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizungumzia uchumi, uzungumzie na bandari, bandari ya Dar es Salaam msongamano ni mkubwa lakini Bandari ya Tanga ni kiungo kikubwa cha barabara hii ya Handeni lakini Bandari ya Tanga itakuwa haina faida iwapo bandari ile itakuwa haikutengenezwa au kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kuna mkakati wa kuweka lami Tanga-Horohoro. Barabara ile ikiwekwa lami Kenya itafaidika, Tanzania haitafaidika bila kujenga Bandari ya Tanga. Ukitaka tufaidike na barabara ya Tanga – Horohoro kwa ajili ya lami hiyo, tujenge kwanza bandari ya Tanga. Tukijenga bandari ya Tanga tunafungua na milango mingine ikiwemo barabara ya Turiani - Handeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye umeme, umeme ni tatizo. Wananchi vijijini wanalalamika, yapo maeneo, nguzo tatu, umeme umefika na watu wamepata huduma. Bajeti ya kupeleka umeme vijijini, naomba Serikali iangalie tena na tena. Tunalia na umeme kila siku kwamba ni huduma muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Mvomelo, kuna mradi mkubwa wa umeme katika Tarafa ya Mgeta. Mradi umeanza miaka miwili iliyopita mpaka leo haujakamilika. Naomba Wizara husika sasa ikiwezekana waje watembelee, waone ni fedha kiasi gani zimetumika, ngapi zinahitajika ili mradi ule ukamilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi kama hiyo, iko mingi ambayo haijakamilika, hata kule Malya – Sumve kuna mradi haujakamilika, naomba Serikali ituangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niingie kwenye kilimo kwa haraka sana. Bajeti yetu ya kilimo siyo kubwa sana lakini bajeti yetu ya kilimo itakuwa nzuri zaidi ikiwa sisi wenyewe tutakuwa tumeamua kabisa kuifanyia kazi. Mwaka 2004, tuliweka Sheria ambayo iliunda *income tax*, tukapitisha *capital allowance* katika sekta mbalimbali, sekta ya kilimo, sekta ya utalii, sekta za uzalishaji lakini leo Waziri anakuja na hoja ya kusema kwamba wako watu ambao watalipwa fedha katika maeneo ambayo watapata hasara lakini katika maeneo hayo, hapo sasa, kama kilimo kitaingia, maana yake tunaua kilimo. Wenzangu nafikiri watanielewa zaidi, wataalamu katika eneo hilo kwa kuwa ni muda mfupi siwezi kuzungumza kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba sana nizungumzia suala la *TRA*. *TRA* wenzetu wanafanya kazi nzuri sana na wanastahili kupongezwa lakini kuna upungufu katika *TRA,* ni vema basi wakaujua. Sasa hivi walipa kodi wakubwa wote katika nchi nzima faili zao zimehamishiwa Dar es Salaam, viwanda viko Morogoro, viwanda viko Mwanza, Arusha, uzalishaji kule unasimamiwa na nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, naona kengele ya pili imelia, nasema naunga mkono hoja na naipongeza Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu, kwa kazi nzuri ya juzi. *(Makofi)*

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii kwa jioni ya leo ili na mimi nichangie machache kuhusu bajeti iliyowasilishwa wiki iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, lazima nimshukuru Waziri kwa hotuba nzuri pamoja na Manaibu Waziri wake wote wawili pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi ambao walitoa mchango mzuri katika Kamati ya Fedha na Uchumi nikiwa na mimi Mjumbe wa Kamati hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile namshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa taarifa yake nzuri aliyotoa leo asubuhi ambayo ina takwimu nzuri za kuisaidia Serikali jinsi ya kuhakikisha kuwa bajeti imeboreshwa na inafanya kazi nzuri kwa wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Serikali ya *SMZ* na Serikali ya Muungano, zina nia nzuri tu ya kuhakikisha kuwa uhusiano wa nchi mbili hizi unakuwa mzuri. Nia

hii nzuri ambayo imejengeka kwa muda mrefu na tunaiendeleza lakini bado matatizo madogo madogo yanajitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli upo kutokana na maneno ya Baba wa Taifa aliyosema:-

"Njia ya jehanamu imejaa tele nia njema".

Kwa kweli Serikali zetu zina nia njema lakini zimeelekea katika jehanamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika hotuba hizi mbili, hotuba ya mwaka jana ambayo ilisomwa na Mheshimiwa Zakia Meghji, Bungeni hapa kipindi kilichopita na hotuba hii iliyosomwa na Mheshimiwa Mustafa Mkulo, wiki iliyopita kuhusu Tume ya Pamoja ya Fedha, ukweli uliopo ni kwamba Tume ya Fedha ya Pamoja ni Tume iliyoundwa Kikatiba lakini bado haijafanya kazi ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili kama hatujaliangalia, malalamiko na manung'uniko na kero kwa wananchi wa pande hizi mbili zitakuwepo. Lazima tuhakikishe kuwa Tume hii inafanya kazi ipasavyo. Tume hii kwa taarifa ya Tume ya Mheshimiwa William Shellukindo, ina matatizo yake na changamoto nyingi sana ambazo zinaikabili. Mojawapo ya changamoto ambayo imesemwa katika taarifa ile ambacho ni kikwazo kikubwa, ni kuwa watendaji na baadhi ya wakuu wa Serikali hizi mbili hawajazifahamu vizuri taarifa ambazo zinatolewa na Tume katika kuhakikisha kuwa hizi kero zilizopo zinapatiwa ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama suala hili lipo kwa watendaji na wakuu wa Serikali, kwa hiyo, ni kikwazo kikubwa. Tutakaa hapa siku zote kulizungumzia suala hili kuwa Tume haifanyi kazi lakini kikwazo kwa watendaji na baadhi ya wakuu hawajaamua hasa nini kiamuliwe kuhusu Tume hii. Kwa hiyo, itakuwa ni tatizo kubwa sana, kila siku tutaleta taarifa Tume ya Fedha, ataleta Mheshimiwa huyu, Mheshimiwa mwingine, Mheshimiwa Mustafa Mkulo akiwepo mwaka kesho ataleta tena hivi hivi lakini uchanganuzi na mfumo mzima wa kuhakikisha kuwa Tume hii inafanya kazi na zile kero zinaondoka bado haujapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nashauri kuwa lazima tuwe wakweli na tuwe waangalifu katika suala hili, tuhakikishe kuwa tunalipatia ufumbuzi mara moja ili wananchi wa pande hizi mbili wasisumbuke na zile kero ambazo zipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala la misamaha ya kodi. Suala hili ukilizungumzia kwa upande wa Zanzibar, upande wangu mimi naona ni aibu kubwa kweli kweli, nchi ambayo kwa kweli msamaha wa kodi unafika kile kiwango ambacho kinakusanywa, ni kitendo ambacho kwa kweli kinasikitisha na kinatia aibu kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ipo haja kama utaratibu mzuri upo kuhakikisha sheria zetu kama bado zina upungufu tuziangalie, kama sera zetu zina upungufu tuziangalie, kama utendaji wetu una upungufu tuangalie. Lakini bado asilimia 96 ya mapato inakwenda katika misamaha ya kodi, hiki ni kichekesho kikubwa kweli kweli yaani wema unapita uwezo wa yule ambaye anatoa, huu ni msemo wa Kiswahili. Kwa hiyo, ni kitu ambacho kwa kweli lazima tukiangalie. Suala la misamaha ya kodi tulingalie vizuri zaidi na tuhakikishe kuwa wale ambao wanasamehewa kodi wawe ni watu muhimu sana. Pia hii kodi inayosamehewa iwe inaleta faida kwa wananchi wa Zanzibar. Kama haileti faida, kwa kweli haina haja ya kusamehe kodi kwa kiwango cha namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nilitaka kulizungumzia ni kuhusu asilimia 4.5 ya misamaha ambayo inatoka sehemu tofauti ambayo Tanzania inapata. Ni kitu ambacho kwa kweli kama ile Tume ingekuwa inafanya kazi vizuri hii 4.5% ingekuwa haina malalamiko wala haina matatizo lakini bado katika ile Tume haijachunguza vizuri zaidi na haijafanya kazi kuhakikisha kuwa 4.5% inaangaliwa na inaongezwa ili kuhakikisha kuwa inaweza ikasaidia na kuondoa malalamiko na manung'uniko yaliyoko. Tume ihakikishe kuwa inafanya kazi vizuri na mwananchi wa Zanzibar hawi na malalamiko kuwa Serikali ya Muungano wanachukua kiasi kikubwa kuliko Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Tume ingekuwa na mkusanyiko mzuri au mchanganyiko mzuri wa mawazo ili kuhakikisha tunaweza tukaboresha hii asilimia 4.5, basi ingekuwa ni busara na hii ni ili kuhakikisha kuwa inafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu Benki Kuu ya Tanzania. Kwa kweli Benki Kuu ya Tanzania, ni taasisi ambayo kwa kweli inasimamia vizuri tu sera ya fedha, inasimamia vyombo vya fedha na inatoa ushauri wa hali ya uchumi wa nchi tuliyonayo. Katika tathmini ya uhakika ambayo imefanywa katika mabenki yetu ya Tanzania, kuna baadhi ya mabenki yanafanya vizuri sana. Mpaka tarehe 30/8, kuna baadhi ya mabenki yamefanya kazi nzuri ya kuhakikisha kuwa benki zetu zinafanya kazi vizuri. Kwa mfano, *NMB*, amana zake zilizopo ni bilioni 1550.96, hiyo ni benki ya mwanzo ambayo inafanya vizuri. Benki ya pili, *CRDB,* bilioni 1019.36, benki ya tatu *NBC* bilioni 880.55 yaani benki hizi kwa kweli zinafanya kazi vizuri sana lakini suala la kujiuliza ni hili kuwa baadhi ya hizi Benki Zanzibar bado hazijafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili tunaliulizia mara nyingi sana. Kwa nini *CRDB* na *NMB* hazifika Zanzibar? Ni suala ambalo kwa kweli lazima lishughulikiwe kikamilifu. Kwa sababu mazingira yaliyoko Zanzibar na mazingira yaliyoko benki nyingine, ni sawa sawa. Kwa nini benki hizi hazijahakikisha kuwa zinafika katika eneo lingine la Muungano na kuhakikisha kuwa linatoa misaada na mikopo iliyopo kama inavyotoa katika upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu *TASAF*. Mfuko wa *TASAF* unafanya vizuri sana Tanzania na kwa kweli ni wa mfano na wapongezwe sana kwa juhudi ambazo wanachukua za kuhakikisha kuwa wananchi wetu

wanapata ajira ndogo ndogo na wanaondokana na hali ngumu ya umaskini. Tatizo lililopo hivi sasa kuhusu suala hili na linapigiwa kelele sana ni kuhusu asilimia 20, imekuwa ni kubwa na mzigo kwa wananchi wa Tanzania. Kama ipo haja na kama kuna uwezekano tupunguze ile asilimia angalau ifike 15 au 10 kwa sababu ni mzigo ambao wananchi wanabeba.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu bajeti ambayo inawekwa katika *TASAF* ni bajeti ambayo haibadiliki, inamuumiza mwananchi, hata kama unatokea mfumko wa bei lakini bado *TASAF* inashikilia pale pale kwa fedha iliyoitoa kwa mradi. Kwa hiyo, hili ni tatizo ambalo lipo na tuhakikishe kuwa tunaliondoa. Tuhakikishe kuwa kama mfumko wa bei unatokea, vile vifaa vinavyoongezeka, vinakidhi haja lakini kwa kumbebesha mwananchi ule mzigo wa ongezeko la bei kwa kweli ni jambo ambalo ni hatari na hawawezi kulibeba.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu *SEZ (Special Economic Zone)* iliyopo Mabibo. Suala hili kwa kweli ukilifuatilia ni zuri, ni uwekezaji mzuri na unaweza ukaleta ajira nyingi sana kwa wananchi wetu wa Tanzania. Lengo ni kwamba hadi kufikia mwaka 2020 tuwe tumeshatengeneza ajira zisizopungua milioni mbili mpaka tatu. Lakini Tanzania hivi tulivyo, tulivyokuwa hatuna uharaka wa hili suala, bado mpaka leo tupo katika *zone* moja tu ambayo iko Mabibo ambayo tunatarajia mpaka kufikia mwaka 2020 tuwe tumeshatengeneza *SEZ* kama zile zisizopungua 25 kwa kila Mkoa, itakuwa ngumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kushangaza na kusitikisha hata hiyo *zone* moja iliyopo ya Mabibo ina vikwazo na matatizo mengi. Kwanza Serikali ihakikishe kuwa fedha ambazo wanatengea ukanda ule inakuwa ni nzuri na inafika kwa wakati katika *SEZ* hiyo iliyopo pale Mabibo kwa sababu haifiki kwa wakati. Hii inasababisha ile miradi iliyopangwa kutekelezwa haikamiliki wala haiwi na ufanisi kwa sababu bajeti inayokwenda pale haikidhi haja ya kutekeleza lengo lililokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna baadhi ya wananchi ambao wanazunguka eneo lile la Mabibo bado hawajafidiwa. Serikali inadai haina fedha lakini kwa usalama, lile eneo lazima wananchi wale wafidiwe na wahakikishe kuwa wanaondoka lakini bado Serikali haijatoa fedha za kuhakikisha kuwa wananchi wale wanaondoka ili eneo lile linapatikana ili kufanya kazi ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali isiwe na kigugumizi, wawekezaji kama 50 hivi wamekwishapeleka maombi yao, wanataka kufanya kazi au waanze kufanya kazi katika eneo lile lakini bado Serikali haijaamua kuwa wawekezaji wale waanze kazi. Lile eneo tayari kwa kweli kuna sehemu nyingine imeshakamilika kama linaweza likaanza kazi mara moja basi ianze. Kwa hiyo, tunashauri kama kuna uwezekano wale walioomba wapewe zile nafasi wahakikishe kuwa wanaanza kuwekeza katika eneo lile lililokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu uvuvi. Katika uvuvi, kama alivyosema katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri, kuwa inachangia asilimia 1.6 ya pato la Taifa, ni kuhakikisha kuwa uvuvi tulionao hivi sasa unakidhi haja. Kwa kweli uvuvi tuliona nao sasa hivi siyo uvuvi wa kukidhi haja au wa kuongeza pato. Ukiangalia bahari tuliyonayo na maziwa tuliyonayo ambayo yanatoa samaki ni mengi sana lakini cha kushangaza uvuvi uliopo hapa, zana ambazo zinatumika ni duni, hazimsaidii mwananchi wa kawaida. Kwa hiyo, ipo haja kwanza kufanya utafiti wa samaki wote ambao wanapatikana nchini ili kuona je, wanakidhi haja ili tuweze kuwasafirisha nje au tunaweza tukawatumia katika soko la ndani? Kwa hiyo, lazima tuwasaidie wananchi kuhakikisha tunaboresha suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine la muhimu ambalo lazima tuliboreshe ni kuhakikisha kuwa wavuvi wetu wanapewa zana za kisasa. Tuachane na zile zama za kusafiri na nguo za kitambaa ndiyo wanakwenda kuvua. Hilo kwa kweli siyo suala ambalo kwa kweli tunaweza kumsaidia mwananchi. Lazima tupate chombo ambacho kinaweza kikafika bahari kuu, anaweza akavua na anaweza akapata kipato cha uhakika kuwa anaweza kujisaidia yeye na nchi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu soko. Tuwe na masoko ya uhakika kwa baadhi ya vitu ambavyo vinapatikana baharini, kwa mfano, mwani na *shells* zinapatikana katika bahari lakini hazina soko maalumu. Tuhakikishe kuwa wananchi wetu wanapata masoko ya kuuza bidhaa zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo tunashauri ni zile zana za uvuvi ziwekwe hapa nchini, mwananchi akitaka awe anaweza kuzipata na kuzitumia. Kwa hiyo, zana zote za uvuvi hapa nchi hazipo, kwa kweli hili ni tatizo. Kwa hiyo, tunaomba zile zana za uvuvi ziletwe hapa nchini ili mwananchi anapoamua kwenda kununua basi aweze kuinunua kwa wakati muafaka ambapo anaweza kufanya kazi ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache, nina hakika hotuba yangu imeeleweka na kabla sijamalizia, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niungane na wenzangu, kwanza kukiri kwamba naunga mkono hotuba hii ya bajeti. Napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkulo, kwamba kwa namna ya pekee amewasilisha bajeti hii ambayo kweli imeleta matumaini. Kumekuwa na bajeti za kila aina, zingine bajeti za walala hoi, bajeti tulivu na zingine zimepewa majina ya kila aina lakini yeye safari hii bajeti yake haikupata jina lolote lile, isipokuwa Watanzania wenyewe ndiyo tumeweza kuipa jina kwamba ni bajeti inayomfaa Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya mwaka huu imeweza kuweka walau mfumo ambao unaonyesha kwamba tunaanza kutoka kwenye hatua moja kwenda hatua ya pili. Bajeti hii ukiangalia ameweza kuianisha vizuri sana mambo mbalimbali. Bajeti kama tatu za nyuma zilizopita ukilinganisha na hii utaona hii kwa kweli imefanyiwa kazi ya

ziada. Napenda nikupongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na wenzako ambao wameandaa bajeti hii vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii bila kuwasifia, *TRA* kwa kweli wanastahili kupongezwa kwa kazi nzuri. Napenda kuchukua nafasi hii kwanza nimpongeze sana Kamishna Mkuu, Bwana H. Kitilya. Kwa kweli *TRA, this is a job well done.* Kila mwaka tunawapa malengo lakini wanayafikia na kuyavuka. Hii kwa kweli inaonyesha chombo hiki kimekuwa ni chombo imara sana. Nampongeza Ndugu Kitilya pamoja na Mwenyekiti wa Bodi hii na watumishi wote wa *TRA* kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo sio kupata, tatizo ni kutumia na hapo sasa ndiyo tunasema kwamba kupitia bajeti hii, Mheshimiwa Waziri atusaidie, ni lazima tuweke mfumo mzuri wa matumizi. Kwa sababu hata ungejaza maji kwenye pipa, kama pipa linavuja basi haliwezi kujaa maji. Tumekuwa na hadithi nyingi huku nyuma za fedha za Serikali kutumika visivyo na nyingine zikaingia kwenye lugha ya ufisadi, kupitia bajeti hii, naomba neno ufisadi tulisahau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tunahitaji kweli sasa tufunge mikanda ili maendeleo yanayotokana na bajeti hii yamnufaishe Mtanzania. *We need to have a trickle down effect* kwenye bajeti hii. Uchumi huu ambao unakuwa sasa hivi lazima utafsiriwe kwa hali halisi ya maisha ya Watanzania. Leo hii unakwenda kijijini, mimi niliulizwa na mpiga kura wangu mmoja, akiwa na umri wa miaka 95, akasema mimi nimekaa katika dunia hii, nimeshuhudia utawala wa mkoloni, utawala wa Baba wa Taifa, Nyerere, nimeshuhudia utawala wa Mwinyi, utawala wa Mkapa na huu utawala wa sasa lakini katika maisha yangu, sijaona chumvi inapanda bei kutoka shilingi 50 mpaka 250 ndani ya miaka miwili. Sasa hiyo ilikuwa ni changamoto, kuonyesha kwamba maisha ya kawaida ya mwananchi yanaguswa sana na ukali wa maisha au kutokuwa na utengemavu wa uchumi katika nchi yetu. Sasa naomba takwimu hizi za kukua kwa uchumi tuzitafsiri vizuri ziendane na uhalisia wa maisha ya Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu hii, ni nchi tajiri sana lakini nadhani tuna ka-ugonjwa kadogo kakutokutambua hilo kwamba sisi ni matajiri, isipokuwa kusema sisi ni maskini. Tuna kila sababu ya kujivunia, katika ukanda wa Afrika, ni nchi inayoongoza kwa kuwa na rasilimali nyingi kuliko nchi zingine lakini hatujaweka mfumo sahihi wa kuweza kuzalisha mapato ya kutosha na kuyatumia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa najaribu kuangalia katika miaka iliyopita kama miwili, mitatu hivi, fedha ambazo zimekuwa zikifujwa, kutoka kwenye ripoti ya Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali, ni fedha nyingi sana. Sasa hii yote, kama tutakuwa makini katika kutumia pesa hii, nina imani maisha ya Watanzania yatabadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania tuna kama ka-ugonjwa kidogo. Kwa sababu akija mwekezaji Mzungu, hata amekuja na *briefcase,* tuko tayari kumpigia magoti na kumpa kila aina ya msaada na hata ukiangalia misamaha mingi ya kodi hii, ni kwa wawekezaji wanaosema ni wawekezaji wakubwa lakini hawa watu wanakuja na *capital*

kiasi gani? Wengine wanakuja na *briefcase* baada ya siku mbili, tatu anapata mtaji hapa hapa, anazalisha hapa hapa, anatengeneza faida yake hapa, anapeleka nje ya nchi, sisi Watanzania tunabaki pale pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kitu kingine Watanzania tumejawa na roho ya korosho kwa sababu ukiona Mtanzania anaendelea, unataka tumteremshe. Tutasema huyu namna gani, unajaribu, atafika tu huyu, hatupendi kuona mafanikio ya Mtanzania mwenzetu, tunapenda kuthamini mafanikio ya mgeni anayetoka nje, badala ya Mtanzania. Kwa hiyo, naomba Watanzania wenzangu tujaribu kubadilika katika mtazamo wa namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu inahitaji kuweka miundombonu iliyo sahihi kwa kufanya hivyo, naamini kabisa uchumi wetu utakuwa kwa haraka sana. Leo hii ukiamua kwamba sasa barabara za Mtanzania za msingi, kama *Central Corridor, Mtwara Corridor, Northern Corridor,* zikifunguliwa vizuri, uchumi wa nchi hii utapaa kama ndege iliyokuwa inasemwa inapaa lakini bila kufanya hivyo, haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii mwananchi anayekaa kwa mfano Mwanza, anachukua bidhaa kutoka Dar es Salaam, bidhaa zimepanda sana lakini *factor* kubwa pale ni ya usafirishaji pamoja na uzalishaji kwa sababu gharama ya kuzalisha bidhaa hapa nchini ni kubwa sana lakini bado gharama ya kusafirisha vile vile ni kubwa sana. Kwa hiyo, nadhani cha msingi tujaribu kuhakikisha kwamba bajeti yetu hii inatoka kwenye utegemezi, ni wazo zuri sana na naiunga mkono na nampongeza Mheshimiwa Waziri kwamba sasa bajeti yetu kwa matumizi yetu ya kawaida ya ndani tunaizalisha sisi wenyewe, *this is very good*, lakini ile bajeti ya maendeleo kuiacha kwamba tupate fedha kutoka kwa wahisani, hii mimi natia shaka sana. Nadhani ni bora tukaanzisha mfumo rasmi wa kuweka maendeleo yetu kwa kutumia pengine mikopo ya muda mrefu zaidi, badala ya kutegemea fedha ambazo wahisani wanaahidi lakini wakati mwingine haziji matokeo yake tunakuwa na takwimu kwenye vitabu ambazo hazitekelezeki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina wasiwasi sana na barabara ya kutoka Mwigumbi-Shinyanga kuja Bariadi kwenda Ramadi ambayo imepitia katika Jimbo la Busega kama itajengwa. Tuliahidiwa kwamba itajengwa mwaka 2009 lakini mpaka leo maandalizi sioni. Sasa naomba nitoe changamoto kwa Waziri mhusika kwamba kwenye miradi kama hii, ni lazima tuiangalie kwa sababu mimi inanigusa na inagusa uchumi wa wananchi wa maeneo ya Mkoa wa Shinyanga, Mwanza na Mkoa wa Mara. Kwa hiyo, naomba niseme kwamba ni vema tujaribu kuangalia sana suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufufua uchumi wa nchi yoyote, miundombinu kama umeme, ni muhimu sana kuzingatiwa. Kwa kweli leo hii tunasema kwamba tunaharibu mazingira kwa sababu ya kukata miti na kadhalika lakini yote haya ni kutokana na kutokuwa na mfumo mzuri wa kuzalisha nishati ambayo ni nafuu ili kila Mtanzania aweze kuimudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii inasema mishahara juu, minono, lakini na kodi imepanda. Sasa sijui kama mfanyakazi wa kawaida ataona ile *wage differencial,* ni kubwa kwake kwa sababu ukiangalia mfumko wa bei unazidi kupanda, unakua kwa kasi sana, bado na uchumi na wenyewe hauendani na mfumuko wa bei, mwananchi unasema unamwongezea mshahara kwa kima cha chini cha shilingi laki moja, bado haujamsaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kuna haja ya kujaribu kutafsiri maisha ya Mtanzania kwa gharama halisi ya kuishi, tusiishi kwa nadharia. Haiwezekani Mtanzania umwambie shilingi laki moja hiyo sasa wewe na mke wako na watoto wako wanne ule hiyo hiyo, ujitibu hiyo hiyo na usomeshe watoto wako, huyo mtu utamfanya ashindwe kumudu maisha. Kwa hiyo, kuna haja katika bajeti zijazo, Mheshimiwa Waziri ajaribu kuangalia mfumo halisi wa kutambua gharama ya mtumishi katika Serikali hii na kwenye nchi hii ambayo itamwezesha kuwa na *liveable income.*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la misamaha ya kodi. Misamaha ya kodi, nashukuru kwamba kupitia bajeti hii, Serikali imejaribu kuainisha misamaha hii ili iweze kurekebishwa. Mimi nafikiri ni mfumo mzuri sana na kwa kweli ningeomba wawekezaji hawa wakubwa wakubwa tujaribu sana kuwabana wachangie kodi ya kutosha katika nchi hii kwa sababu *tax base* yetu bado siyo kubwa sana. Uchumi unabadilika, ndiyo, walipa kodi wanaongezeka, bado *informal sector* ambayo ni kama asilimia 30, hatujaipata vizuri. Hawa watu ukiangalia uzalishaji wao yanakuwa *determined* na miradi yao, sasa kuchangia kwao katika pato la Taifa lazima tuangalie sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kilimo, wenzetu wa Kenya bajeti ya kilimo, wametenga shilingi trilioni 15, bajeti ya kilimo peke yake, trilioni 15. Sasa sisi hapa bajeti ya nchi nzima ni trilioni 7.2. Sasa ukiangalia Kenya hawana ardhi kama ya kwetu. Kwa hiyo, kuna haja ya kuwa *very strategic* kupanua kilimo na kumsaidia mkulima. Kilimo ndiyo kinachowaajiri Watanzania wengi zaidi lakini leo hii maisha ya mkulima wa kawaida hayajabadilika. Nikimwuliza Waziri wa Kilimo kwa miaka miwili umefanya nini kwa mkulima wa kawaida kijijini, hawezi kujibu. Sanasana atasema nimewapelekea pengine ruzuku ya mbolea na wengine hawajafanya chochote kile lakini huyu mkulima tunataka azalishe, atoke kuzalisha kwa jembe la mkono, azalishe kwa nyenzo ambazo zitamfanya awe *more productive.* Katika bajeti hii tumetenga fedha kidogo kwenye bajeti ya kilimo, kwa kweli ni *very unfair.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hii pesa nyingine ambayo tunasema haionekani, kuna pesa inayokuja *indirect* nyingine huku, inaleta *confusion.* Nadhani katika bajeti ijayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ninaomba fedha yote ambayo tunadhani kwamba itakuja kwenye bajeti ni vema tuka-*identify* kwa sababu matokeo yake tunasema tuna miradi hii, tutaitekeleza lakini mwisho tunashindwa kuitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii lazima tuisimamie. Leo hii tumeweka nguvu kubwa sana kwa Halmashauri zetu lakini Madiwani tunawasaidiaje wao kusimamia bajeti zetu hizi? Mimi naomba kwamba tuweke utaratibu wa makusudi wa kuwasaidia Madiwani ili na wenyewe waweze kuwa *more effective* katika kusimamia bajeti.

Hatuwezi kupeleka rasilimali kubwa kwenye Halmashauri wakati Diwani huyo huyo hutumwezeshi kikamilifu kuweza kusimamia bajeti. Nashukuru katika bajeti hii kumekuwa na hilo wazo na kuna mtazamo huo. Naomba tuongezee nguvu zaidi na hasa kwa kuona kwamba sasa Watendaji wetu na hasa Madiwani ambao wanafanya kazi kubwa sana na wenyewe wanawezeshwa kinamna ya pekee katika kusimamia bajeti zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natoka katika ukanda wa Ziwa ambako tuna masuala ya uvuvi. Wavuvi, wavuvi, wavuvi, naona katika bajeti hii hawajasaidiwa sana. Naomba kwa kweli tujaribu kuboresha suala zima la uvuvi katika maziwa yetu na hata katika bahari zetu kwa sababu nchi zingine zinapata mapato mengi sana kutokana na maliasili inayotokana na uvuvi. Sisi tuna fursa hiyo, naomba tuitumie kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema machache haya, naomba nirudie kusema kwamba naunga mkono bajeti hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kupata nafasi ili niweze kuchangia bajeti yetu ya Serikali ambayo iliwasilishwa na Waziri wa Fedha wiki iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwanza kama walivyoanza wenzangu kuipongeza sana Wizara ya Fedha kwa maana ya Waziri, Manaibu wake na Wataalamu wake kwa kazi kubwa sana ambayo wamefanya katika kuandaa bajeti hii ambayo kwa hakika Watanzania wengi wameiona kwamba ni bajeti nzuri. Mimi huwa nawaambia wenzangu kwamba tusitegemee miujiza katika bajeti zetu za nchi maskini, hapa ndipo tulipofika na ndiyo tumejitahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba nichangie machache kwenye bajeti hii. Nianze kwanza na Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi. Tulipokuwa tunajinadi sisi, tulitumia Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwamba tutaekeleza haya ambayo tuliyanadi kwa wananchi wetu. Jambo kubwa ambalo tulilisema sana kwa wananchi wetu na ambalo tumeliandika kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ni kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma ukurasa wa 22 wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kwa ruhusa yako naomba ninukuu, Sura ya Tatu, Sekta za Uzalishaji, inasema:-

*“Kilimo cha kisasa ndiyo msingi wa uchumi wa kisasa”.*

Ibara ya 30 inasema:-

*“Kilimo ndiyo msingi wa uchumi wetu na kina nafasi ya kimkakati katika modernization ya uchumi wa Tanzania. Kilimo cha kisasa ni sharti muhimu katika kujenga msingi wa uchumi wa kisasa”.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ukiendelea kwenye Ibara ya 31 inasema:-

*"Ili uchumi wa nchi yoyote ukue kwa kiwango cha asilimia 10 ifikapo mwaka 2010 lazima kilimo kifikie ukuaji wa angalau asilimia 20, ifikapo mwaka huo, kwa lengo la kufikia kiwango hicho cha ukuaji ifikapo mwaka 2010".*

Kumeorodheshwa hatua ambazo CCM itachukua, naomba niseme hatua chache tu. Ya kwanza:-

*"Mbegu bora, mbolea ni pembejeo zenye umuhimu wa kwanza katika mageuzi ya kilimo na kuongeza tija. CCM katika kipindi cha Ilani hii, itaitaka Serikali kuchukua hatua za dhati kuweka utaratibu wenye uhakika wa upatikanaji wa mbegu bora na mbolea na kuzifikisha waliko wakulima kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa, Vyama vya Ushirika na watu binafsi na kadhalika".*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo muhimu ambalo naomba liwe la mwisho kwenye Ilani hii kuisemea, ni kifungu kidogo cha (l) kinasema hivi:-

*"CCM itaitaka Serikali kuhakikisha kuwa Sekta ya Kilimo inatengewa si chini ya asilimia 10 ya uwekezaji unaofanywa na Serikali sambamba na lengo la Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi zilizo Kusini mwa Afrika yaani SADC".* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kwamba pamoja na tamko la Wakuu wa Nchi za Afrika ambao walikutana Maputo mwaka 2003 na wakaazimia kwamba kilimo kitengewe si chini ya asilimia tatu lakini hadi leo Serikali yetu imeendelea kutenga asilimia 6.4 kwenye bajeti yake. Mwaka jana zilitengwa asilimia 6.3 ya bajeti, mwaka huu asilimia 6.4 ya bajeti, kiwango cha ongezeko la asilimia 0.1.

Mheshimiwa Naibu Spika, sioni kama tuko *serious* sana. Tunajua bajeti yetu ndogo, lakini nafikiri tungeweza kabisa kuhakikisha kwamba pengo siyo kubwa sana kati ya sekta moja na nyingine lakini sekta moja inakuwa na asilimia 18 sekta muhimu kama ya kilimo inatengewa 6.4 lakini wakati huo huo kuna Azimio la Wakuu wa Nchi za Afrika walioazimia tutenge bajeti ya kilimo kwa kiasi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesikia wenzetu wa Kenya. Kama alivyotoka kuzungumza Mheshimiwa Chegeni hapa, wenzetu Kenya wametenga bajeti kubwa sana kwenye kilimo na wenzetu Kenya ndiyo kilimo chao kiko mbele zaidi kuliko sisi na wameendelea zaidi kuliko sisi, tatizo ni nini? Mimi naomba Serikali ichukue hatua za dhati. Tumeandika haya kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi na pengine Mheshimiwa Waziri atueleze atakapokuwa ana-*windup,* tutatumia miujiza gani tufike asilimia 10 au vinginevyo Wakuu wa Nchi za Kiafrika walikuwa wanaweka malengo ambayo hawawezi au walikuwa wanatoa *statements* ambazo wao wenyewe hawawezi kuwa na uhakika wa kuzitekeleza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niseme kwamba mimi natoka Mbozi na wakati wote nimekuwa nazungumzia suala la mbolea. Naomba nizungumzie suala la mbolea tena kwamba bila kuwa na nia ya dhati kabisa kuwapa wananchi wetu mbolea, pamoja na pembejeo nyingine, bado hatutafanikiwa kwenye suala la kilimo, hatutaweza kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshazungumza suala hili mara kadhaa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ninamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko *positive* kwenye suala hili lakini tuwe *positive* na wakati huo huo tuwe na mipango mahususi ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata mbolea hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu. Juzi nilimsikia alikuwa Minjingu kule ambako mbolea inazalishwa. Ameahidi kwamba Serikali itanunua mbolea yote ambayo inazalishwa pale na kuisambaza kwa wakulima, hilo ni jambo jema sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba kama inawezekana basi Serikali iwape nguvu wenzetu wa Minjingu ili waendelee kuzalisha zaidi. Tuna hakika kwa sababu mbolea hii inazalishwa nchini, basi na bei zake pia zitakuwa nafuu zaidi kwa wakulima wetu na kwa maana hiyo watajiandaa vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni ukweli pia kwamba kiwanda kimoja hicho cha Minjingu hakiwezi kuzalisha mbolea ya kutosha wananchi wakulima wote wa Tanzania. Waziri alipokuwa anawasilisha Hali ya Uchumi, sikuona mipango yoyote ya kushirikiana na sekta binafsi kwa ajili ya kujenga viwanda, bila ujenzi wa viwanda hatuwezi kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na mpango wa kujenga kiwanda cha mbolea kule Mtwara. Nitaomba tuelezwe limefikia wapi, kwa sababu sijaona popote pale niliposoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Hali ya Uchumi. Naomba atumie nafasi hiyo kutueleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapata pia wasiwasi, pamoja na hatua hizo nzuri ambazo Mheshimiwa Waziri Mkuu amezifanya, mwaka jana tulikuwa na bajeti ya mbolea ambayo ilikuwa takribani bilioni 21, Lakini mwaka huu tumeelezwa kwamba zitakuwa karibu bilioni 31, ni ongezeko kama la bilioni 10, bado ni pesa kidogo sana. Sisi Mbozi tunahitaji wastani wa tani karibu 30,000 ili tuweze kuzalisha sawasawa na Mkoa wa Mbeya unahitaji takriban tani 70,000 za mbolea ili tuweze kuzalisha sawasawa. Sasa ukichukulia mbolea hiyo ambayo tunaweza tukaipata tu Minjingu kama wakizalisha tani hizo 150 ukizigawa kwa nchi bado zitakuwa ni kiasi kidogo sana. Ninaomba sana sana niisihi Serikali kwanza tuzingatie tamko la Maputo la Wakuu wa Nchi za Kiafrika ambalo walifanya mwaka 2003 ili tuweze kuzalisha vile inavyopaswa na kwa maana hiyo ili tuweze kuzalisha sawasawa, ni lazima wananchi wetu wapewe mbolea ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hilo, ninaomba nizungumzie suala la mikopo. Mikopo ni moja ya jambo ambalo litawafanya wananchi wetu waweze kuzalisha mali katika maeneo mbalimbali bila matatizo au kwa urahisi zaidi lakini tuna tatizo la msingi la riba kubwa kwenye mikopo. Kinachotushinda ni nini hapa, mimi sielewi. Nilitegemea Benki Kuu ndiyo watoe sera za mikopo na mikopo ambayo inawasaidia wananchi wetu lakini *interest rates* ni kubwa sana pia kuna masharti makubwa ya ajabu ajabu, masharti makubwa sana na magumu ya ukopeshaji. Mimi nadhani haya mabenki hayapo hapa kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wetu yapo hapa pengine kuwasaidia watu wachache sana ambao ni wafanyabiashara wakubwa kuliko wananchi wa kawaida. Wakati faida ambayo anapata mtu ambaye ameweka fedha benki kwenye amana ni kati ya asilimia mbili na tatu lakini *interest rates* ambayo anatozwa huyu mwananchi ni asilimia kati ya 15 na 20, hizi benki haziko hapa kumsaidia mwananchi hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naomba kwa sababu tuna awamu nyingine ya pili ya kuwapa wananchi wetu mikopo vijijini kupitia bilioni 10 ambazo zimetengwa na Serikali na kupitia taasisi mbalimbali za kifedha, tunaomba zoezi hili kwa wakati huu lisimamiwe vizuri kwa maana ya kwamba wananchi wengi vijijini wakati huu wapate mikopo kwa sababu awamu iliyopita waliopata mikopo wengi walikuwa wananchi wa mijini zaidi. Tunategemea wananchi wengi wa vijijini sasa watatazamwa na wao waweze kupata mikopo hii. Lakini pia ni vizuri zile taasisi ambazo zitapelekewa mikopo huko vijijini zikajulikana kwa sababu nina hakika zitakuwa zinatofautiana Mkoa hadi Mkoa, kwa hiyo ni vizuri wananchi wakazijua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie suala la msamaha wa ushuru wa bidhaa. Wamezungumza wenzangu pamoja na kwamba kuna msamaha wa ushuru kati ya asilimia 5 na 10 kwenye bidhaa, ni jambo zuri lakini tatizo bado linakuja, ni urasimu. Mimi niliwahi kuzungumza wakati fulani kwamba unatoka bandarini pale uje *long room*, uende *TISCAN,* mlolongo ni mkubwa mno, wakati huo huo unalazimika kwenda Ubungo kule kwa ajili ya watu wa *TBS*. Tuliwahi kukutana wakati fulani na watu wa *TRA* tukashauri kwamba huduma zote hizi zisifanyike mahali pamoja ili kuwapunguzia wananchi wetu matatizo wakati wanafanya *clearance* ya mizigo yao? Tunategemea Waziri wa Fedha anapo-*windup,* hili pia atatueleza kwamba ni hatua gani sasa wamechukua?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nizungumzie suala la shamba la *NAFCO* kule Magamba. Shamba hili lilikuwa s*pecified* tangu mwaka 1996 chini ya *PSRC* lakini nilipokuwa napitia kwenye Hali ya Uchumi ya Waziri wa Fedha, sijaona linapotajwa popote, kwa sababu najua pia hatua hizo hazijakamilika. Kwa hiyo, kama kuna hatua zozote ambazo zimefikiwa, naomba pia atueleze kwa sababu wananchi wamekuwa wanaliomba lile shamba na mimi kama mwakilishi wao nimekuwa nimelizungumza sana. Serikali haijatoa majibu yoyote mpaka leo. Kwa hiyo, naomba Waziri atakapokuwa ana-*wind up* watueleze kwa sababu hapa tunazungumza kwamba kuna taratibu za uwekezaji tatizo ni letu na Waziri amekiri kwenye hotuba yake kwamba kuna matatizo. Sasa

mambo mengine yako ndani ya uwezo wetu wenyewe lakini tunasema kwamba ni tatizo. Tunaziita changamoto, ziko ndani yetu sisi wenyewe. Kwa mfano, riba za mikopo tunasema ni matatizo lakini mimi nadhani tuna uwezo na mambo haya mengine, ni suala la kuamua tu halafu tukaendelea mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la umeme. Nilishazungumza na Mheshimiwa Ngeleja, Waziri wa Nishati na Madini, amenihakikishia kwamba miradi yangu yote ambayo imebaki ya viporo ile ya mwaka 2003, 2006 ataitekeleza na kweli naomba itekelezwe kwa sababu itakuwa vigumu sana itakapofika zamu ya Wizara ya Nishati na Madini kuunga mkono bajeti hiyo. Kwa sababu miradi hiyo ni ya muda mrefu. Wananchi wanatupigia kelele sana hawawezi wakatuelewa. Sitaunga mkono mpaka amenihakikishia kwamba atalitekeleza hili, kwa hiyo, sina sababu pengine ya kulisema sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme jambo lingine na hili wamenituma pia wapiga kura wangu. Sijaona kwenye bajeti ya Serikali. Wenyeviti wetu wa Serikali za Vijiji wanafanya kazi ngumu sana. Hawa ndio wanaosimamia shughuli nyingi zinazofanywa kwenye vijiji. Hawa ndiyo wanaofanya kazi na ma-*VEO* kule vijijini. Ma-*VEO* wanalipwa mshahara lakini Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji ambaye ndiye anayemsimamia *VEO,* ambaye ndiye anayeongoza vikao kwenye Kijiji, Mwenyekiti huyu halipwi kitu chochote. Najua tunaweza tukasema kabisa nchi ni kubwa. Wenyeviti wa Serikali za Vijiji ni wengi lakini Serikali hebu ilifikirie hili, kama Chama cha Mapinduzi, chama ambacho kinapata ruzuku toka Serikalini kinalipa shilingi 5,000 kwa Makatibu wa Tawi, hivi Serikali kwa nini ishindwe kuwalipa Wenyeviti wa Serikali za Vijiji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Serikali itoe majibu ya kuridhisha. Naomba nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili walifanyie kazi kubwa kwa sababu mimi kule ninakotoka wananchi wanataka kusita kuchukua hata fomu kwa ajili ya uchaguzi unaokuja. Watafanyaje kazi ambayo haina tija? “Tunaifanyia kazi Serikali kazi kubwa lakini Serikali haitambui kama tunafanya kazi kubwa”. Kwa hiyo, naomba Serikali pia Mheshimiwa Waziri wa Fedha au Waziri Mkuu atakapokuwa anawasilisha bajeti yake basi na hilo pia alisemee ili tuweze kuelewa majibu ni nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikimalizia, naomba niseme kwamba kumekuwa na upunguzaji wa ushuru kwenye magari lakini *pickups* hutumika sana vijijini zenye CC1500 mpaka CC2500 zimepunguzwa kwa takribani shilingi 30,000, ndizo wanazotumia wananchi wetu wengi vijijini kule, wengi sana. Mheshimiwa wa Kambi ya Upinzani asubuhi alisema yale magari makubwa kama mabasi yaondolewe ushuru. Hizo zenye CC1500 hadi CC2500 ushuru ungepunguzwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo, ninaomba niseme kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kuweza kuzungumzia bajeti hii. Napenda nitoe pongezi zangu kwa Waziri wa Fedha, Manaibu Waziri, Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuwasilisha bajeti yao ambayo imekuwa na matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya ya pongezi, nipende tu kushukuru Serikali, miaka iliyopita sisi Wabunge wa Kanda ya Ziwa tulikuwa na tatizo kubwa la usafiri hasa barabara lakini tarehe 6/5, Mheshimiwa Rais alikuja kufungua barabara ya kutoka Kamunyorwa mpaka Geita na kufungua ujenzi wa barabara kutoka Geita kwenda Usagara. Si jambo dogo ni jambo moja kubwa kabisa. Nipende kuishukuru Serikali kwa kutimiza ahadi ambazo ziko kwenye Ilani ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kufunguliwa kwa barabara hizo kunailetea tija Wilaya yetu ya Geita kwasababu ilikuwa kama kisiwa. Tulizungumza sana tukaielekeza Serikali na tukataka kugoma katika bajeti za miaka iliyopita, lakini kwa ujasiri mkubwa Serikali imeweza kutusikia. Kwa niaba ya wananchi wa Geita na Sengerema, napenda kutoa shukrani za dhati kabisa kwa kazi hiyo na hasa kwa kukifungua kivuko cha Busisi ambacho sasa hivi kinafanya kazi. Si jambo dogo kwa Serikali kutimiza mambo makubwa kwa muda mfupi kama huo. Tunasema asante sana kwa niaba ya Wilaya ya Geita na Sengerema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mazuri na mabaya ambayo yanaweza yakajitokeza katika bajeti hii. Tumesema bajeti ni nzuri, lakini kuna mengine ambayo yanaweza yakawa ni mapungufu katika maeneo fulani. Katika kitabu hiki cha bajeti ambacho Waziri amewasilisha, ukurasa 31 kifungu (d) kinasema: "Inaonekana kushuka ikilinganishwa na mwaka huu wa fedha 2007/2008. Sababu kuu ni kwamba ujenzi wa mradi mkubwa Shinyanga – Kahama, umekamilika. Aidha, fedha za miradi ya maendeleo za nje zinaendelea kupungua."

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kutoa kilio cha wananchi wa Geita. Wananchi wa Geita tatizo lao kubwa kabisa sasa hivi ni maji, baada ya kumaliza tatizo la barabara. Wilaya ya Geita na Mji wa Geita kwa ujumla wananchi wake wengi hawana maji safi. Kama mtakumbuka Wilaya ya Geita, mara nyingi imezungukwa au ina wawekezaji na wachimbaji wadogo wengi wa dhaghabu. Mchakato wa kupata dhahabu unatumia zebaki na zebaki nyingi unakuta inaingia ardhini kiasi ambacho inachafua maji wanayotumia wananchi wa Geita. Sasa ukisema kwamba bajeti imepunguzwa katika eneo hili la maji, unakuta kwamba tunaiumiza Wilaya ya Geita ambayo sijaona hata sehemu moja imetajwa kwamba itatengewa pesa ya aina yoyote au mradi mkubwa kwasababu miradi inayotengewa ni midogo tu ya *picnic* ambayo haiwezi ikakidhi mahitaji ya Wilaya ya Geita.

Wilaya ya Geita katika mpangilio ambao tulikuwa tumeshapanga kutokana na pesa za *MCC* ambazo hazikulengwa katika utumiaji wa maji, tulikuwa tunategemea kwamba ungekuwa mradi wa Sh. 18,000,000,000/= ambao Serikali sasa hivi haiwezi ikatoa pesa hizo. Sasa nilikuwa najiuliza, kama Serikali imeshaahidi kwamba itatoa fedha hizo katika kipindi cha miaka mitano mpaka mwaka 2010, kwa sasa hivi haijatoa na hatujatenga sehemu yoyote na bajeti hii inazidi kushuka ukilinganisha na bajeti zilizopita: Je, Wilaya ya Geita itapata maji kweli? Nilikuwa naomba kabisa Serikali kwa ujumla, iingilie kati iweze kuikomboa Wilaya ya Geita katika kuiletea maji safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna miradi mingi ambayo ilikuwepo, lakini yote ile imetelekezwa. Kuna miradi ya nyakagomba ambayo ilianzishwa mwaka 1976 na mradi wa Nyamtukuza, miradi yote hii imelala na hakuna inayofunguliwa. Kuna mradi ambao uko Kasamwa, kuna mradi uko Nzela, lakini yote hii imekaa tu. Kama Serikali ingeweza kuifungua hii miradi ingeweza ikawapunguzia wananchi wa Geita wakaweza kupata maji safi ambayo nategemea kabisa Wizara kama Wizara ya Fedha, iweze kutenga fungu maalum kuweza kuinusuru Wilaya ya Geita ambayo imeathiriwa sana na wachimbaji kutokana na Zebaki iliyoko katika maeneo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo tumejaribu kuliangalia kwamba lina matatizo. Katika Wilaya ya Geita, kuna wachimbaji wakubwa na wengi wanahitaji kuja kuwekeza katika Wilaya ya Geita. Lakini tatizo kubwa lililokuwepo ni kuwaacha wananchi katika maisha ya chini sana, hasa kwa maeneo yao mengi kuchukuliwa na wachimbaji wakubwa na wao kusukumwa sehemu ambazo zisizojulikana. Ningependa kushukuru kampuni ya *East Africa* ambayo imeweza kutenga angalau kidogo katika eneo lake sehemu za Lwamgasa na kuwapatia wachimbaji wadogo. Lakini kampuni ya *GGM* inaonekana imehodhi maeneo makubwa. Kwanza ina leseni, nitaizungumzia katika Wizara ya Nishati na Madini. Ina leseni kubwa kabisa ambayo ina eneo kubwa, wanaita *special mining license,* lakini tena imechukua leseni nyingine ndogondogo katika maeneo yanayozunguka Wilaya ya Geita. Sasa unakuta wananchi ambao wangeweza wakajipatia kipato chao na kuongeza pato la Taifa wananyimwa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba makampuni haya makubwa yanapopata leseni za uchimbaji, basi wawaachie hizi leseni nyingine wananchi au wachimbaji wadogo waweze na wao kujipatia vipato katika maeneo husika. Wilaya ya Geita karibu yote imezungukwa na dhahabu, lakini unakuta kwasababu wachimbaji wakubwa wameshachukua wananchi wanalazimika kuanza kuingia katika maeneo na hapo unakuta kunakuwa na migogoro ambayo ingeweza ikatatuliwa. Mfano mzuri ambao tunaweza tukausikia ambao kesi yao iko Mahakamani ni wananchi wa *mining* mpya. Kwa hiyo, namwomba Waziri wa Sheria ajaribu na yeye kuliangalia suala hili ili wananchi walioko pale Geita mjini sehemu ya Mahakama ya Mwanzo walimalize tatizo hili kimahakama haraka iwezekanavyo ili tuweze kupata ufumbuzi wa maana. Lakini kutokana na haya, inaonekana wachimbaji wakubwa wanachukua maeneo makubwa kiasi ambacho wananchi wengi wa Geita wanakosa mapato yao au kuliongezea pato la Taifa kutokana na uzalishaji wa dhahabu zinazotoka pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia eneo hili la wachimbaji wakubwa unakuta kwamba pesa nyingi wanapeleka kwao, lakini kama wakiachiwa wachimbaji wadogo wadogo hawana sehemu zozote za kupeleka hizi pesa. Wata-*invest* hapa nchini, watazalisha hapa nchini na kwa hiyo, pato la Taifa litapatikana hapa hapa. Lakini tumejaribu kuwathamini sana. Kama Waheshimiwa wengine walivyozungumza kuhusu wawekezaji kutoka nje kwamba wanakuwa na malengo yao makubwa tu. Mtu hawezi akaja hapa akasema anakuja kukupatia faida, mara nyingi anakuja hapa ili na yeye avune apate chochote atakachokihitaji. Naomba wachimbaji wadogo katika maeneo haya watengewe sehemu ambazo wanaweza wakajipatia riziki.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri wa Nishati na Madini, katika Wilaya ya Geita kuna maeneo ya Nyamatagata, Mgusu, Nyaulilima, Lwenge, maeneo yote yale yana dhahabu lakini sasa unakuta sehemu zote zile wamechukua wakubwa. Nilikuwa naomba sana eneo hili litiliwe maanani ili kuweza kuokoa maisha ya wananchi wa Geita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweza kuliongezea pato la Taifa, nafikiri Mawaziri wengi wameshapita, wanajaribu kuangalia ni jinsi gani ambavyo tunaweza tukaongeza pato la Taifa. Tumeangalia katika maeneo mengi, miaka ya 90 nafikiri ndio tukaanzisha *TRA.* Niwashukuru kwamba wamefanya kazi moja kubwa kabisa ya kuweza kukusanya pato la Taifa. Kila mtu ameliona, lakini sio *TRA* tu, nilikuwa naomba kitu kimoja kifuatacho kiangaliwe, kwamba tuimarishe vyombo vyetu vya ulinzi, kwasababu bila kuimarisha vyombo vyetu vya ulinzi hayo yote tuliyoyazungumza ni kazi bure. Kwasababu kutakuwa na vurugu, kutakuwa hakuna amani, na bila amani hamuwezi mkazalisha na bajeti ile tusingeweza kuizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kumekuwa na wimbi moja kubwa sana la ujambazi la uporaji, lakini unakuta vyombo vyetu vya ulinzi havina vitendea kazi vya kuweza kuwasaidia kuweza kurahisisha kazi zao. Kwa mfano, Wilaya ya Geita ni kubwa sana, lakini ina gari moja tu la Polisi, unategemea watafanya kazi gani? Watawasaidiaje wananchi ili waweze kuleta amani katika sehemu ile? Nilikuwa naomba kabisa kwamba katika bajeti hii au bajeti ya mwaka ujao kipaumbele kiwekwe katika vyombo vya ulinzi. Wakiweka bajeti kubwa kwenye Jeshi la Polisi, Magereza, *TAKUKURU,* Usalama wa Taifa, nina hakika vyombo vile vikiimarishwa sidhani kama kuna sehemu ambazo hata Serikali yenyewe itakuwa na ule uwoga. Lakini sasa tunawaruhusu kwasababu hawana lolote, watafanya kazi gani? Watu wamebweteka! Lakini nilikuwa naomba waongezewe fedha ili waweze kutuletea tija katika uongezaji wa bajeti katika nchi yetu. Hilo lilikuwa ni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa vifaa vya ujenzi, sisi kanda ya Ziwa, tumekuwa na matatizo sana. Nilipokuwa kwenye ziara katika jimbo langu nilikuwa naulizwa, Mheshimiwa Mbunge, sasahivi tunahamasika kujenga nyumba kwa tofali za kuchoma, lakini tunashindwa kuezeka kwa sababu ya bei kubwa ya mabati. Sasa tutafanyaje?

Nilikuwa naiomba Serikali, kama kuna uwezekano, maeneo ambayo yako mbali na usafiri ni mbovu, basi Serikali iweke ruzuku katika vifaa kama hivi muhimu ambavyo wananchi wanahitaji angalau na wenyewe wajikomboe katika nyumba bora. Bila hivyo, utakuta wananchi wengi wanaishia kukaa katika nyumba za majani au tunazoziita *full suit.* Napenda sana kutoa fursa hiyo ili wananchi wa Jimbo la Geita waweze kujenga nyumba safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna sehemu nyinggine vijijini kuna umeme. Kuna vijiji vingi vingi sana vinahamasika sasahivi kutumia umeme na wengine ukikuta hata vijijini wanatumia *solar,* wengine wanatumia hata betri za magari ili angalau wapate mwanga.

Lakini kwa utaratibu huu wa Serikali wa kupeleka umeme vijijini nilikuwa nakuomba kabisa wafanye kazi hiyo katika maeneo mbalimbali hasa katika Wilaya ya Geita na Jimbo la Geita. Kuna maeneo ya wavuvi sehemu za Nkome, sehemu za Maramba, sehemu za Nzela, sehemu za Lwenzela, basi wapeleke umeme maeneo yale ili kuwarahisishia wavuvi kupata angalau tija katika eneo hili.

Lakini kuna sehemu nyingi ambazo ni za machimbo mengi ambayo yakipelekewa umeme, unaona kwamba kutakuwa na uzalishaji mkubwa hasa wachimbaji wadogo wadogo. Sehemu za Mgusu wakipelekewa umeme wa vijijini, naona watapata au wataweza ku…. *(Hapa kengele ililia)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye hoja hizi zilizo mbele yetu. Kwanza kabisa, nampongeza Waziri, Manaibu Waziri, pamoja na timu yao yote kwa hotuba nzuri. Naungana na Watanzania wengi ambao wameunga mkono bajeti hii kwa kusema hii bajeti ni nzuri na inawajali watu. Nami nasema bajeti ni nzuri kwasababu kwanza kabisa kwenye kima cha chini hawalipi kodi, halafu asilimia kwenye viwango mbalimbali vya mishahara imepungua.

Naipongeza Serikali kwa kuondoa kodi kwenye mafuta mazito. Hii itawafanya Watanzania walio wengi kuacha kutumia mkaa na kuni, watatumia mafuta kupikia na kwa hiyo, watakuwa wanahifadhi mazingira. Naipongeza Serikali vilevile kwa kuondoa kodi kwenye matrekta, majembe ya mikono, magunia, gesi, haya yote yatasaidia kupunguza makali ya maisha kwa Mtanzania wa kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotakiwa sasahivi ni kulinda uchumi wetu kuhakikisha kwamba hautatokea mfumuko mkubwa wa bei, kusudi haya mabadiliko yaweze kuwafaidisha walio wengi. Naipongeza *TRA* kwa sababu wameweza kukusanya kodi kwa kiwango kikubwa sana cha kujivunia. Ila natoa ushauri nikiamini kwamba wanaweza kufanya vizuri zaidi, wanaweza kupanua wigo kwa kusajili walipa kodi wengine, wanaweza kupanua wigo kwa kutafuta vianzio vingine vya mapato na vilevile wanaweza kuongeza mapato kwa kupunguza hii misamaha ya kodi. Kwa sababu hii,

misamaha ya kodi unaweza ukakuta kwamba wafanyabiashara wengine wanaopewa hii misamaha wanapitisha biashara tofauti na zile zilizokusudiwa na kwa kufanya hivyo, unakuta tunapoteza mapato ya Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania zaidi ya 70% wanakaa vijijini na zaidi ya 80% ya wanaokaa vijijini ni wakulima walio masikini. Kama Serikali ina dhamira ya kweli ya kuondoa umasikini, tunapaswa tulenge Watanzania walio wengi na ambao ni masikini, tuweke mikakati ya kuwatoa hapa walipo waweze kupata maisha mazuri.

Mheshimiwa Waziri, kasema uchumi wetu unakua kwa 7%, naipongeza Serikali. Lakini *it doesn't trickle down* mpaka kwenye *grass root* watu hawajisikii kwamba wana hela mifukoni inayolingana na ukuaji wa uchumi. Nchi ya Angola ambayo ni nchi ya Afrika kama sisi Waziri ametueleza kwamba uchumi wao umeweza kukua mpaka 21.1% na wamefanikiwa kufanya hivyo kwasababu sasahivi imetokea *opportunity,* fursa, bei za mafuta zimepanda duniani, kwa hiyo na wao wameuza mafuta mengi nje, uchumi wao ukaweza kufikia kiasi hicho. Nasi tunaweza! Bei za mafuta duniani zimepanda lakini nchi za Ulaya na Amerika, wameamua kutumia nafaka kutengeneza mafuta. Kwa hiyo, nasi tunaweza tukaitumia hii kama neema, kama fursa tuweze kupanua kilimo chetu. Bajeti iliyopangwa ya Sh. 460,000,000,000/= haitoshi kuweza kukidhi kiwango cha upanuzi unaohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa mapendekezo yafuatayo: kwanza kabisa, tunachotakiwa kufanya ni kubainisha maeneo humu ndani ya Tanzania yenye mahali pazuri pa kulima, mahali ambapo tunaweza tukapata mashamba makubwa, hali ya hewa ni nzuri, kuna mvua za kutosha na rutuba ya kutosha tulime huko mashamba makubwa tuachane na hivi vishamba kimoja kimoja. La pili, lazima Serikali ihakikishe kwamba inawekeza kwenye miundombinu ya barabara pamoja na mifumo ya umwagiliaji. Hatuwezi kuendelea kulima kwa kutegemea mvua! Sasa hivi inabidi tuwe na mifumo ya umwagiliaji.

Vilevile ninajua Serikali ilishajiondoa kwenye kufanya biashara, lakini kwa hili, kwa kuwa tumepata fursa hii, nilikuwa naipendekeza kwa Serikali kwamba sasa wafanye linalowezekana wakati wanaendelea kushawishi wawekezaji, lakini Serikali inunue matrekta, inunue *heavy equipments.* Serikali inunue ma-*combined harvester,* wahakikishe kwamba tunalima mashamba makubwa. Haiwezekani miaka 48 baada ya kupata uhuru tukaendelea kutumia jembe la mkono ambalo limetumiwa na vizazi kama vine au vitano nyuma yetu. Kama kweli tuko *serious* tunataka kupanua kilimo inabidi tulime kwa *heavy equipments.* Hatuwezi kuendeleza kilimo kama tutaendelea kutegemea mvua. Mvua zenyewe hazitabiriki, mtu atalima, mazao yatakauka, atapata hasara. Kwa hiyo, inabidi Serikali iwekeze katika umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napendekeza vilevile kwa Serikali kwamba wakati umefika wa kuwa na benki ya wakulima. Mabenki ya biashara hayawezi kuwakopesha wakulima kwasababu ya *risks* zilizopo. Kwa hiyo, inabidi tuwe na benki itakayowakopesha wakulima, itakayoweza kutoa mikopo mikubwa kwa wakulima na mikopo hiyo ikawa ya muda mrefu, kufanya hivyo tutaweza kupanua kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nafikiri Serikali vilevile ingeendelea kukiwezesha kile kiwanda cha mbolea tulichoambiwa, kusudi mbolea iweze kutengenezwa hapa. Lakini wakati maandalizi ya kiwanda yanaendelea, basi Serikali ihakikishe kwamba inaagiza mbolea yote inayohitajika isambaze kwenye maeneo kufuatana na aina ya mbolea inayohitajika katika mkoa huo. Nilikuwa pia napendekeza kwamba, wananchi wahamasishwe sasa waweze kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya kuongeza thamani ya hayo mazao, kwa maana ya nafaka hizo kwa kuzisafisha, ku-*grade,* kufunga, kuisindika, nakadhalika. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tumeongeza thamani ya haya mazao na yatauzika kirahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napendekeza vilevile kwamba zianzishwe bodi za mazao mchanganyiko ili huyu mkulima sasa akilima aweze kupata bei nzuri kuliko ilivyo sasa hivi wanalima wanapata bei ndogo kwa sababu wanaendelea kuwauzia wale walanguzi. Kwa hiyo, kuwe na chombo ambacho kitaweza kumpa mkulima bei nzuri. Mpango huu ukiwezekana, kwanza kabisa tutapata chakula cha kutosha, pili tutapata ziada tutauza nje, nasema sasa hivi fedha za nje zinatosha kuagiza vitu vya miezi minne, kwa mpango huu tunaweza kupata fedha za kigeni za kuagiza hata bidhaa zinazotosha takribani miezi nane.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu mojawapo tuliyoambiwa inayoleta mfumuko wa bei ni upungufu wa chakula. Jamani, sasa imetokea fursa, tupanue kilimo tupate chakula cha kutosha. Kwa kufanya hivyo, tutahakikisha kwamba mfumuko wa bei umedhibitiwa. Pato la Taifa linaweza kuongezeka kwa muda mfupi tukafikia hata *digit* mbili, 10% na kuendelea. Mungu ametushushia neema, tumepata muarobaini wa kukuza uchumi wetu, tujipange vizuri tupanue kilimo na tulime kisasa. Sasa najua wengi watachangia hili eneo kwasababu limemgusa kila mtu baada ya kuona kwamba fursa ipo. Ningependa basi Waziri wa Fedha atakapokuwa ana-*wind-up* atuambie atafanya nini kuhakikisha kwamba sasa bajeti ya kilimo inaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuendelea kuipa sekta ya Miundo Mbinu, kipaumbele. Bilioni 973.3 zilizotengwa zitatusaidia kweli kuendeleza ile miradi ya barabara iliyoishaanza na kulipa madeni. Lakini ikumbukwe kwamba miundombinu ya barabara siyo miundombinu pekee ya usafirishaji, kuna meli, kuna reli, kuna ndege, Mkoa wa Kagera unafikika kirahisi kwa ndege, kwa meli, vilevile na barabara. Moja ya ahadi za Rais Kikwete, ilikuwa ni kupanua na kutengeneza uwanja wa ndege ulio Bukoba Mjini kwa kiwango cha lami. Miaka miwili imepita, huu ni wa tatu, nimeangalia kwenye vitabu vyote vya bajeti, sikuona hata senti moja iliyotengwa kwa ajili ya uwanja huo. Wakazi wa Kagera wanateseka, vyombo vya maji vyenyewe havitoshi baada ya kuzama *MV Bukoba* iliyokuwa meli kubwa, ikabakia *MV Victoria* ambayo imezeeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka jana, miezi 10 kati ya 12 meli hiyo ilikuwa *grounded* kwasababu ilikuwa kwenye matengenezo. Watu waliendelea kuhangaika wakawa wanapanda meli za mizigo. Bilioni 973 zote ni za barabara, labda ningeomba Waziri atuambie ni nini hatma ya barabara ya Kagoma, biharamulo mpaka

Lusahunga? Wanakagera kwanza wanashukuru tumeweza kutengenezewa barabara ya lami kutoka Mtukula, Bukoba mpaka Kagoma, lakini Mkandarasi aliyekuwa anatengeneza barabara ya kutoka Kagoma alifanya uzembe akasimamishwa. Ni miezi mingi takribani miezi 5 hatuoni harakati zozote za kumchagua Mkandarasi mpya, ndio maana nauliza hatima ya barabara hiyo ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu barabara hii ikishatengenezwa ikaunganisha Mkoa wa Kagera na Mikoa mingine itachochea kukua kwa uchumi. Wote mnajua kwamba wananchi Kagera ni walima ndizi na ndizi sasa hivi zimekuwa *international food,* kila mtu anakula ndizi. Tunaweza tukasafirisha ndizi zikaenda kwenye migodi ya Geita, Kahama na Mikoa mingine ya jirani kama hii barabara itakuwa imetengenezwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha kutotenga fedha kwa ajili ya uwanja wa ndege wa Bukoba. Kimenisikitisha sana! *ATC* walikuwa hawapeleki ndege Bukoba pamoja na kwamba ni shirika la Taifa. Iliyokuwa inapeleka huduma ni *Pricision Air,* zilikuwa zinakwenda ndege ndogo kwa sababu ule uwanja ni mfupi na ni wa matope. Sasa hivi zile ndege ndogo zimekatazwa kimataifa, zimefungiwa.

Kwa hiyo, tangu tarehe 1 Mei, hakuna usafiri wowote kati ya Mwanza na Bukoba kwa sababu ndege za *Precision* zimeacha kufanya kazi. Ikumbukwe kuwa mwaka 2007, alipokuja aliyekuwa Waziri Mkuu - Mheshimiwa Lowassa, wakati wa kuondoka ilibidi watu wengine waondoke kwenye ndege wasafirishwe kwa magari mpaka Mwanza, kwa sababu ndege isingeweza kuinuka kwenye yale matope.

Mheshimiwa Naibu Spika, alipokuja Mheshimiwa Rais Kikwete, mwaka huu ndege iliishafika mpaka Bukoba, tunaiona, ila ikabidi igeuze, ilishindwa kutua. Rais wa watu ikabidi arudi aende kutua Geita, magari yaondoke Bukoba yamfuate Geita.

Sasa kwa kweli tunaomba mtueleze ni lini sasa wananchi wa Bukoba wataondolewa hii adha na kuhakikisha kwamba huu uwanja unatengenezwa kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, kwa kuahidi sasa kwamba atazingatia jinsia. Ikumbukwe kwamba katika Tanzania hii kuna wanawake zaidi ya 51% lakini nataka nikwambie kitu kimoja tu kwamba kwa takwimu za mwaka 2006 asilimia ya wanawake Mabalozi ilikuwa ni 3%, Makatibu Wakuu 28%, Wakurugenzi wa Wilaya 21%, Wakuu wa Wilaya 21%, Wakuu wa Mikoa 10%, na *RAS* 23% na kadhalika, Mawaziri 21.5% na Wabunge humu Bungeni ilikuwa 30.4%. Sasa mmesema mnaandaa mkakati wa kufikia *fifty fifty*, kwa kweli nawapongeza sana na huo mkakati tunausubiri kwa hamu. Inawezekana kwa sababu hata nchi jirani ya Rwanda, wao wameweza kufikia 48.8%. Je, mkakati huo utakuwa tayari lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii nami niungane na wenzangu kwa kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, pamoja na Naibu wake na Katibu Mkuu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na mambo mengi yaliyozungumzwa na wenzangu na pia nakubaliana na bajeti. Kwa hiyo, naunga mkono moja kwa moja ingawa wenzetu walipitia kiongozi wa upinzani asubuhi hii ameiponda kweli bajeti yetu, lakini mimi ninavyoiona bajeti mbadala aliyoileta ni alfu lela ulela tu. Lililopo kubwa kwa kweli sisi ni kuiboresha bajeti yetu na kuboresha yale yaliyosemwa na Serikali ili tuweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo juu ya ilani ya Chama cha CCM na hasa juu ya maneno muhimu ya *Ari Mpya, Kasi Mpya na Nguvu Mpya.* Kusema kweli Tanzania katika maendeleo ya kiuchumi tunakwenda kwa kasi na kasi hii ni ya kwenda mbele. Tumejitahidi sana kwenda mbele, lakini naona kuna hitilafu kidogo. Hitilafu hiyo naiita ni kasi ya *reverse* au ni kasi ya kurudi nyuma ambayo inafanywa na watendaji wa Serikali. Hiyo nitaitolea mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa mradi wa *Mnazi Bay,* Mheshimiwa Rais alikuja Mtwara mwezi Novemba na alipouliza umeme utawaka lini kwa Mikoa ya Kusini aliambiwa wakati wa *Christmas* mwezi Desemba, 2006 na yeye akasisitiza kuwa basi umeme upatikane. Kuanzia hapo watu wote wa Mikoa ya Kusini, tulianza nasi kusema *kuchele! Kuchele!* Maana yake kumekucha! Kumekucha! Giza linaondoka mwanga unafika. Sasa ikatiwa *gear* ya *reverse* kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo *gear* imetufanya mpaka leo hata wakati huu nazungumza Masasi iko gizani, Nachingwea haina Umeme, Ruangwa haina umeme, Newala haina umeme na Tandahimba haina umeme. Yote hii ni kwa sababu ya *reverse gear* ya utendaji! Ukiuliza, mara mikataba bado, mara sijui Hazina kufanya nini, mara *TRA,* mara *BOT*, sasa Kamati chungu nzima mpaka kiasi kwamba watu wa kusini hawaelewi nini kinatokea! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka leo kilometa zile zilizobaki 32 kati ya Nyangao na Ndanda, nyaya za umeme hazijasambazwa. Ni eneo dogo sana, kilometa 32 lakini kilomita 32 hizo zinafanya umeme katika maeneo niliyoyataja upatikane kwa masaa manne tu. Mara nyingi umeme huo unapatikana kuanzia saa 8.00 ya usiku mpaka saa 12, *astakhfirullah (Makofi).*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa siyo kwamba hakuna jitihada zinazofanywa, jitihada kweli zimefanywa na Hazina juzi tarehe tisa kwa bahati tumepata barua kwamba sasa makubaliano yanaweza kuendelea, tukasema ndio kutakucha sasa. Sasa ninachoomba Waziri wa Nishati tafadhali aiambie *GNT* ikutane mara moja ili mikataba kati ya *ARTUMAS* na Serikali ikamilishwe tuweze kupata umeme, hiyo ndio kasi mpya na nguvu mpya tutokane na ile *reverse* ya kasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tukifurahia hiyo, kwamba hilo limekamilika mara tukasikia kuna tatizo lingine limejitokeza na nikasema balaa gani hii? Limejitokeza kwa sababu hiyo, kampuni itakayoleta umeme imearifiwa kwamba Serikali imewaambia kwamba hawana ruhusa ya kuuza gesi yoyote nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wao wameshtuka kwa sababu kama mlivyomsikiliza ndugu yangu Rished hapa asubuhi, amesema gesi tuliyonayo pale ni nyingi *trillion 1.2 cubic units* sijui wanaitaje kitaalamu! Kusini. Lakini mimi nitaita *cubic meters*, ipo nyingi sana. Inatosha kwa umeme hizo megawati 28, na megawati 300 kupeleka katika Gridi ya Taifa. Inatosha pia kwa viwanda vya mbolea na viwanda vya sementi na kwa viwanda vya vyuma na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tusi-*export*? Kwa upesi upesi nina takwimu hapa, niwaelezeni kidogo kwamba kama tukipeleka Mombasa *cubic units* hizo 35,000 kwa bei ya dola 10.5, mapato yatakuwa dola bilioni 1071 ambazo kwa mgawanyo Serikali itapata kwa kupitia kwenye kodi dola milioni 477, *TPDC* itapata dola milioni 364 na hiyo kampuni ya *ARTUMAS* itapata dola 230, yaani katika utaratibu huu Serikali tunahakikishiwa dola milioni 844.

Sasa ukiwa na kiwanda cha mbolea wao wanataka hizo *cubic units* 49,000 na kwa bei itakuwa dola 2.35, Serikali hata hivyo itapata dola milioni 76, *TPDC* itapata dola milioni 88 na kutakuwa na hasara hapo ya dola milioni 51.

Mheshimwa Naibu Spika, kwa kuuza gesi meli zitakuja Mtwara kuchukua kwenda Mombasa au hata Japan. Tukiuza gesi tutaweza wakati huo huo kujenga viwanda vyetu vya mbolea pamoja na kufidia hasara zote za utengenezaji wa mbolea na wakati huo huo tunaweza kupata faida kubwa katika kuwekeza katika hivyo viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba Serikali iliangalie jambo hili upya ili uwezekano wa biashara uwepo na sisi kuwaringia Wakenya ku-*export* kutoka Tanzania ili wajue kwamba Tanzania ni babu kubwa siku hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jamani tusiliache! Ninaomba sana hili Serikali ilifikirie. Wakati huo huo kama mnavyofahamu, gesi hii imevumbuliwa Msimbati, kule ni mpakani kati yetu na Msumbiji, wenzetu wa upande wa Msumbiji nao wanaendeleza, wakiona sisi hatutatumia gesi yetu vizuri wao watachukua soko hilo. Kwa hiyo, kwa nini sisi tupate hasara halafu wenzetu wa Msumbiji wapate faida? Serikali chonde chonde, hebu fikirieni jambo hili muweze kuinufaisha nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili nililotaka kulizungumzia ni juu ya maendeleo yanayoibuka Mkoani Mtwara. Mtwara sasa hivi rasilimali zinaanza kuibuka, ndio kuchele hasa viwanda vya mbolea, viwanda vya sementi.

Kwa hiyo, bandari ya Mtwara naomba Serikali iipanue na kuhakikisha kwamba inaimarishwa, kimiundombinu na kupeleka zana za kufaa za kuweza kupakua mizigo kila

wakati. Bandari ya Mtwara ina bahati kwamba ina kina kirefu na inaweza kuwa bandari ya pili kutoka Dar es Salaam kwa kuweza kuhudumia bidhaa nyingi. Kwa hiyo, tuchukue nafasi hii kupanua hii bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuna kiwanda cha ndege kizuri tu! Ni suala la kukifanya kiwe cha kimataifa, kuwekea taa, kuweza kujenga *terminal* nzuri ili ndege ziweze kuja moja kwa moja kutoka Ulaya mpaka Mtwara na kuna *business* ya kutosha ya kufanya hivyo pale Mtwara.

Kwa hiyo, naomba sana hili likamilike. Naomba pia wakati huo huo barabara yetu hii toka Dar es Salaam, tunaiimbia kila siku, zimebaki sasa kilometa 60. Hatuwaombi lingine, kilometa 60 tu jamani, zikamilike upesi tupite! Namna nyingine, kipande kile majambazi wanaweza kukaa wakaanza kuleta kila aina ya rabsha na kuiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, naomba pia kwa upande wa maji, jamani Mji wetu wa Masasi una shida kweli kweli na kwa bahati nzuri kulikuwa na ahadi wakati Mheshimiwa Rais anapita kwenye kampeni, aliahidi kwamba maji Masasi yatakamilika na baada ya uchaguzi Rais hivyo hivyo aliahidi tena kwamba tutakuwa na mradi mkubwa wa kutoka Mbinji.

Sasa jamani miaka miwili na nusu imepita chonde isiwe *reverse* ile ya umeme iwe *forward* tu, kasi na hiyo kasi ikiwa *forward,* basi ninaamini maji yatapatikana katika muda huu uliobaki. Kwa kweli tunaomba sana sana Wizara ya Maji ijitahidi hata ikibidi tutumie fedha za humu ndani, hivi tutakuwa tunangoja fedha za kutoka Saudi Arabia na China mpaka lini? Tujitegemee wenyewe tuanze miradi ya maji muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Waziri wa Fedha umweleze Waziri wa Maji kwamba aweke kiasi fulani tupate maji pale Masasi, hilo ndio tunaloliomba sana wananchi na kwa kweli wananchi wote wa Kusini kama nilivyosema, wala hawana matatizo, wanataka Kusini kuwe na mambo ya umeme, maji, barabara, tunaamini haya yanawezakana kukamilika katika bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninaiunga mkono sana bajeti hii wala haina wasiwasi, tutaitekeleza bila maneno. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tukipata yote kutakuwa kuchele kweli kweli! *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu dhati kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hizi mbili, hotuba ya bajeti na hotuba ya hali ya uchumi na ninafahamu ya kwamba sisi kama Kambi ya Upinzani ni Serikali kivuli.

Kwa jukumu letu la kidemokrasia ni kuonyesha pale ambapo wenzetu hawapaoni na tumeonyesha katika bajeti yetu kivuli maeneo ambayo wenzetu hawakuyaona katika

bajeti iliyopita, wameyaona katika bajeti ya mwaka huu na wakawa wamepelekea Serikali kuweza kuongeza mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wanapozungumza na kudhihaki bajeti kivuli ambayo Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed ameitoa kwamba ni alfu lela ulela nashindwa kuelewa sifa zilizowafanya Wabunge hao kuja katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na hali ya uchumi.

**NAIBU SPIKA:** Naibu Spika husikiliza yote tu, alfu lela ulela na mengineyo. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na hali ya uchumi. Tuna changamoto kubwa sana kama nchi kwamba hivi sasa tunaishi katika uchumi unaokuwa, lakini umaskini haupungui na hii ndio changamoto ambayo bajeti inapaswa kuijubu na haiwezi kujibiwa kwa bajeti ya mwaka mmoja inajibiwa kwa utaratibu maalum na toka tumeingia katika Bunge hili na hii ni bajeti ya tatu kumekuwa na rekodi za uchumi kukuwa, lakini taarifa mbalimbali za Serikali, taarifa za hali ya umaskini toka tumekuwa Wabunge kumekuwa na taarifa mbili za hali ya umaskini, zote zinaonyesha kwamba umaskini kwa wananchi bado ni mkubwa na katika bajeti iliyopita tulizungumzia suala zima la madhara ya kupandisha kodi za baadhi ya vitu kwa maisha ya wananchi na wenzetu wakakataa kata kata, lakini athari zinaonekana hivi sasa na leo tunaiita bajeti ambayo Mheshimiwa Waziri Mkulo ameitoa kwamba ni bajeti ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezi kuwa bajeti ya mwananchi kwa sababu kodi ambazo zilipandishwa mwaka 2007 hazijashushwa kurudishwa katika viwango vya mwaka 2006/2007, itakuwa ni bajeti ya mwananchi iwapo tu kodi hizo zitakuwa zimeshushwa.

Lakini kitendo cha kuziacha kodi hizo kama zilivyo bado kitaendelea kufanya mfumko wa bei uweze kuendelea na nitaelezea huko chini.

Uchumi wetu umebadilika tumetoka katika uchumi unaotegemea kilimo tumekwenda katika uchumi unaotegemea huduma, asilimia 47.3 sasa ya uchumi wetu ni huduma na asilimia 28.2 tu ndio kilimo.

Lakini mipango yetu bado ni kana kwamba uchumi unategemea kilimo na tumeonyesha baadhi ya wasiwasi wetu kutokana na takwimu ambazo zimetolewa, lakini mipango ya nchi ambayo uchumi wake ambao takriban nusu unategemea huduma ni tofauti na mipango ya nchi ambayo takriban zaidi ya nusu inategemea kilimo. Bajeti hii ni mwendelezo wa bajeti zilizopita ambapo huduma ilikuwa ina mchango mdogo sana katika uchumi. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile, kutokana na bajeti hii, ni vigumu sana changamoto za sasa za nchi kuweza kujibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya madini ambayo ndio ilikuwa sekta inayoongoza kwa ukuaji, hivi sasa imekuwa ni sekta ya pili au ya tatu kwa ukuaji. Ukuaji wa uchumi sasa unategemea sekta ya mawasiliano na sekta ya mawasiliano kwa kiasi kikubwa bado haichangii vya kutosha katika mapato ya Serikali.

Kuna baadhi ya maeneo ambayo Waziri wa Fedha ameonyesha ili Serikali iweze kukusanya pesa zaidi, lakini wakati anaangalia maeneo hayo, bado eneo lenyewe la sekta ya madini bado halikuangaliwa hata kidogo na huwa tunapata wasiwasi mkubwa sana kwamba baadhi ya mapendekezo ambayo Kamati ya Rais ya kuangalia sekta ya madini iliyotoa na si baadhi mapendekezo yote hayajachukuliwa. Matokeo yake ni kwamba bajeti imeangalia zaidi kupandisha kodi za walaji, yaani *consumption tax* na kuacha kabisa kupandisha kodi kwa watu ambao ni wale wazalishaji kwa maana ya wawekezaji na wawekezaji wa ndani na wa nje ya nchi siyo wawekezaji wa nje peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumejikuta tuna chumi mbili ndani ya nchi moja uchumi wa matajiri na uchumi wa maskini. Uchumi wa masikini wanaita ni *rural economy* ambapo ndiko wanakoishi na matokeo yake ni kwamba maskini, *either* bidhaa ambazo yeye analima anazozalisha hazikui, lakini bei za bidhaa ambazo yeye anatumia zinakua.

Kwa hiyo, masikini anauza kwa bei za vijijini na ananunua kwa bei za mjini. Kwa hiyo, hali yake ya kipato ni lazima iendelee kuwa chini. Ni tegemeo la bajeti yoyote ile katika nchi yoyote ile iwapo bajeti ikitumika kama sera ya kuangalia ni jinsi gani ambavyo uchumi wa nchi unakwenda wataweza kuangalia ni jinsi gani ya kupunguza gharama hii ambayo mkulima anapata kwa ajili ya kuhakikisha kwamba anabakia na fedha ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeelezwa kwamba Serikali imeweka vipaumbele na vipaumbele vimetajwa na pesa zimetajwa kwa ajili ya vipaumbele lakini napata wasiwasi sana kwamba inawezekana kuna ukosefu wa uratibu ndani ya Serikali.

Taarifa ya hali ya umaskini ya mwaka 2007 ambayo imetolewa mwaka huu imeonyesha changamoto ambazo nchi inazo na ni maeneo gani ambayo yakitiliwa mkazo tutaweza kwenda mbele kiuchumi wenyewe wanaita *drivers of growth* na wameweka maeneo manne ambayo yanapaswa kuangaliwa na kuwekewa mikakati maalum, *transport services* ambayo ndani yake kuna miundombinu na huduma nyingine za usafiri, madini, *horticulture* kwa Kiswahili nadhani ni masuala ya maua, ukulima wa maua na utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukiangalia bajeti jinsi ilivyokaa, jinsi gani ambavyo tumegawa rasilimali zetu kidogo ambazo tunazipata haikuangalia kabisa vipaumbele hivi ambavyo taarifa ya Serikali imezitoa, taarifa ambayo ndio inafanya tathmini ni wapi ambapo tunakwenda kuhusiana na suala zima la kupunguza umasikini. Nadhani Wizara ya Fedha na Uchumi inabidi iangalie kwa sababu taarifa ya hali ya umasikini inatolewa na idara ndani ya Wizara ya Fedha na Uchumi.

Kwa hiyo, ni rahisi sana kwa idara hiyo kuondoa umaskini kuwasiliana na Idara ya Sera ya Wizara ya Fedha, kuwasiliana na Idara ya Bajeti ya Wizara ya Fedha ili kuweza kuangalia ni vipi ambavyo tunavyofanya vipaumbele vyetu, tukiamua kuweka vipaumbele kufurahisha wananchi kwa sasa huko tunakokwenda kutakuwa ni kugumu sana kwa sababu utagawa pesa kwa kila sekta, lakini zile sekta hazitachochea sekta nyingine. Kwa hiyo, kuna umuhimu mkubwa sana wa kuweza kuangalia vitu kama hivyo katika hali ya juu na ni suala lile lile la kubadili *main set*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vipi ambavyo bajeti yetu inaendana na changamoto ambazo tunazo hivi sasa? Kwanza, bajeti imeshindwa kabisa kukusanya kodi zinazostahili kwenye madini na ninashindwa kuelewa ni kwa sababau gani! Kwa sababu inafahamika wazi kabisa kwamba mwaka 1997 na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed ameielezea hapa, Bunge hili lilitunga sheria ambayo ilitoa unafuu usio na lazima kwa makampuni ya madini kwa kiasi cha asilimia 15, unafuu mbao umelifanya Taifa lipoteze shilingi bilioni 883 katika kipindi cha miaka 10 toka sekta ya madini ianze kukua katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitegemea kwamba katika *finance bill* ya mwaka huu Waziri wa Fedha angefuta kabisa sheria hiyo kwa sababu bado iko kwenye vitabu vyetu vya sheria na inafanya makampuni ya madini ambayo yana mikataba yasiweze kulipa kodi hiyo.

Kuna mashauriano ambayo Serikali imefanya na baadhi ya makampuni ya madini, lakini kama suala hili hatutalitoa kwenye sheria, halitaweza kusaidia na mfano mmoja tu wa madhara ya sheria hiyo ni kwamba kampuni ya Bulyankhulu *Gold Mine* ambayo ingepaswa kuwa imeanza kulipa kodi ya mapato haitalipa kodi ya mapato kutokana na faida yake mpaka mwaka 2019, yaani haitaanza kulipa *corporate tax* mpaka mwaka wa mwisho wa Rais wa awamu ya tano na hawa wameanza na Rais wa awamu ya tatu. Kwa hiyo, unaweza ukaona ni jinsi gani ambayo Taifa linapoteza na mabilioni ya fedha kwa sababu ya sheria ambazo tumezitunga sisi wenyewe na tunao uwezo wa kuweza kuzirekebisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2005 wakati tuko kwenye kampuni za uchaguzi Serikali ilitoa misamaha ya kodi miwili. Wa kwanza, mafuta kwamba makampuni ya madini hayatalipa kodi ya mafuta mpaka watakapomaliza kama ni dhahabu wanayochimba, kama ni almasi wanayochimba, kama ni *Tanzanite* wanayochimba na tulishauri kwamba msamaha huo ufutwe kwa sababu ni msamaha ambao hausaidii chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, msamaha huu ungefutwa ungeweza hata kusaidia kupunguza zile kodi ambazo tulizipandisha mwaka jana kupelekea mfumuko wa bei uweze kutokea. Sisi kama Tanzania hatuna uwezo hata kidogo wa ku-*control* bei ya mafuta katika soko la Dunia, lakini tunao uwezo wa ku-*deal* na kodi zetu ili kuweza kuhakikisha kwamba tunapunguza ukali wa upandaji wa bei katika soko la Dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ilipaswa kuangalia hizo kodi zetu ili ziweze kupunguza huo ukali wa maisha. Mwaka 2007/2008 aliyekuwa Waziri wa Fedha Mheshimiwa Zakia Meghji alionyesha katika sura ya bajeti kwamba Serikali itakusanya kiasi fulani cha mapato shilingi milioni 239 kutokana na marekebisho mbalimbali ya kodi, katika bajeti ya mwaka huu. Waziri wa Fedha hakuonyesha viwango mbalimbali vya mabadiliko ya kodi vitaifanya Serikali ikusanye kiasi gani? Kwa hiyo, ninadhani ni muhimu sana kuwa na mtiririko ulio sawa au *consistence* ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na hali ambayo ni nzuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, bajeti ina vitabu vinne. *Volume one* mpaka *volume four*. *Volume one* ndio inayo-*deal* na mapato ya Serikali na ninasikitika kwamba mara nyingi hatuiangalii *volume.* Ukiangalia kitabu cha kwanza cha bajeti utagundua mambo mawili. La kwanza, tunategemea sana kodi za biashara kwa maana ya *import duties*. Mabadiliko ya kodi ambayo Serikali imeyatangaza sasa asilimia 50 itatokana na *import duties*. Hii ni hatari sana katika uchumi wa sasa tunaokwenda. Tuna *East Africa Customs Union,* tunakwenda kwenye *common market*, tunasaini *EPA* ambayo itaondoa kodi mbalimbali dhidi ya *European Union,* tutapata tatizo kubwa sana kurekebisha kodi hizi. Tutajikuta tunakuja kuumia sana huko baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *revenue book* wakati Waziri wa Fedha anasema kwamba tutakusanya shilingi bilioni 58 kwa mauzo ya hisa za *NMB,* kwenye *revenue book* zinaonekana shilingi bilioni 42. Tunapopitisha bajeti tunachoangalia ni *revenue book,* ni nini ambacho tunakichukua? Ni hotuba ya bilioni 58 au ni *revenue book* ya bilioni 42? Nilikuwa ninaomba Waziri wa Fedha aweze kuliangalia hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa, kama tunataka kuongeza uzalishaji wa kutosha kwenye baadhi ya mazao ambayo tunayo ni lazima tuangalie jinsi gani ya kutoa *incentives* kwa baadhi ya mazao. Mimi nitatoa mfano mmoja. Nilitoa taarifa toka mwaka 2007 kwamba leo India wameweka *compulsory usage* ya magunia yao ya *duty* kwa ajili ya mazao yote ya India. Sisi hatujaweka *compulsory usage* ya maguni yetu ya katani, matokeo yake ni kwamba tunakuwa tuna-*export* kwenda Bangladeshi na India kwa sababu hatulindi katani yetu wala hatulindi viwanda, matokeo yake ni kwamba baadhi ya wawekezaji wamenunua viwanda, havifanyi kazi kwa sababu ya mazingira hayo ya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninaomba Waziri wa Fedha ajaribu kuangalia uwezekano wa angalau mazao mawili mahindi na korosho ziwe ni *compulsory* kutumia maguni ya katani ili ku-*stimulate* uzalishaji wa katani na kufanya viwanda vya katani ambavyo vimekufa hivi sasa viweze kuzalisha magunia ya katani na yaweze kutumika katika nchi. Vinginevyo itakuwa ni tatizo ambalo tutaendelea nalo, kutegemea kodi kutokana na *imports* ambazo madhara yake ni makubwa sana kutokana na dunia ya sasa ya *globalization*. Ni lazima kuangalia Serikali isikwepe kazi yake ya *distributive role.* Ni kazi ya Serikali yoyote duniani kukusanya kutoka matajiri kuwapeleka maskini ili kuweza kupunguza gharama za maisha yao na ndio kazi ya bajeti kama sera na siyo bajeti kama urari wa mapato na matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii nami pia niweze kuchangia hotuba zilizopo mbele yetu, hotuba mbili, hotuba ya Bajeti na hali ya Uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mustafa Mkulo pamoja na Manaibu wake Mheshimiwa Jeremiah Sumari na Omar Yusuff Mzee na pia nichukue fursa hii pia kutoa pongezi kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha bwana Grey Mgonja na Naibu wake na watendaji wake wote wa Wizara kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kutuandalia bajeti ya mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba inaelezwa kwamba ni kupanga ni kuchagua. Msemo mzuri uliowahi kutolewa na Hayati Baba wa Taifa - Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Ni msemo ambao sasa hata sisi Watanzania na sisi hapa tunautumia kwa ajili ya kuelekea katika maendeleo ya nchi yetu. Mwaka 2007 *priority* yetu katika bajeti ilikuwa ni suala la elimu na pia mwaka huu tumeendelea na kipaumbele hicho hicho cha elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kabisa elimu ni ufunguo wa maisha na ukiweza kuelimisha watu wote, wakaelimika na wakapata elimu bora, basi wataondokana na masuala ya umaskini. Lakini tuangalie fedha hizi nyingi tunazopeleka katika sekta ya elimu tunafanyia ufuatiliaji kwa kiwango gani, zinafanya kazi kwa kiwango gani? Tukiachia hivyo, tukaziacha pesa zikatengwa, pesa nyingi bila kufanya *tracking* bado tunaweza tukajikuta tunarudia mwaka hadi mwaka kipaumbele hicho hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za elimu ni muhimu sana na mwaka 2007 tangu tulipoingia katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2005/2010 tulisema tutahakikisha kwamba ni lazima tutakuwa na Shule za Sekondari kwa kila Kata. Kwa hivi sasa ni kiwango kikubwa sana kwa nchi yetu na hasa nikizungumzia mimi, kwa upande wa Jimbo langu ni kwamba tumetekeleza yale malengo yaliyozungumzwa kupitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi lakini bado yako matatizo makubwa sana ambayo yana ukosefu, kwa mfano kukosa walimu katika shule hizi, kukosa vitendea kazi sasa hatuwezi tukawa tunaendelea mwaka hadi mwaka tukapanga pesa lakini utekelezaji wake ukawa bado hauwezi kuonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia suala la kilimo. Ukiangalia kwenye Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi, katika moja ya sekta za uzalishaji, kilimo kimetajwa kama sekta namba moja ya uzalishaji. Kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu, na kilimo ndicho kilicho na watu wengi kwa Tanzania. Tunayo zaidi ya asilimia 80 ya wananchi ni wakulima.

Sasa nakubaliana kabisa kweli kupanga ni kuchagua, lakini bajeti ya mwaka huu inasema kwamba tumetenga bilioni 460 sawa na asilimia 6.4 kwa ajili ya kilimo na katika fedha hizi imeelezewa zinakusudiwa na zinaelekezwa katika maeneo yapi? Imetajwa

hapa maeneo yaliyoelekezwa fedha hizi, naomba ninukuu. Hii ni ukurasa wa 30, inasema:

"Katika bajeti ya mwaka 2008/2009 sehemu kubwa ya fedha zimetengwa kwa ajili ya kilimo, zinaelekezwa katika ruzuku ya mbolea, hifadhi ya chakula *SGR*, utafiti hasa wa mbegu bora na mafunzo."

Mheshimiwa Naibu Spika, ni sahihi kabisa hizi fedha zilipoelekezwa, kwa sababu kulingana na vipaumbele kama tutafuata ilani kama kipaumbele namba moja, ni sahihi kabisa. Lakini lipo tatizo katika namna ya mgao wa fedha hizi. Tunapozungumzia suala la mbolea tunasema kwamba sasa tunataka kufanya *modernization* ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini fedha nyingi za mbolea zimetengwa katika Mikoa nane tu, Mikoa mingine ambayo sasa hivi nasi tunafanya mapinduzi ya kilimo pesa hizo hazipo. Unapozungumzia suala la kilimo bora ukaanza na Mikoa nane hii Mikoa mingine ukaiacha, hapa bado tutakuwa hatufanyi mapinduzi ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika mgao wa fedha hizi ilikuwa ni dhahiri Mikoa yote ingeweza kuzingatiwa na tukapata fedha za ruzuku ya mbolea na wakulima wetu wa Singida wakapata ruzuku ya mbolea ili na wao waingie katika kilimo bora na wafanye mapinduzi ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika mgao wa fedha hizi ilikuwa ni dhahiri Mikoa yote ingeweza kuzingatiwa na tukapata fedha za ruzuku ya mbolea na wakulima wetu wa Singida wakapata ruzuku ya mbolea ili na wao waingie katika kilimo bora na wafanye mapinduzi ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizi kuna suala la mfuko wa pembejeo, mfuko wa pembejeo ni muhimu sana. Tumekuwa tukiandika vitabuni, tumeandika kuhusu mfuko wa pembejeo, lakini huu mfuko wa pembejeo unamfikia mkulima wa kawaida? Mkulima mdogo aliyepo Jimbo la Iramba Magharibi anafikiwa na mfuko huu? Mfuko huu unaishia kwa watu wanaouelewa na watu wa mijini, lakini hata wanapoambiwa wananchi wanahamasishwa kwamba waende wajaze fomu katika mfuko wa pembejeo wanapewa milolongo mingi kiasi kwamba wanakatishwa tamaa na hawawezi kupata huu mfuko wa pembejeo.

Kwa hiyo, kama tunahitaji kumnyanyua huyu mkulima wa hali ya chini, yaani mkulima mdogo ni kwamba lazima tuhakikishe vitu vilivyotajwa kupitia Ilani ya Chama Cha Mapinduzi mbolea, kwa ukulima wa kisasa na matumizi ya trekta, lazima hivyo vitu wakulima watumie, hapo tunaweza tukawa na kilimo endelevu na wananchi wakafanya mapinduzi ya kilimo na hivyo pato letu la taifa likaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napata taabu sana ninaopoona kilimo kinakwenda kwa baadhi ya Mikoa ndiyo inayopewa kipaumbele na baadhi ya Mikoa inaendelea kuachwa bila kuwa na utaratibu ambao unaweza kuiendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia hilo hilo katika kilimo suala la umwagiliaji. Miradi mingi sana imeletwa kwa kupitia fedha za wafadhili, lakini miradi hii sio endelevu na kila mwaka tutaendelea kutumia fedha na tunatenga pesa tunapotenga pesa bila mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ukija ukiangalia hasa katika Jimbo langu, maeneo mengi yaliyotengewa umwagiliaji na ikawekwa fedha, miradi ile imekufa na iliwekewa fedha nyingi na haijafanya kazi yoyote. Sasa sijui tutakapofika katika Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ajiandae na awe majibu mazuri kuhusiana na zile pesa zilizopotea, yaani zilizowekwa tukiambiwa kwamba kutakuwa na kilimo cha umwagiliaji, lakini fedha nyingi zikawa zimepotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la Sekta ya Maji. Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi inasema kwamba hadi tutakapofika mwaka 2010 tutakuwa kwa 65% maji safi na salama yamefika vijijini. Lakini leo hii bajeti ya Wizara ya Maji imerudi chini yaani imepunguzwa, bajeti ya mwaka 2007 ilikuwa bilioni 309.1 lakini ya mwaka huu imekuwa ni bilioni 230.6 punguzo linalofikia bilioni 78.5. Sababu zilizotolewa tunaambiwa katika kitabu hiki kwamba kutokana na ule mradi mkubwa wa maji Shinyanga kukamilika. Kwa hiyo, bajeti hiyo ndiyo maana imelazimika ipungue. Hivi napenda kuuliza kweli tutafikia hiyo 65% mpaka tutakapofika mwaka 2010? Tuna uhakika mwananchi atakuwa tayari ana uwezo wa kupata maji safi na salama kwa 65%.

Mimi ninaona ni wakati muafaka kwamba tuboreshe baada kumaliza ule mradi mkubwa sasa ilikuwa ni wakati muafaka kuelekeza nguvu vijijini ambapo wananchi bado wanatumia visima, maji machafu, bado wanachangia maji na mifugo ili sasa nguvu tuelekeze huko tuhakikishe wananchi wetu wanapata maji safi na salama. Kwa hiyo, naomba nayo atakapofika Waziri wa Maji na Umwagiliaji ukweli lazima watueleze sababu za msingi tujue tunawezaje kufikia hizo 65% hadi kufikia mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuzungumzia suala la miundombinu. Naipongeza sana Serikali hasa kwa kukamilisha barabara kwa kiwango cha lami ile ya kutoka Shelui hadi Shingida. Naipongeza sana, kazi ya barabara imekamilika na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Iramba Magharibi, nasema Serikali tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini barabara hii toka Singida imeishia Isuna na sasa tunashukuru *Contractor* yupo, sasa hivi wa kutoka Isuma kuja Manyoni, lakini kale eneo lilikobakia kidogo la kutoka Chikuyu hadi ukafika Manyoni, juzi juzi limesimama. Kwa hiyo, tunaomba Serikali imalizie hela impe yule *Contractor* wa KONOIKE pesa ili akamalizie lile kaeneo ili sasa yale manung'uniko au sisi Wabunge wa Singida kila tukifika hapa tukalalamikia suala la barabara tukaachana nalo, naiomba sana Serikali iweze kumalizia eneo hilo lililobakia hasa la Chikuyu hadi Manyoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba kweli kutokana na hata mazungumzo yaliyozungumzwa na wenzangu na hali halisi hata ya wananchi jinsi walivyozungumzia

kuhusiana na hii bajeti na kama kweli tutafuata kama ilivyowasilishwa na utekelezaji wake ukawa makini, naamini basi tutakuwa tumepiga hatua mbele zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono bajeti hii kwa asililimia mia moja ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo na msemaji watu wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Mohammed Amour Chomboh.

**MHE. JUMA ABDALLAH NJWAYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niungane na Wabunge wenzangu kutoa mchango wangu katika bajeti iliyopo mbele yetu jioni hii ya leo.

Awali ya yote, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi pamoja na Manaibu Waziri wake kwa kuleta bajeti ambayo kwa muono wangu mimi naiona ni nzuri kwa sababu imezingatia hali ya ugumu wa maisha kwa kupunguza kodi na pia kupunguza utegemezi kutoka kwa wajomba. Kwa hiyo, nitangulie kusema naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Kwa kweli nimevutiwa na taarifa ya kutengwa kwa shilingi bilioni 21 kwa ajili ya kuimarisha mtaji wa Benki ya Raslimali yaani *TIB* ili kupunguza tatizo la mikopo ya kilimo na viwanda. Mimi napongeza sana kwenye eneo hili, hongereni sana.

Lakini nina mawazo kwamba kwa kuwa natambua hizi hazitoshi kwa sababu kwa kuwa na bilioni 50 sasa hazitoshi kwa wakulima wote wa Tanzania pamoja na viwanda vyake. Rai yangu kwa Serikali ione uwezekano wa kufanya mashauriano na mabenki mengine ambayo yana hisa nayo ili kuhakikisha kwamba wakulima wa Tanzania wanakopeshwa. Utaratibu uliopo sasa unawanyanyapaa wakulima bure. Kuna haja ya kufanya jitihada za makusudi hapa ili wakulima wale wakopeshwe. Mazingira yakiwekwa vizuri wakulima wanakopesheka na wanalipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mfano mzuri tu. Hela hizi za bilioni moja maarufu kwa jina la JK, kwangu kule Tandahimba na Newala wamelipa wakulima kwa zaidi ya 80%. Lakini huko nyuma kazi ilikuwa ooh, hawakopesheki, hawakopesheki! Mbona hii wameweza kukopesheka? Hapa cha msingi ni kuwawekea mazingira mazuri na utaratibu ukiwekwa wananchi hawa wanakopesheka, hakuna shaka.

Kwa kweli kwa sababu ya kutoweka mazingira mazuri ya wakulima hawa kukopesheka ndiyo maana baadhi ya mazao ya kilimo yamepungua. Nichukulie mfano wa korosho kwangu, maana mimi natoka kule na kwetu siasa ni korosho. Liko tatizo, unakuta mkulima akienda Benki kukopa anaambiwa hawezi kukopeshwa kwa sababu mbalimbali zinazosemwa. Lakini mnunuzi wa korosho anakopesheka, hivi sasa kama mkulima huyu asipolima hizo korosho huyu mnunuzi atanunua korosho za nani? Naomba Serikali ibadilike katika hilo tuweke mazingira mazuri kwa wakulima wetu ili kilimo chetu kilete tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, raslimali zinazotumika kama dhamana hapa duniani mara nyingi ni majumba, mashamba au kwa ujumla niseme ardhi. Lakini kuna tatizo kubwa hapa kwetu. Wakulima kule wanapima maeneo yao ya mashamba, taasisi za Serikali, Mawakala, Mashirika ya Umma leo yakienda Wizara ya Ardhi na Makazi kupata hati, yaani *Certificate of Occupancy* za raslimali hizo inakuwa tatizo. Mimi naomba kwa kuwa sasa tumechelewa, basi bajeti ijayo tulete mkakati wa maana hapa hivi ndivyo vitu vitakavyosaidia kujenga uchumi imara kwa wananchi wetu. Utaratibu wa sasa uliopo pale Wizara ya Ardhi na Makazi kuhusu hati hautusaidii Taifa letu, tubadilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyotangulia kusema awali siasa kwetu ni korosho na maji. Kwanza nataka nitangulie kuipongeza Serikali ya awamu hii kwamba imesaidia sana kupunguza tatizo la kuibiwa wakulima wa korosho kule kwetu. Nampongeza Mkuu wa Mkoa wetu, Kanali Mstaafu Anatory Tarimo, Ma-*DC* wote wa Mkoa wa Mtwara, Viongozi mbalimbali pamoja na Wabunge wa Mkoa wa Mtwara kwa ushirikiano mzuri tuliouonyesha hadi kuwasaidia wananchi wetu wale. Lakini nitafanya makosa sana nisipomtaja Mheshimiwa Stephen Masatu Wasira, maana mchango wake nao ulikuwa mkubwa sana. *(Makofi)*

Baada ya hayo yote, rai yangu basi, kwa sababu Wakulima wale wamelelewa utaratibu huu tusiendelee kuwalipa nusunusu. Kwenye msimu ujao tuwatengenezee mazingira ya kupata *full payment.* Ile *bonus* ndiyo walipwe baadaye kwa sababu wanapolipwa *full payment*, itawasaidia kupanga bajeti yao vizuri ni kama vile Serikali ilivyofanya kuwaomba wafadhili walete kwanza kwenye kapu ndiyo tupange bajeti na wao tuwatengenezee mazingira ya kuweza kupanga bajeti yao sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba ni-*declare interest*. Mimi ni Mwenyekiti wa Bodi ya Maji ya Makonde, lakini mara nyingi huwa nachelea kusema kwa wapiga kura wangu kwa sababu kwanza inakuwa ni aibu, aibu kuwa Mwenyekiti wa Bodi ambayo haina maji. Kaka yangu Mheshimiwa Mark James Mwandosya amejionea mwenyewe hali hiyo maana wiki mbili zilizopita tulikuwa wote pale lakini mimi nasema natambua mikakati ya Serikali katika kupunguza tatizo la Maji Jimboni kwangu, Jimbo jirani la Newala, Masasi na Mtwara vijijini. Sasa mikakati hiyo ni *long term* bado haitusaidii tatizo tulilonalo mkononi ni kwamba sasa hatuna umeme na hivyo hatuwezi kupata maji.

Maji haya ndiyo kitu cha msingi kwenye maisha yetu ya kiubinadamu lakini pia kama nilivyosema, zao letu kubwa kule ni korosho kwa sasa ili uweze kupulizia korosho zinahitaji maji. Kwa hiyo, kwa ajili ya kujenga uchumi wetu maji yawepo pale, kwa ajili ya maisha yetu maji yawepo pale. Mimi naiomba Serikali ichukue jitihada za makusudi sasa kufanya mpango wa dharura kwenye bajeti hii ili tuhakikishe tunapeleka majenereta pale Masasi ili tuweze kupata umeme unaoweza kusukuma maji kule.

Mheshimiwa Juma H. Killimbah hapa ametaja ilani, nami nataka nikariri pia Ilani yetu ya Uchaguzi inatuelekeza kwamba tutaboresha huduma ya maji kwa 65% vijijini.

Lakini katika hali iliyopo sasa haipendezi sana na haishawishi kwamba ilani hiyo tunaitekeleza ipasavyo na hasa ukitilia maanani kwamba hata bajeti imepunguzwa. Nilidhani, kwa sababu ya umuhimu wa maji bajeti ya maji ingepewa kipaumbele zaidi nadhani tu–*reconsider* hii bajeti na hasa kwenye kipengele cha maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala la pango ya majengo. Nimekuwa nafanya utafiti wa kirahisi rahisi nimekuja kubaini kwamba taasisi nyingi za umma, mawakala na Serikali kwa ujumla imekuwa ikitumia majengo ya kupanga kuendesha shughuli za kila siku za Serikali. Nafikiri sasa tubadilike Serikali inapata hasara isiyo ya lazima kwenye mapango ya majengo.

Kuna mahali nimekuta wamekarabati jengo kwa milioni 700. Hivi milioni 700 si unajenga jengo lako tu ukaachana na ukarabati na kulipalipa pango? Hili suala la kupanga tuachane nalo, tujenge majengo ya kwetu maana kwa mfano baadhi ya mawakala wanatakiwa wakusanye mapato yao kwa mwaka baadaye walete ruzuku Serikalini lakini wakiwa na jengo la kwao, tayari umeshapunguza tatizo na tunapata ruzuku nzuri tu hapa ya kupeleka Serikalini! Mimi naomba jambo hili tuliache sasa tutengeneze mkakati wa kuhakikisha majengo yetu tunayajenga na tunayatumia ipasavyo na pale ambapo inaweza kusaidia kulete pato la Taifa, basi lisaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti Mheshimiwa Naibu Waziri amejaribu kuleta hoja ya kuimarisha na kujenga uwezo wa wataalamu kuwafanya wanunuzi wa umma. Mimi kwa kweli naomba nimpongeze katika hili na hasa kwa kutambua kwamba matumizi ya Serikali karibu zaidi ya 80% yanatumika kwenye manunuzi ya vifaa na huduma. Ombi langu au rai yangu kwa Serikali isimamie kwa umakini Kanuni zilizowekwa na ziwabane wasiozifuata.

Utaratibu uliopo wa kuweka Kanuni pale lakini haubani siyo *water tight* kwa wadau hautusaidii ndiyo unaotuletea matatizo na tumejifunza hapa mwezi wa nne. *PPRA* ilitoa ushauri mzuri tu wa kitaalamu kwenye suala la *Richmond* haukufuatwa. Kwa hiyo, tusipoendelea kufuata tutaendelea kuleta matatizo kwenye nchi yasiyo na sababu, Kanuni zifuatwe.

Lakini pia mwaka 2007 nilipokuwa nachangia mchango hapa nilisema kwamba wataalamu hawa wa ununuzi na ugavi sasa waandaliwe *directorate* yao kwa sababu tatizo kubwa lililopo ni viongozi wa juu wanaowaongoza hawa wanawalazimisha kufanya vitu ambavyo ni kinyume na miiko ya ununuzi wa umma matokeo yake kwa sababu ni wakubwa wao, wanaingia kwenye mitengo inayosababisha *audit query* na athari kwa nchi.

Kwa hiyo, tukiwatengenezea *directorate* yao watakuwa wanawajibika kwanza kwenye *directorate* hiyo lakini kwa sababu watakuwa *at per* na *DAP* ambaye ni Mkurugenzi na Utawala na Mimi Mkurugenzi wa Ugavi na Huduma hapa tunaongea kauli moja siyo ya kumdhalilisha mwingine na kumlazimisha kufanya mengine ambayo sio lazima ayafanye maana anamwambia Bwana hivi *codes* za kazi yangu au wajibu wangu hauniruhusu hivyo na wataheshimiana hapa. Lakini inapokuwa mkubwa anamtawala mdogo, basi wanalazimisha na mambo yasiyo na haki na utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la uwanja wa ndege wa Mtwara. Uwanja huo ni wa kihistoria na umechangia sana ukombozi wa nchi mbalimbali zilizoko Kusini mwa Bara la Afrika. Uwanja huo sasa najua unakarabatiwa lakini unakarabatiwa katika kasi ndogo na ningeomba nishauri hapa kwamba uwanja huo uandaliwe sasa kuwa uwanja wa kimataifa. *(Makofi)*

Nasema uwanja wa kimataifa kwa sababu mazingira yaliyopo sasa ya Mji wa Mtwara huu mji unakua. Mheshimiwa Mrope alipokuwa anachangia ameeleza vigezo vyote na kila bahati Mwenyezi Mungu alizotaka kuzionyesha kwa mji wa Mtwara, gesi ipo pale, Bandari ipo pale na katika hali iliyopo yapo mengi ambayo tu najua haijafika wakati wake lakini kuna fununu tunazisikia kwamba suala la kutumia Bandari ya Mtwara liko njiani muda si mrefu. Kama hivyo ndivyo, mji utapanuka ule, wageni watakuwa wanafika pale, itakuwa *entry point* ya mambo mengi. Kwa hiyo, nawaomba tutengeneze mazingira mazuri ya uwanja ule kuwa wa kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi jioni hii, nasema tena naonga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMMED AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na mimi naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kupata nafasi hii jioni hii nikatoa mchango wangu kuhusiana na hotuba hii ya uchumi na bajeti ya mwaka 2008/2009.

Nianze kwa kumpongeza Waziri Fedha na Uchumi na Manaibu Waziri wake na timu nzima ya Wizara ya Fedha na Uchumi. Katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri inayohusiana na mambo ya mwelekeo wa uchumi na bajeti ya fedha kuna mambo mengi mojawapo ya yaliyojitokeza ni maboresho ya mfumo wa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba hii nataka kuchangia katika kifungu ambacho kinahusiana na kurekebisha viwango vya ushuru wa bidhaa katika huduma za simu kutoka 7% mpaka 10%. Ni vizuri kwa sababu ni sehemu ambayo itaongeza pato au kodi katika mfuko wetu wa bajeti hii.

Sasa nitakwenda zaidi ya hapa ambapo walikusudia hasa kuhusiana na haya makampuni ya simu. Kampuni za simu zilipaswa au Wizara ya Fedha ilipaswa kwenda ndani zaidi ya hapo walipofikia, lakini sio zaidi ya hapo kwa upande wa watumiaji ilikuwa kwa kampuni zenyewe. Kampuni za simu zinafanya faida kubwa sana na ukiangalia hayakuwekeza kitu hata kidogo cha kuweza kuendeleza uchumi na faida kwa nchi hii zaidi ya kujenga minara yao minara ambayo kwa wao ni kama mfano wa mwiko wa kusongea ugali, lakini ugali wenyewe wanachukua wote wao wenyewe na ndiyo maana ukiwapeleleza kwamba hawaoni shida wao kujenga minara popote pale, lakini hawana jambo lolote la kitega uchumi zaidi ya kuweka kule minara. Duniani kote kampuni kama za simu, mafuta, madini ndiyo zinazojenga uchumi wa nchi.

Kampuni kama *Vodafone* ina majengo makubwa makubwa Afrika Kusini. Hata hapa hawana hata jengo moja zaidi ya kukodi. Kuna mashirika kwa mfano shirika letu la *NSSF* wanachama wake hawafiki hata milioni nne, lakini kampuni ya *Vodafone* inasema kwamba familia yake sasa hivi ni milioni nne na hiyo ni wao tu. Lakini kampuni moja kama hiyo inachangiwa na kila mtu na kila kampuni nyingine kwa sababu kuna *interconnection*. Katika fedha yote wanayoipata ile hakuna hata moja ambayo wanaweza angalau wakajenga jengo lao kwa mfano hili ni *Vodafone House*, hakuna! Huo ni mfano tu, lakini hakuna hata kampuni moja labda *TTCL*!

Kampuni kama ya *Mobitel* ambayo inaitwa *mic Tanzania* ilianza kama *Mobitel*, ikaja *Buz* na sasa *Tigo* ni kampuni hiyo hiyo. Jengo gani ambalo linaitwa hili ni *Mobitel House*? Hizi kampuni zinachukua fedha zote kupeleka kwao hawawekezi hata kitu kimoja hapa kwa hiyo kulikuwa na mpango mzuri tu ingekuwa Serikali inaliangalia hili kwa makini zaidi, mimi nina wasiwasi hata kama *TRA* wanafanya ukaguzi wa hesabu zao na ni rahisi sana kuweza kufanya ukaguzi wa hesabu hizo kwa sababu katika mtiririko wa kozi zote zile au *traffic* zote zinajirekodi na utajua kwamba kampuni fulani imeingiza kiasi fulani kwa kipindi fulani kwa hiyo inapaswa kulipa kodi kwa kiasi fulani, siyo kuwakamua wapiga simu. Hii naona kidogo itakuwa nzito zaidi kuliko kuwakamua hao wapiga simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu najua nimefanya na Kampuni ya *Mobitel* kwa miaka mitano, najua wanapataje pesa. Wao wanatuuzia sisi *air time,* wao wananunua kutoka wapi wakatuuzia sisi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa endelea tu.

**MHE. MOHAMMED AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Wanachotuuzia sisi ni *air time* wao wanakodi *frequency* kutoka *TCRA* na kulipa leseni ya biashara. Sisi tukinunua ile *voucher* tunalipia gharama ya utengenezaji, gharama ya kodi ya ushuru, lakini wao wanaipata ile *cream* wanakwenda nayo kwao. Ndiyo maana nikawaambia kwamba wanachotufanyia sisi kutubabaisha kutupa lambalamba kutufanyia bahati nasibu hii.

Leo *promotion* hii ni kwamba hakuna chochote! Hatutaki hiyo! Tunataka watoe gawio fulani liingie katika uchumi wa nchi hii na ndivyo wanavyofanya makampuni kote duniani. Wajenge majengo hapa, tujue kesho na keshokutwa wakiondoka wametuachia kitu ambacho tuna uwezo wa kupata ajira pale kwa sababu jengo moja kujenga *blocks* ni watu wangapi watapata ajira kutoka pale? Lakini leo wanatujengea minara hii, wakimaliza wanaondoka zao wanatuachia minara kila mahali ukija kutoka Dar es Salaam kuja hivi kuna mji kama pale Dakawa kuna minara mitano sehemu moja na ukiona bango kubwa kabisa katika nchi hii, basi ni la kampuni ya simu. Lakini tunapata nini? Wanachukua ugali wote wanatuchia sisi mwiko tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea, nakuja kwenye suala la masoko. Nafikiri tumefika wakati sasa Wizara ya Biashara na Viwanda iweze kutafakari sana masoko ambayo yanaweza yakawanyanyua watu wetu na wakulima wetu ndani ya nchi na nje ya

nchi. Kwa sababu Tanzania tuna vitu vingi sana ambavyo vinahitajika nje ya nchi yetu na vinaweza vikaingiza pato kubwa sana katika nchi yetu. Hatuna viwanda lakini tuna vyakula ambavyo vinahitajika kwa mfano matunda na masoko yapo lakini tatizo ni kwamba tuna mipango mizuri lakini utekelezaji wetu haupo sijui kwa nini sasa imefika wakati sasa hivi tuache tena kupigapiga vinanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa mfano mmoja kwa ruhusa yako huu mziki wa taarabu asili yake kwa hapa kwetu Tanzania ni mziki wa mwambao hasa sehemu za kwetu Zanzibar. Taarabu asilia yake ni kwamba hupigwa vinanda na mwimbaji akakaa mbele watu wamekaa kwenye viti wanatoka mmoja mmoja kwenda kutunza taratibu. Lakini imefika wakati sasa hivi wameona kwamba mtindo ule wa taarabu haupo. Sasa hivi watu hawakai tu kwenye viti wanahemkwa tu wanakwenda kucheza. *(Makofi)*

Maana yangu ni kwamba suala la kukaa tu na kupiga *story* tu hapa imepitwa na wakati lazima tuifanye *in reality* yale mambo tunayoyapanga tuyafanye sasa hivi tuingie uwanjani tutekeleze. Hayo mambo ya vinanda vinanda yalikuwa zamani na sasa hivi mpaka wenzetu wa Bara wameshahemkwa na taarabu. Sasa siyo wa mwambao tena, iko mpaka Njombe, Tabora, Kagera na kadhalika. *(Makofi)*

Mimi nafikiri tuna haja ya Wizara ya Biashara na Masoko kuweza kuyaendeleza masoko yetu kwa ajili ya kuwanufaisha wakulima wetu hasa wakulima wa matunda, kuna soko zuri sana katika nchi ya Ghuba na uwezekano wa kufikisha kule upo. Zinakuja ndege kutoka Ghuba zinakuja na *full cargo* tuna *import* tu lakini hakuna *export* ndege zinaondoka tupu, tuna ndizi, machungwa mananasi, lakini hatufikishi na yanahitajika sana tu, lakini na Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Wizara ya Biashara washirikiane namna ya kuweza kuwaelekeza wakulima wetu ili wafanye yale mambo ya namna ya kuweza kusafirisha na hasa hasa Idara ya masoko nasikia kuna kituo cha masoko cha Wizara ya Biashara kiko Dubai kinafanya nini? Ukienda kule unakuta bidhaa kutoka Kenya. Leo hii imefika hadi Tanzania, sisi hapa, mimi juzi nimeshangaa! Nimefika Mombasa kuna maembe yanatoka Mombasa yanakuja Tanzania. *You can't imagine* sasa hivi tumefika hali hiyo! Pale Dar es Salaam zimejaa embe tele zinatoka Mombasa. Ardhi yetu inaota kila kitu!

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye suala hili la Tume ya Pamoja ya Fedha. Tume ya Muungano ya Fedha, hii *story* imekuwa ya siku nyingi na ndiyo yale niliyoyasema kwamba sasa hivi mambo ya vinanda hatutaki tena, tunataka machezo. Huu ni mwaka karibu wa tatu sasa, mimi toka kuwepo Bungeni hapa Tume hii kila siku inazungumzwa, mpaka lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachotaka ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Muungano tumalize suala hili tukae tujue ni namna gani tutagawana mapato yetu ikiwa ni ya gesi, petroli na kama kweli kuna harufu ya petroli, sasa hivi tuweze kufanya haya mambo tunufaike. Siyo watu wa kulalamika kwamba petroli imepanda bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna gesi nzuri na magari yanaweza kutumia gesi, lakini tunalalamika petroli, ya kazi gani? Tunasikia kuna harufu ya petroli, lakini kwa sababu Tume haijakaa tukajua tutagawanaje, mpaka lini? Tunalia umaskini na nchi yetu tuna kila kitu! Hii hata Mungu atakuja kutupiga laana. Maana wewe kitu unacho, halafu unalia kwamba bado wewe ni masikini. Umasikini wetu uko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mimi ni kitinda mamba, nafikiri muda bado?

**NAIBU SPIKA:** Endelea umeambiwa una kengele yako. Endelea!

**MHE. MOHAMMED AMOUR CHOMBOH:** Nafikiri sina la ziada, isipokuwa naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani siku ya leo tumeimaliza vizuri. Nawapongeza wachangiaji wote na waliotoa michango yao nadhani tumefurahi wote. Kwa hiyo, kilichobaki sasa ni kwamba tukapumzike ili kesho tuweze kuendelea na kazi yetu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(*Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne tarehe 17 Juni, 2008 Saa Tatu Asubuhi*)